# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 7 Juni, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**MHE. LEAH J. KOMANYA K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, sasa aulize swali lake.

Na. 343

### Kuipandisha Hadhi Zahanati ya Kijiji cha Sojo - Bukene

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuipandisha hadhi Zahanati ya Kijiji cha Sojo ili kiwe Kituo cha Afya na kuweza kuhudumia wananchi na watumishi wa Mradi wa Bomba la Mafuta?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jummane Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Sojo ni moja kati ya vijiji saba vya Kata ya Igusule yenye wakazi 23,237. Kata hii ina zahanati moja iliyopo katika Kijiji cha Sojo ambayo inaendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kwenye Kata ya Igusule.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru sana kwa jibu zuri sana lililotolewa na Mheshimiwa Waziri na nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu Sita, chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea na kutupatia shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya pale Sojo Igusule.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu ni kwamba Mheshimiwa Waziri, utakuwa tayari baada ya Bunge hili la bajeti uongozane na mimi kwenda Kijiji cha Sojo ili wananchi wa Sojo Igusule wakakushukuru kwa kutupatia shilingi milioni 500 za kujenga kituo cha afya ambacho tulikuwa tunakihitaji sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Zedi amekuwa akifuatilia sana juu ya ujenzi wa kituo hiki cha afya na Serikali sikivu ya Awamu wa Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, imewasikia wananchi wa Jimbo la Bukene, na kituo hicho kitakuja na niko tayari kuongozana nawe kwenda Sojo ili wananchi waweze kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kutoa fedha kwa ajili ya kituo cha afya hicho. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mchakato wa upandishaji hadhi wa zahanati zetu kwenda vituo vya afya unafanywa na Wizara; je, Wizara haioni sasa mchakato huu mkaziachia Sekretarieti za Mikoa ifanye kazi hiyo kwa vigezo vilevile ili kupunguza huo urasimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilai Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upandishaji hadhi wa zahanti kuwa vituo vya afya au kuwa hospitali za Halmashauri unafanya na Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo Halmashauri wanafanya tathmini kulingana na vigezo, wanawasilisha mikoani kwa *RAS* na wanawasilisha Wizara ya Afya, lakini pia Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utaratibu huu ni shirikishi haifanyi Wizara pekee yake ni ngazi zote zinahusika na tutaendelea kufanya hivyo kwa sababu ndiyo maana ya *D by D.* Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 344

**Ujenzi wa Stendi ya Kisasa katika Mji wa Manyoni**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imekwishaandaa wazo mradi *(concept note)* kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa kimkakati wa *stand* ya mabasi. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kutafuta msanifu wa mradi kwa ajili ya kuandaa michoro ambayo itawezesha kujua gharama halisi za mradi huo. Kazi hii ya usanifu inatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata gharama halisi za mradi huo na kukidhi vigezo vya mradi wa kimkakati, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuutekeleza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa nimeliuliza hili swali mara mbili hapa Bungeni na majibu ya Serikali yamekuwa kwamba Halmashauri bado haijawasilisha andiko; na kwa kuwa tayari Waziri ana taarifa kwamba kuna andiko ambalo limeshaandikwa, lakini limechukua muda mrefu.

Sasa je, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba inaweka mkakati wa kuzisaidia Halmashauri zote nchini

ambazo zinahitaji kuja na hii miradi ya kimkakati ili ziwasilishe hii miradi kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Waziri yupo tayari kuambatana nami kwenda katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ili akajionee hali halisi ya stendi ya mabasi ambayo ipo? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Chaya amekuwa akifuatilia sana sana miradi ya maendeleo kwa wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki ikiwemo *stand* hii na ni kweli ameuliza hapa mara pili. Na nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kwamba andiko hili limekuwa likisubiriwa kwa muda mrefu na sasa tunatoa maelekezo kwa tarehe hiyo ambayo wameji-*comment* tarehe 30 Juni, lazima andiko liwe limefikishwa hapa ili Serikali ifanye tathmini na kuona namna ya kuwaletea wananchi wa Manyoni maendeleo.

Mheshimiwa Spika, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda Manyoni, tutakubaliana baada ya Bunge hili tuweze kwenda kuona *stand* hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Katika Manisapaa ya Mtwara Mikindani, *stand* ya mabasi makubwa iliyopo eneo la Chipuputa hali ya miundombinu yake ni mbaya, mvua ikinyesha maji yanajaa

wasafiri wanapata shida. Nataka kujua tu kauli ya Serikali, watarekebisha lini ili *stand* ile iweze kutumika kwa matumizi ambayo yamekusudiwa? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tunza Malapo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Tunza kwa kufuatilia maendeleo ya wananchi wa Mtwara, lakini nimhakikishie kwamba tumetoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri zetu kuhakikisha yale maeneo ambayo ni vipaumbele ambayo yanagusa moja kwa moja maslahi ya wananchi zikiwemo *stand,* kufanya tathmini kuona uwezekano wa kufanya matengenezo kwa kufanya mapato ya ndani au kuandika maandiko maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani kufanya tathmini hiyo au kufanya matengenezo au kuleta maombi kwa ajili ya kufanya kupitia Serikali Kuu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mbogwe inazo *stand* mbili, lakini hali yake ni mbaya sana hasa mvua ikinyesha, mabasi huwa yanapata shida kupita.

Je, ni nini kauli Serikali kuweza kuzikarabati *stand* hizo ili zikae kwenye *standard?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Maganga kwa namna anavyowasemea wananchi wa Mbogwe. Lakini nitoe maelekezo kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe afanye tathmini ya gharama zinazohitajika kufanya matengenezo kwenye *stand* hizi mbili ambazo ni chakavu sana ili tuone kupitia mapatao ya ndani wanaweza kufanya matengenezo, lakini kama mapato ya ndani hayatoshelezi basi waweze kuwasilisha maandiko ya kimkakati Serikali itafute fedha kwa ajili ya kutengeneza *stand* hizo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Mji wa Kibara ndiyo makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi hatuna *stand* ya mabasi. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge wa Jimbo la Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Kajege kwa kazi nzuri na kubwa anayowafanyia wananchi wa Mwibara, lakini nimuelekeze Mkurugenzi na Halmashauri kwa ujumla kuainisha eneo hili kama ni eneo la kimkakati na kwamba ni mahitaji ya Halmashauri ili kuona uwezekano wa kupata *stand* katika eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi; kwa kuwa *stand* nyingi inakuwa unaingia tu kwa kuwa huna la kufanya lakini hazina mwelekeo wa *stand;* kwa nini Serikali haiji na *model stand* kwa Makao Makuu ya Mikoa zikafanana zote kama vile ilivyo vituo vya polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze kwa kazi kubwa anayoifanya kuwasemea Watanzania kwa ujumla wake, lakini Serikali tulishatoa maelekezo na *standard drawings* za *stand* za ngazi ya Halmashauri, Mikoa lakini na majengo mengine. Kwa hiyo suala hili tunaendelea kuliboresha, kumekuwa na utofauti, kati ya mikoa na mikoa, lakini tumeshatoa sasa utaratibu ambayo ile michoro yote itakuwa inafanana. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuwa usafirishaji wa abiria ni jambo la muhimu kwenye nchi yoyote yenye ustaarabu.

Je, Serikali haioni ni muda sahihi sasa wa kuhakikisha wanatengeneza mkakati maalum wa kuzijenga *stand* kwenye miji inayoendelea ikiwemo Mlandizi ili kuachana na mipango ya mradi wa kimkakati ya Halmashauri isiyotekelezeka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mwakamo kwa ambavyo anawakilisha ipasavyo wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini, lakini Serikali ilishaweka mkakati tayari wa kujenga *stand* katika maeneo yote ambayo yanahitajika na ndiyo maana tunatekeleza kwa njia ya aina mbili; moja kwa mapato ya ndani ya Halmashauri kwa gharama zile ambazo zinafikika lakini kwa kutumia miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mkakati tayari upo na tunaendelea kuutekeleza, suala ni Halmashauri pia kuhakikisha kwamba wanawasilisha mahitaji hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, *stand* ya Lindi Manispaa bado haiko vizuri, mabasi yote yanayotoka Mtwara, Songea na mkoa mzima kwa ujumla yanapitia pale.

Je, Serikali ina mkakati gani kujenga *stand* ile kuu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Tecla Ungele, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ungele amekuwa ni miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge ambao wanawasemea sana wananchi kwa Watanzania kwa ujumla na wananchi wa Mkoa Lindi, naifahamu sana *stand* ya Manispaa ya Lindi kwa sababu nimekuwa kule kwa miaka kadhaa, ninafahamu kwamba tunahitaji kuijenga, tuotoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, kutambua hii ni kipaumbele cha Halmashauri kufanya tathamini ya gharama na kuona kama inaweza ikajengwa kwa mapato ya ndani au wawasilishe kama mradi wa kimkakati. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaelekea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge sasa aulize swali lake.

Na. 345

**Changamoto ya Upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa Jimbo la Nkenge**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, ni lini wananchi wa Jimbo la Nkenge ambao hawajapata Vitambulisho vya Taifa au Namba za Usajili watatambuliwa kama raia wenye haki na kupatiwa vitambulisho hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi ikiwemo wananchi wa Jimbo la Nkenge. Katika Mkoa wa Kagera jumla ya wananchi 1,009,653 wamesajiliwa na kutambuliwa baada ya maombi yao kuhakikiwa. Jumla ya vitambulisho 310,847 vimezalishwa kwa ajili ya wananchi wa mkoa huo. Katika Wilaya ya Misenyi inayojumuisha jimbo la Nkenge wananchi 85,439 wamesajiliwa na kutambuliwa na jumla ya wananchi 32,235 wamepatiwa Namba za Utambulisho ambazo wanazitumia katika kupata huduma mbalimbali. Aidha, vitambulisho 24,694 vimezalishwa na kugaiwa kwa wananchi wa Wilaya hiyo. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa nafasi, na naipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini ndani ya muda mfupi wameweza kutengeneza vitambulisho. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Wilaya ya Misenyi kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, imetengeneza vitambulisho 24,000 lakini mpaka sasa ni vitambulisho 5,000 vimegawiwa kwa wananchi. Shida kubwa ni kwamba wananchi wanatakiwa kuhakikiwa kwa mara nyingine, hii imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Misenyi na hivyo wananchi kuona kwa kweli kuona kwamba sio sahihi kuhakikiwa mara ya pili.

Je, ni nini tamko la Serikali kuhusiana na usumbufu huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sasa kuna baadhi ya wananchi ambao walikuwa hawajafikiwa kwa ajili ya kujaza

fomu kwa ajili ya kupata vitambulisho ikiwa ni pamoja na wale ambao wamefikisha umri wa miaka 18 ambao wametiza sasa vigezo sasa vya kupata vitambulisho.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha na wananchi hao wanafikiwa kwa ajili ya kupata vitambulisho? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kyombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu idadi ndogo ya wananchi waliogaiwa vitambulisho 5,000 tu kati ya wananchi 24,694 ambao vitambulisho vyao vimetoka, nitoe tu maelekezo kwa wenzetu wa *NIDA* Mkoa wa Kagera na hususan Wilaya ya Misenyi kwamba wakati wanawahakiki mwanzo mpaka vitambulisho vinatoka bila shaka walikuwa wamejiridhisha. Hata hivyo, pale ambapo kuna mashaka kwamba huenda wanaokwenda kutoa vitambulisho siyo raia wa Tanzania wana haki ya kufanya uhakiki mara ya pili; lakini uhakiki huo usiwe sehemu ya usumbufu kwa wananchi kwa sababu haieleweki kwa nini wananchi 5,000 pekee kati ya 24,000 ndiyo wapate. Kwa hiyo, waharakishe uhakiki huo ili wanaostahili kweli waweze kupewa vitambulisho vyao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la mkakati wa Serikali, tumelijibu kwa nyakati tofauti kwamba tulikuwa na changamoto ya kimkataba kati ya Serikali na Mkandarasi, lakini changamoto hiyo imemalizwa na mkataba umeuhishwa mwezi Machi, 2022; kwa hiyo, wakati wowote kuanzia sasa vitambulisho vingine vitazalishwa na watu wengine ambao wamefikisha miaka 18 wataendelea kutambuliwa kwa madhumuni ya kupewa vitambulisho vyao. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kuna wanafunzi wa Shule za Sekondari ambao wamekuwa wakimaliza shule na wanazaidi ya miaka 18. Je, nini mkakati wa Serikali kutoa elimu katika shule mbalimbali ili wanafunzi wanapomaliza waliozaidi ya miaka 18 waweze kupata vitambulisho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baadhi ya wanafunzi huitimu masomo yao wakiwa na zaidi ya miaka 18 na wanafunzi wa aina hii wana haki ya kupewa vitambulisho. Kwa hiyo, pengine tutashirikiana na Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI ili elimu ya uraia ikiwa ni pamoja na nafasi ya kuwa na vitambulisho kutolewa mashuleni, lakini wanafunzi hawa ni sehemu ya jamii kule ambako elimu inatolewa kwenye jamii kwa ujumla wake kupitia redio, televisheni na kadhalika wanaweza pia wakapata elimu hiyo. Kwa hiyo, nadhani halitakuwa tatizo kubwa sana litatekelezwa. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, wananchi wanaoishi Visiwa vidogo vidogo Jimboni Ukerewe wanalazimika kusafiri kwenda Makao Makuu ya Wilaya kufuatilia vitambulisho vya *NIDA* jambo linalopelekea usumbufu na gharama kubwa.

Nini mkakati wa Serikali kuwapelekea huduma lakini wakati huo huo ikiwaondolewa usumbufu wa wananchi hao? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuwapunguzia usumbufu hawa wananchi wanaokaa mbali na makao makuu wakiwepo hawa wa visiwani, vitambulisho hivi vimepelekwa mpaka ngazi ya Kata ili maofisa wetu kwenye ngazi ile aweze kuwagawia wananchi wao, nadhani kwa kufanya hivyo tutakuwa tumepunguza usumbufu wa wananchi. Naomba niwaelekeze wenzetu wa Ukerewe kama lipo tatizo la kuwataka wananchi wote wasafiri kwenda Nansio warekebishe ili vitambulisho hivi wavipate kwenye Makao Makuu ya Kata zao. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wengi wanapata tatizo na eneo hili la uhakiki kwa ajili ya kupata hivyo Vitambulisho vya Taifa. Sijui Serikali inasemaje kuhusu muda hasa ni muda gani ambao uhakiki unachuku ili wananchi waweze kupata vitambulisho vyao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhakiki hautakiwi kuchukua muda mrefu sana, lakini tunafanya uhakiki ili tujiridhishe kwamba

wanaopewa vitambulisho hivi ni raia wa Tanzania. Kwa hiyo, itakapotokea taarifa yoyote hasa wananchi wakatia mashaka juu ya mtu aliyetambuliwa inabidi tufanye uhakiki kujiridhisha.

Sasa juu ya muda gani itategemea pale itakapokamilisha, lakini aombe maafisa wetu wasichukue muda mrefu kwa sababu wanapaswa kushirikiana na vyombo vingine vikiwa Kamati za Usalama za Wilaya na Idara za Uhamiaji ili kujiridhisha na kumpa jibu yule ambaye anatafuta kitambulisho. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, hivi karibuni tumemuona Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akifanya mazungumzo na viongozi mbalimbali wa vyama vya upinzani kwa ajili ya kuleta maridhiano na mshikamano ya nchi yetu.

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kueleza na kuwasihi wananchi wa Tanzania waliopo nje ya nchi ili waweze kurejea hapa nchini na kushiriki ujenzi wa Taifa?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la msingi linahusu upatikanaji wa vitambulisho. Lakini swali lililoulizwa hapa ni la msingi sana, kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri sina uhakika una majibu hapo, labda nikupe muda kwa sababu ni jambo ambalo limeshazungumzwa zungumzwa sana.

Kwa hiyo, pengine nikupe muda ukayatafute hayo majibu, halafu utakapokuwa tayari utaniambia hapa mbele kipindi hiki cha maswali kabla hakijaisha kama unayo utayaleta; kama itakuwa sivyo basi utaniambia yapo tayari halafu mimi nitatoa fursa kwa ajili ya kumjibu swali hili ambalo limekuwa likizungumzwa zungumzwa sana. *(Makofi/ Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaelekea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea sasa aulize swali lake.

Na. 346

**Mustakabali wa Maeneo ya Wananchi wa Kipunguni – Dar Es Salaam**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya wananchi wa Kipunguni waliozuiwa kuendeleza maeneo yao kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege?

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah wewe mwenyewe upo kwa niaba yao tayari hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Kamoli, Mbunge wa Segerea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kufanya uthamini mpya kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wote wa Kipunguni waliopisha ununuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(JNIA).* Zoezi la uthamini linatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2022. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli, swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante nilikuwa naomba pamoja na majibu mazuri na mambo yanayoendelea katika hii Wizara kwa hawa wananchi, nilitaka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri; ni lini hawa wananchi watapata barua ya kuwaambia kwamba sasa wanakwenda kufanyiwa tathmini upya, ni lini maana yake mlikuwa mkiongea kila siku?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nilikuwa nataka nijue ni lini hiyo tathmini itaanza kufanyika, wapate barua rasmi lakini pia wapate tarehe na mwezi ambao wataanza kufanyiwa tathmini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tarehe na mwezi unaweza ukamwambia Mbunge baadaye kama huna hayo majibu, lakini kama unayo, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bonnah Kamoli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua ni lini barua tutapeleka kwa wananchi ili wajue, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshakwisha andika barua kwenda Jiji na Jiji wao watachukua wajibu wa kwenda kuwajulisha na kuwahabarisha wananchi kwamba zoezi hili la tathmini linaanza rasmi, na ninaamini na kwa kuwa Jiji tumeshawaandikia tangu mwezi Aprili naamini watakuwa wamelifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, zoezi lenyewe swali lako la pili linaanza lini? Linaanza mwezi Julai na litakamilika mwezi Septemba, 2022. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, swali la nyongeza.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba je, fedha zilizotengwa za ujenzi wa upanuzi wa uwanja wa ndege Pemba zimejumuisha pia malipo ya fidia kwa wananchi ambao wameingia kwenye eneo hilo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Bakar Hamad kuhusu uwanja wa Pemba; katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha utakaoanza mwezi wa Julai na tunashukuru Bunge lilipitisha tumetenga fedha kwa ajili ya upanuzi wa uwanja kwa Pemba lakini pamoja na fidia eneo lile ambalo tutatwaa kwa ajili ya ujenzi huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa swali la nyongeza.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, ni kwa muda mrefu sana wananchi wa Mkoa wa Singida wameelekezwa kupisha maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege Mkoa wa Singida. Nataka kujua ni lini Serikali itaanza uboreshaji na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Mkoa wa Singida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Kishoa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nimemsikia mara kadhaa Mheshimiwa Mbunge akizungumzia suala la Uwanja wa Ndege wa Singida na sisi kama Serikali kupitia Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi tunasema tuainishe eneo la ujenzi wa Uwanja wa Ndege na kufanya tathmini kwa maana ya kujua gharama halisi. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023

tumetenga bajeti kwa ajili ya kufanya hizo tathmini kwa ajili ya eneo la ujenzi wa uwanja wa ndege hapa Singida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaelekea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete sasa aulize swali lake.

Na. 347

**Ujenzi Mradi wa Maji Iwawa - Makete**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa maji Kata ya Iwawa Makete Mjini?

**SPIKA:** Swali namba ngapi?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, swali namba 347.

**SPIKA:** Simama useme.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba swali namba 347 lipate majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa

kuhudumia Kata ya Iwawa kwa kutumia chanzo cha Mto Isapulano. Mradi huu unahusisha ujenzi wa chanzo, ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilometa 12.5, ulazaji wa mabomba na usambazaji umbali wa kilometa 39 na ujenzi wa matanki matatu yenye ujazo wa lita 450,000. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwanza niipongeze Serikali kwa sababu mradi huu unatumia takribani shilingi 3,000,000,000 kwenye utekelezaji wake lakini tayari wameshatoa shilingi 500,000,000. Ni lini Serikali itatoa shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kukamilisha mradi huu kwa ajili ya wananchi wa Kata ya Iwawa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna mradi wa Matamba - Kinyika ambao Serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 2.8 kuujenga, lakini hadi leo hamjaukamilisha takribani miaka saba.

Ni lini Serikali itakabidhi mradi huu kwa wananchi wa Kijiji cha Nungu, Ng'onde, Mbela na Hitani ili waweze kupata huduma ya maji kwa sababu imebaki tu eneo la *distribution* kwa maana ya usambasaji? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Festo Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi ambao tayari tumeshautolea shilingi milioni 500 na utekelezaji wake unakwenda vizuri ni ule mradi ambao umetumia fedha za

mapambano dhidi ya UVIKO-19 na fedha iliyobaki tutaendelea kutoa kuanzia mwezi huu wa Juni, tutaendelea kuongeza fedha. Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuonane tuliweke sawa hili kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Mradi wa Matamba - Kinyika ni kweli mradi umechukua muda mrefu, lakini ni katika ile miradi ambayo ilikuwa ni chechefu na tayari tunaendelea kuikwamua, hivyo mradi huu pia kwa sasa hivi umeshafikiwa hatua nzuri ni zaidi ya asilimia 80 umeshaweza kutekelezwa, tutakuja kuumalizia hivi punde na watu wa *IRUWASA* watakabidhi kwa watu wa *NKOMBEWASA* ili waweze kufanyakazi ndani ya mkoa wao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Lazalo Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mradi wa Maji wa Uhambi Ngeto ambao umetengewa fedha kwa mwaka huu umekuwa ukitafutiwa mkandarasi tangu mwaka umeanza na mpaka sasa mkandarasi hajaanza kazi.

Je, ni lini mkandarasi huyu atapata mkataba ili aweze kufanyakazi kukamilisha mradi ule?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi huu bado haujapatiwa mkandarasi lakini taratibu zipo mwishoni kabisa. Mheshimiwa Mbunge naomba tuwasiliane baada ya hapa tuliweke sawa suala hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa mradi mkubwa wa maji wa Kibamba, Kisarawe na Pugu ambao tayari umeaanza kusambazwa kwenye kata mbalimbali za Jimbo la Ukonga.

Swali langu je, Serikali sasa ina mpango gani wa usambazaji wa Kata ya Kitunda, Mzinga, Kivule na Kipunguni ambazo hazina usambazaji wa maji haya safi na salama ya *DAWASA?* Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyokiri Serikali tumeendelea kufanya kazi nzuri kwa Mkoa wa Dar es Salaam na katika maeneo haya aliyoyataja tayari tunafedha zaidi ya shilingi bilioni 25 kwa ajili ya mradi huu na sasa hivi tayari mkandarasi ameshapatikana tunaratajia kufika mwishoni mwa mwaka 2022 haya maeneo yote usambazaji wa maji utakuwa umewafikia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunayo miradi ya *World Bank* ambayo ilianzishwa katika Jimbo langu la Nanyumbu, miradi ile ni chechefu; je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba miradi ili chechefu inafanyakazi katika Kata ya Mnanje, Kijiji cha Holola, Kata ya Nandete, Chiwilikiti na Ulanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuna *speed* kubwa sana ya kuhakikisha miradi yote iliyokaa muda mrefu inakamilika. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ameendelea kutupatia fedha na tunaona namna kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais kwa kuijali Wizara ya Maji na kuona kwamba akina mama wanatua ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mbunge kwenye maeneo haya uliyoyataja tunakuja kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 348

**Utekelezaji wa Mradi wa Maji Toka Mto Rufiji Wilaya ya Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, je, ni lini mradi mkubwa wa maji toka Mto Rufiji utaanza kutekelezwa ili kuwaondolea wananchi wa Kata 23 za Wilaya ya Kilwa tatizo la ukosefu wa maji safi na salama ambalo limekuwa likiwakabili kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji huduma ya maji katika Wilaya ya Kilwa ni wastani wa asilimia 64. Katika mwaka

wa fedha 2021/2022 Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi tisa ambayo inatarajiwa kukamilika mwezi wa Julai, 2022 na kuboresha huduma ya maji kufikia asilimia 86.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itaajiri Mtaalam Mshauri na kufanya usanifu wa mradi wa kimkakati na kwa kutumia chanzo cha maji cha Mto Rufiji ikiwa ni mpango wa muda mrefu wa kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Kilwa na maeneo mengine ya Mkoa wa Lindi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nitoe shukrani kwa Serikali ambapo jana tuliweza kusaini Mkataba wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Kilwa Masoko wenye thamani ya shilingi bilioni 81. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niulize swali la nyongeza sasa, kumekuwa na hali chechefu katika utekelezaji wa miradi ambayo inahudumiwa na Mfuko wa Maji ikiwemo mradi ambao unatekelezwa katika Kijiji cha Kinjumbi kutokana na mlolongo mrefu wa malipo.

Je Serikali ina utaratibu gani ambao umeupanga ili kupunguza mlolongo mrefu wa malipo ili miradi hii inayotekelezwa kwa mfuko wa maji iweze kuhudumiwa kwa ufanisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndulane, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kupokea shukrani kwa uzinduzi wa miradi ya maji ya miji 28, kwenye hili tumpongeze sana Mheshimiwa Rais na tumshukuru na

tumuombee kwa sababu kazi aliyoifanya ni kazi iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na malipo ya Mfuko wa Maji kuwa na mlolongo mrefu, Mheshimiwa Mbunge unaelewa hapo nyuma kulikuwa na matumizi mabovu ya fedha katika hali ya udhibiti ilipaswa Wizara kuweka taratibu zote hizo, lakini tunaendelea kuziboresha kuhakikisha kwamba udhibiti utaendelea lakini pia fedha itatoka ndani ya wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nakuomba kwa ruhusa ya kiti chako nitangulize shukrani kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa tamko lake la jana kwamba sasa mradi wa Mwanga, Same, Korogwe unakwenda kuanza tumepata usingizi watu wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo naomba nimuulize sasa Naibu Waziri; je, ni lini mradi mkubwa wa chanzo cha maji cha Ziwa Chala ambao utawapatia maji wananchi wa Holili, Ngoyoni, Chala na wengine tambarare ya Rombo utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mradi wa Ziwa Chala unatarajiwa sana kuona kwamba unakwenda kutatua tatizo la maji, lakini Ziwa Chala tukitaka kutumia mradi ule maana yake ni mradi wa ku-*pump,* ni mradi ambao utaleta gharama kubwa na matokeo yake wananchi watalipa huduma kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini tayari kuna miradi mitatu pale ya *gravity* inayoendelea kujengwa katika Mji wa Rombo na tunatarajia miradi hii ikija kukamilika kwa sababu ni miradi ya miserereko itakuwa ni miradi rafiki kwa wananchi na tatizo la maji linakwenda kukoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami niungane na wenzangu kuipongeza Serikali kwa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa Makonde ambao mkataba umesainiwa jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kujua sasa kuna mradi mkubwa wa kutoa maji mto Ruvuma, Kijiji cha Mahechini kupeleka Manispaa ya Mtwara mradi ambao utanufaisha Jimbo la Nanyamba Mtwara Vijijini na Manispaa ya Mtwara; je, mradi huu utaanza kutekelezwa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Chikota kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakika nimeelewa anayeshukuru anaomba tena, tayari ni jana tu Mheshimiwa Rais ameweza kufanya jambo zito sana la kuona Mradi wa Makonde unaenda kufanyiwa kazi, lakini mradi huu wa Mto Ruvuma nao ni moja ya mikakati ya Wizara tunakwenda kuhakikisha maji ya Mto Ruvuma yanakwenda kutatua matatizo ya maeneo yote ambayo utayapitia. Mara tutakapopata fedha tutaingia kwenye mradi huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 349

**Mradi wa Maji Ikozi- Sumbawanga Vijijini**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Maji wa Ikozi uliopo Sumbawanga Vijijini utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bwawa la Ikozi unaohudumia Viijiji vya Ikozi, Kazwila, Chituo na Tentula vya Kata ya Ikozi, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini. Mradi huo unahusisha ujenzi wa bwawa, ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilometa 1.2, nyumba ya mtambo, ununuzi na ufungaji wa *pump* za kusukuma maji na ujenzi wa mfumo wa kusafisha na kutibu maji. Utekelezaji wa mradi utakamilika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawilli ya nyongeza.

Swali la kwanza; Serikali ina mpango gani sasa wa kuwalipa fidia wananchi ambao walikuwa wanaishi katika eneo lile na walikuwa wanalima mashamba yao?

Swali la pili, shida iliyoko Ikozi ni sawa na shida iliyoko Mpui kata ambazo zinakaribiana, Serikali sasa ina mpango

gani wa kukamilisha mradi ulioko Mpui pale ambao mradi upo lakini wananchi hawapati maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia, tayari Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa maeneo ambayo miradi inapita tumeshaanza malipo na mradi wa eneo hili pia watafikiwa hivi punde. Kata zinazokaribiana hiyo Kata ya Mkuyu na yenyewe pia kuna mradi, mradi huu sasa hivi tunaendelea kuufuatilia kwa karibu sana kuhakikisha dhima ya Serikali kumtua mama ndoo kichwani inakwenda kutekelezeka hata kwa wananchi watokao Mkuyu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali kwamba tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo ameifanya jana kwa miji 28 kupata mradi wa maji na kwa kweli kwa nchi nzima kuna mabadiliko makubwa sana ya maji hata Tarime kuna mabadiliko makubwa sana.

Sasa nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba nilikuuliza swali hapo ukasema Tarime itapata maji katika miji ile 28, lakini kwenye hii *list* ya jana Tarime haimo; nini kauli ya Serikali juu ya watu wa Tarime ili waweze kusubiri maji? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waitara kama ifuatavyo:-

Tarime imo Rorya, Tarime ipo kwenye mradi wa miji 28; vuta subira wakati wa utekelezaji utakapoanza utashuhudia kwamba Tarime imo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge na mimi jana nilikuwepo Ikulu nikiwawakilisha Tarime imo msiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 350

**Kuanzishwa kwa Vyama vya Maendeleo ya Ushirika vya Zao la Mchikichi**

**MHE. SLYVIA F. SIGULA** aliuliza:-

Je, ni lini Vyama vya Maendeleo ya Ushirika vya zao la mchikichi vitaanza kufanya kazi katika Mkoa wa Kigoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Slyvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma una Vyama vya Msingi vya Ushirika wa Kilimo na Masoko 14 *(AMCOS)* vya zao la michikichi katika Halmashauri za Wilaya za Kigoma vipo tisa, Kigoma Manispaa viwili, Uvinza viwili na Buhingwe kimoja ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuendeleza zao la michikichi.

Mheshimiwa Spika, vyama hivyo vimeshaanza kufanya kazi na kwa sasa vipo katika hatua ya kupata mkopo wa shilingi bilioni 2.9 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* utakaowezesha kuboresha mashamba ya wakulima, miundombinu ya uhifadhi mikungu ya michikichi, mashine za uchakataji na ukamuaji wa mafuta ya mawese.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SLYVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Wizara na tunashukuru kwa kupata hizo shilingi bilioni mbili tunaishukuru sana Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa mafuta ulioko nchini na hamasa iliyofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi wa Kigoma wamehamasika sana katika kuingia kwenye zao la michikichi lakini kumekuwa na uhaba wa upatikanaji wa miche ya michikichi inafikia hatua mche mmoja unauzwa hadi shilingi 5,000.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kutoa ruzuku ya miche ya michikichi katika vyama hivi vya ushirika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Slyvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kwamba tutoe miche bora ya michikichi kwa wakulima wa Mkoa wa Kigoma ili kuongeza uzalishaji na ninavyozungumza ni kwamba zoezi hili linaendelea katika Kambi ya JKT Bulombola, lakini vilevile pamoja na Gereza la Kitwanga ambapo jumla ya mbegu zilizozalishwa mpaka hivi sasa ni milioni tisa na miche iliyopo kwenye viriba ambayo bado kugaiwa milioni moja, lakini kwa wananchi tumeshagawa miche 970,000 ikiwa ni elekezo la Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge haya ni maelekezo ya wananchi hawa watapatiwa miche hii bure, isipokuwa tu kwa sharti la kwamba lazima wawe katika mashamba makubwa ili tuweze kui-*trace* miche hii na kuona inaleta tija katika nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa zao la michikichi limekuwa likifanya vizuri katika mikoa ya Kigoma, Rukwa pamoja na Katavi lakini pia hata kule Kyela inafanya vizuri sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba miche bora inagawiwa katika mikoa yote hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephat Kandege, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mikoa aliyoitaja na yenyewe ikolojia inakubali kuzalisha michikichi na mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji wa miche ili kuweza kufikia maeneo haya yote na nichukue fursa hii pia kutoa rai kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa katika mikoa ambao umeitaja kutenga maeneo makubwa ya mashamba makubwa tumeanza kuwaleta wawekezaji wakubwa kwenye mchikichi.

Kwa hiyo, nitoe rai kwa wakuu wa mikoa kuhakikisha kwamba wanakuwa na maeneo ya kutosha ili wakija wawekezaji hao wawe na maeneo ya kuwapeleka na naamini kabisa kwa mkakati tulionao tutakwenda kutatua changamoto hii ya upungufu wa mafuta ya kula hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona; kwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo wa wakati huo Mheshimiwa Bashe alifanya kikao Mkoa wa Kilimanjaro na akatoa maelekezo kwamba Vyama vya Ushirika vya Wilaya ya Hai badala ya kubaki na zao la kahawa peke yake viingie na mazao mengine ya mbogamboga na mazao ya biashara kama vile mgomba, vanilla na mazao mengine.

Je, ni lini Serikali itapeleka waraka maalum wa kuonyesha mfumo wa uendeshaji vyama hivi vya ushirika ili kuweza kuchukua mazao hayo yote kwa Warajis Wasaidizi na Kata zile za Boma Ng'ombe, Bondeni, Mnadani, Weruweru ziweze kunufaika na vyama hivi vya ushirika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saashisa Mafuwe, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Hussein Mohamed Bashe alitoa kauli hiyo ndani na inatekelezwa na mimi niirudie tena kwa msisitizo na kuwataka Warajis Wasaidizi wote kuhakikisha jambo hili linatekelezeka la kwamba Vyama vya Ushirika vinaruhusiwa kusimamia zao zaidi ya moja katika maeneo yao ili kuondoa *multiplicity* ya vyama vingi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuhusu waraka Tume inafanyia kazi jambo hilo ili kutoa maelekezo mahsusi ambayo itawafanya Warajis Wasaidizi wote waweze kuyasimamia maelekezo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Nishati Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 351

**Kukamilisha Umeme Vijiji 138 Vya Mkoa wa Simiyu**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha kuweka umeme katika vijiji 138 vilivyobaki vya Mkoa wa Simiyu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Yusuf Makamba, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Simiyu una jumla ya vijiji 471; kati ya vijiji hivyo, vijiji 269 tayari vina umeme na vijiji 202 bado havijafikiwa na huduma ya umeme. Vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na umeme katika Mkoa wa Simiyu vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili unaotekelezwa na wakandarasi wawili yaani *M/S Sengerema Engineering Group Ltd* na M/*S Steg International Services.* Aidha, hadi sasa jumla ya vijiji 40 kati ya 202 tayari vimeshawashiwa umeme. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; kwanza kabisa nampongeza Waziri kwa majibu mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutenga zaidi ya shilingi bilioni 66 kwa ajili ya kujenga kituo cha kupoza

umeme katika Mkoa wa Simiyu na shilingi bilioni 55 tayari zinatoka mwaka huu. Je, ni lini ujenzi huo utaanza?

Swali la pili, chanzo cha maji kinachohudumia Hospitali ya Mkoa wa Simiyu kinatumia umeme wa jua siku jua halipo maji hamna hospitalini. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *TANESCO* pale kwenye kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha ni kweli zimetengwa shilingi bilioni 65 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Bariadi, lakini pia na *line* ya kutoka Ibadakuli, Shinyanga mpaka Bariadi na ujenzi huu utaanza mara moja baada ya mwaka wa fedha kuanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kituo cha kupeleka maji katika Hospitali ya Mkoa wa Simiyu ambacho kinaendeshwa na *solar,* katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi milioni 150 ili kupeleka umeme katika kile chanzo cha maji ili kiendeshwe na umeme badala ya *solar,* hivyo kutoa maji ya uhakika katika Hospitali ya Mkoa wa Simiyu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 352

**Hitaji la Umeme Vijiji vya Qameyu, Madunga na Kiru – Babati Vijijini**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa katika Kata za Qameyu, Madunga na Kiru Babati Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, Mbunge wa Babati Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Qameyu ina jumla ya vijiji vinne ambavyo ni Endaw, Qameyu, Gawal na Merri. Kati ya vijiji hivyo, vijiji vitatu vya Endaw, Qameyu na Gawal tayari vimepatiwa umeme. Kijiji kimoja cha Merri ndio hakijapata umeme na kipo kwenye mradi wa *REA III* Mzunguko wa Pili ambapo mkandarasi anaendelea na kazi ya kuchimba mashimo na kusimika nguzo katika kijiji hicho. Kazi za mradi katika Kijiji hicho cha Merri zinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2022.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Madunga ina vijiji vitatu ambavyo ni Madunga, Utwari na Gidng'war. Vijiji vyote vitatu tayari vimeshafikiwa na huduma ya umeme. Kata ya Kiru ina jumla ya vijiji sita ambapo kijiji kimoja cha Kiru Six tayari kimeshapata huduma ya umeme. Vijiji vyote vitano visivyokuwa na umeme vya Kiru Dick, Kimara, Kokomay, Kiru Ndogo na Erri vinapatiwa umeme katika mradi wa *REA III* Mzunguko wa Pili unaoendelea. Mkandarasi anaendelea na kazi za kuchimba mashimo na kusimika nguzo katika vijiji hivyo. Kazi za mradi zinatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Sillo, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Waziri na maswali yangu ya nyongeza yalijibiwa wakati wa maonesho ya *REA* katika viwanja vya Bunge kwa hiyo naiomba Serikali ijielekeze katika kutekeleza miradi hii ili ikamilishwe kwa wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hizo zilikuwa ni shukrani kwa hiyo siyo swali haya tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Hoja ya Kutengua Kanuni nimuite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa George Simbachawene.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa timu ya wasichana chini ya miaka 17 maarufu kama kwa jina la *Serengeti Girls* imefuzu kushiriki Kombe la Dunia mwaka huu wa 2022 nchini India na hii ni kufuatia ushindi walioupata katika michezo yake ya awali dhidi ya nchi za Botswana, Burundi na Cameroon;

Na kwa kuwa ushindi huo wa timu ya *Serengeti Girls* ni jambo la kupongezwa na wananchi wote tukiwemo sisi Wabunge kwani linaipa sifa kubwa nchi yetu pamoja na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambaye anaendelea kuboresha sekta ya michezo;

Na kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina utaratibu wa kupongeza timu zetu zinapofanya vizuri jambo ambalo huongeza morali kwa wachezaji katika kufanya vizuri zaidi;

Na kwa kuwa timu ya *Serengeti Girls* ipo hapa Bungeni mahsusi kwa ajili ya kupongezwa;

Mheshimiwa Spika, itapendeza endapo pongezi hizi watazipata vizuri wakiingia ndani ya Ukumbi wa Bunge;

Na kwa kuwa Kanuni ya 160(1) inaelekeza kwamba wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni watakaa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao pasipo kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge;

Hivyo basi kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kuweza kutoa pongezi zake kwa timu ya *Serengeti Girls* kwa utaratibu wa Kibunge, Kanuni ya 160(1) itatenguliwa ili kuwezesha timu ya *Serengeti Girls* pamoja na viongozi wake waingie ndani ya ukumbi wa Bunge na kupongezwa rasmi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita *Sergeant-At-Arms* kuwaleta hapa ndani tunao wageni wengine na wakati huo huo leo nitatoa nafasi maalum ya watu kusimama humu ndani mimi nikiwa pia nimesimama na wengine naona wanatembea kabla sijatoa hiyo ruhusa huko nyuma na wengine wanaongea.

Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri mlio upande wangu wa kulia mtasogea kidogo na Waheshimiwa Wabunge mkae kwenye viti vinavyofuata hapo ili kutengeneza nafasi kwa ajili ya vijana wetu wapate kukalia viti vya Wabunge siku ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ahsanteni sana.

Sasa niwatangaze wageni wengine waliopo hapa Bungeni, tunaye Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Charles Kichere pamoja na watendaji wengine wa ofisi hiyo, karibuni sana, sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waziri wa Fedha na Mipango ambao ni viongozi na watendaji wa Wizara hiyo wakiongozwa na Ndugu Jenifa Christian Omolo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Huduma za Hazina, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 90 na walimu kumi kutoka Shule ya Sekondari Itega ya jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza wote ninawaona na nilishasema nikisimama nisikilizeni, pengine ninalo tangazo linalokuhusu wewe. Mheshimiwa unayeongea hapo na Mheshimiwa Mchengerwa geukia mbele, tusikilizane kidogo. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 43 wa Chuo cha Biblia kutoka Sanjaranda Itigi ambao wanatoka Mkoa wa Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwatangaza hawa wageni wengine sasa niwatangaze wageni 37 ambao ni wachezaji 37 wa *Serengeti Girls* ambao wamefuzu kwenda kucheza Fainali za Kombe la Dunia la Wanawake chini ya umri wa miaka 17 nchini India wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Hassan Abbas, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndugu Saidi Yakubu, pamoja na Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania *(TFF)*

Ndugu Wallace Karia, pamoja na Ndugu Aden Mohamed Mwenyekiti wa Mpira wa Miguu Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Sasa *Sergeant-At-Arms* awalete Bungeni mabinti zetu hawa ambao wametupa heshima kubwa sana, karibuni sana. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Timu ya Serengeti Girls Uliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana wanaendelea kupewa nafasi kule ya kukaa. Sasa wale wanaomchelewesha Mheshimiwa Waziri Mkuu pale wamwache apite Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa niwaruhusu mkae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitampa nafasi Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ili awatambulishe kikosi hiki ambacho kinaenda kuliwakilisha Taifa letu huko duniani. Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kukutana hapa leo ili tuweze kufanikisha shughuli hii muhimu ya Kitaifa. Kwa namna ya kipekee nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuruhusu kufanyika kwa mabadiliko mbalimbali yenye tija kwa lengo la kuimarisha sekta ya michezo nchini ambayo ni sekta muhimu inayogusa maisha ya Watanzania wengi kwa kuwafanya watu kuwa karibu, kuburudika na kujenga afya ya mwili na akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa idhini yako kuwatambulisha mashujaa wetu timu ya *Serengeti Girls* ambayo imealikwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ridhaa yako kutembelea hapa Bungeni ili kupata fursa ya kupongezwa pamoja na kusalimiana na

Waheshimiwa Wabunge na viongozi mbalimbali wa Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Timu ya Taifa ya Wasichana wa chini ya umri wa miaka 17 maarufu kwa jina la *Serengeti Girls* ambao wamefanikiwa kufuzu kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika nchini India mwezi Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, katika safari yako ya kufika kufuzu kushiriki michuano hiyo ya Kombe la Dunia, *Serengeti Girls* iliichabanga timu ya Taifa ya Botswana kwa jumla ya magoli kumi na moja kwa sifuri, yaani magoli saba nyumbani na magoli manne kule Botswana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikaibamiza timu ya Burundi kwa jumla ya magoli sita kwa moja, na kuipiga timu ya Cameroon kwa magoli matano kwa moja. Ikiwa ni magoli manne kule Cameroon na goli moja hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu yaani *TFF* imehakikisha kuwa timu hiyo inapatiwa malezi na mafunzo yanayostahili ili kuweza kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na hivyo kufuzu kushiriki mashindano hayo ya Kombe la Dunia nchini India, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mashindano hayo Tanzania itaungana na nchi mbili za Bara la Afrika yaani Morocco na Nigeria, huu ni mwendelezo wa mafanikio lukuki yanayopatikana katika kipindi cha mwaka mmoja cha Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa juhudi zake binafsi, juhudi za Serikali na viongozi mbalimbali wa Serikali kwa ujumla, juhudi za kushirikiana na wadau tumeweza kupata mafanikio ambayo timu yetu ya Taifa pia ya Ulemavu *Tembo Worries* wamefanikiwa kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya dunia yatakayofanyika kule nchini Uturuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuzu huko kumekuja baada ya timu hiyo kuichabanga timu ya Morocco magoli mawili kwa moja, timu ya Senegal kwa goli moja kwa bila na kuibamiza tena timu ya Cameroon kwa mabao matano kwa bila. Kwa sasa timu hii ipo kambini kwa maandalizi ya mashindano ya Kombe la Dunia tangu mwezi Februari kwa gharama za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ndiyo inayogharamia kambi na matumizi yote ikiwa ni pamoja na malazi, chakula, ufundi, usafiri wa ndani na nje pamoja na posho za wachezaji na benchi la ufundi kwa ujumla. Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu yaani *TFF* itahakikisha kuwa timu hizo zinapatiwa malezi na mafunzo yanayostahili ili kuweza kufanya vizuri katika mashindano hayo ya Kombe la Dunia yatakayofanyika nchini Uturuki kwa timu ya wanaume wenye ulemavu wa mpira wa miguu na kule nchini India kwa timu yetu ya *Serengeti Girls*. Nazipongeza timu zetu zote kwa hatua kubwa na ya kihistoria kwa nchi yetu zilizofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawaomba Watanzania wote kujitoa kwa wingi kwa hali na mali ili kuzishabikia na kuzitia moyo timu zetu, Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo itaandaa utaratibu maalum na mahsusi kwa ajili ya kuratibu ushiriki mpana wa Watanzania katika kwenda kujionea mashindano hayo ya Kombe la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa nasi katika safari yote hii na kutuwezesha leo kuwa hapa kwa ufahari kabisa, alitupa moyo, alituwezesha na zaidi kabisa alikuwa karibu nasi kufuatilia maendeleo ya timu, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani sasa tumepata picha ya safari ilivyokuwa ndefu ya hawa *Serengeti Girls* kufikia sehemu hii ambayo wamefika. Kwa hiyo, kwa maelezo hayo ya Mheshimiwa Waziri ambayo na sisi sote tunakubaliana nayo tunawapongeza sana, sana, sana mabinti zetu na tunawatakia kila la heri katika safari iliyo mbele yenu. *(Makofi)*

Sasa mmeingizwa humu ndani leo tunaamini hii ndio ahadi yenu kwamba kombe mtalileta hapa ili mrudi tena humu ndani kuja kukaa hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo tunawapongeza sana sana na tunawaheshimu na tunathamini nguvu mnayotumia, juhudi mnayoitumia kuhakikisha mnaliletea Taifa letu heshima kama hii mliyoileta ya kufuzu na tunaamini kwakuwa mmefuzu basi mtaenda kuonesha viwango vya juu zaidi kule mnapokwenda kushindana na wenzenu wanaotoka maeneo mbalimbali ya sisi kama Bunge tunawatakia kila lililo la heri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa leo wamekaa kwenye hivi viti maalum kabisa, walipokaa hapo wanaponyanyuka kila mtu ajue kazi yake kwenda kuleta kombe maana pengine sasa nchi yetu itapata bahati ya kuleta Kombe la Dunia angalau hawa wakatuwakilishe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri na viongozi wao wote mliopo humu ndani tunawashukuru kwa juhudi mbalimbali mnazozifanya ili kuhakikisha timu yetu inafanya vizuri mkiongozwa na Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote kwa kweli na *captain* hapa ni yupi?

*(Hapa Captain wa Serengeti Girls Ndg. Noela Patrick Lwala Alisimama)*

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujawatoa nje nadhani tumsikie *captain* kidogo aseme neno halafu tutaendelea na yaliyo mbele yetu. *(Makofi)*

*Captain* jitambulishe jina na pia useme neno. Shuka hapa leo umepewa heshima kubwa sana njoo usemee hapa mbele. *(Makofi)*

**NDG. NOELA PATRICK LWALA – CAPTAIN WA SERENGETI GIRLS:** Mheshimiwa Spika, kwa majina naitwa Noela Patrick Lwala ni *Captain* wa *Serengeti Girls. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kusema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**WABUNGE FULANI:** Kazi lendelee. *(Makofi)*

**NDG. NOELA PATRICK LWALA – CAPTAIN WA SERENGETI GIRLS:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama hapa Dodoma, nikiri kwamba hii ni mara yangu ya kwanza kabisa kukanyaga ndani ya sehemu hii ya Bunge, ni heshima kubwa sana kwangu na wenzangu ambao tumeandamana nao. *(Makofi)*

Ushindi huu tulioupata ni wa Watanzania wote na nina uhakika kwamba ni kitu ambacho kila Mtanzania amekisubiria kwa muda mrefu sana. Kwa hakika sasa tumefungua njia ya timu zetu mbalimbali kufuzu na kushiriki katika mashindano ya juu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo yote ya kiufundi na hapa nilishukuru sana benchi lote la ufundi ambalo mimi nilikuwa kiongozi mkubwa tulishikamana kwa pamoja na wote tulikuwa na heshima kubwa ya kuhakikisha kwamba kwanza tunaijenga familia moja na wachezaji na kuweka malengo kwa pamoja kama familia ili tuweze kushinda. Kwa hakika tunamshukuru Mungu malengo yetu yametimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushindi huu pia unatokana na chachu kubwa ya Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambayo kwa hakika tunaona mama anavyojali sekta

ya michezo na kuhakikisha kuwa Wizara yake inakuwa bega kwa bega na timu zetu za Taifa kipindi chote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yetu ya Michezo na BMT wameshirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu mara kwa mara, usiku na mchana bila kuchoka, tumeona vikao baina ya Wizara na *TFF* mara kwa mara wakiwa kitu kimoja na kutupa yote yanayotakiwa kwa kambi yetu, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni Rais wetu wa kwanza mwanamke kutokea katika nchi yetu ya Tanzania kwa hakika anaupiga mwingi sana. *(Makofi)*

Tulipokutana naye tulimuahidi kuwa na sisi ni Timu ya Wasichana ya *Serengeti Girls* itakuwa timu ya kwanza kufuzu kwenda kushiriki Kombe la Dunia la Mchezo wa Mpira wa Miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa tunamshukuru Mungu ahadi yetu kwa mama yetu tumeitimiza, tunamuahidi tena kwa kuwa anaupiga mwingi kwa Watanzania na sisi tunakwenda kuupiga tena mwingi India kwa niaba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi yetu sasa nikujiandaa kwa ajili ya mashindano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika nchini India mwezi Oktoba, 2022. Tuna uhakika na tayari tumepata maelekezo ya kuwasilisha programu yetu kwa Wizara ili maandalizi yaanze mapema ni matumaini yetu kuwa kasi hii ya Wizara tunakwenda kufanya maajabu kule India kama ambavyo tumeyafanya kwa nchi ya Cameroon hawaamini kama Tanzania imewatoa kwa magoli matano kwa moja. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu mbariki Rais wetu mpendwa ambaye tunaona kabisa anatupeleka mbali kwenye sekta ya michezo kwa muda

wake mchache tayari timu mbili zinakwenda Kombe la Dunia. Mama anaupiga mwingi na anaondoka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi/ Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana binti yetu na *captain* wa timu hii iliyofanya vizuri.

Sasa viongozi wa timu hii na timu nzima kama nilivyosema kwamba tunawatakia kila la heri, sasa mtatupisha mtaenda kutusikia mkiwa pale juu, lakini kabla hamjaondoka Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo kwenye taarifa yako wakati ukisoma taarifa ya namna *Serengeti Girls* walivyofanya vizuri umesoma pia taarifa ya namna *Tembo Warriors* walivyofanya vizuri na kwamba na wao wanaenda kutuwakilisha kwenye Kombe la Dunia, lakini hapa ndani *Tembo Warriors* hawajaingia.

Sasa kwa kuwa *Tembo Warriors* na wao wanaenda kuliwakilisha Taifa kwenye Kombe la Dunia la Watu Wenye Ulemavu; na kwa kuwa *Serengeti Girls* wanaenda kutuwakilisha kwa timu za wasichana za chini ya miaka 17 na wameingia hapa ndani; na kwa kuwa huko mbele tunatamani timu nyingi zaidi zipate fursa ya kwenda kutuwakilisha kwenye Kombe la Dunia naagiza kesho *Tembo Warriors* waletwe humu ndani tuwape pongezi zao pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitatoa fursa ya mabinti zetu na viongozi wetu kuondoka na kuelekea kwenye Jukwaa la Spika ili tuendelee na ratiba iliyo mbele yetu. Ahsanteni sana na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Serengeti Girls Uliondoka Ukumbini)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na ratiba yetu nimeletewa taarifa hapa kwa sababu nimeagiza kwamba waletwe kesho sasa naambiwa leo

wanaondoka kuelekea Poland, ila jambo hili halileti picha nzuri sana.

Kwa hivyo, watakaporejea Mheshimiwa Waziri kama tutakuwa bado tupo hapa Bungeni watakuja hapa na kama si Bunge hili basi Bunge la mwezi wa tisa uhakikishe unawaleta hapa Bungeni ili kuweka usawa kati ya vijana wetu ambao wanajituma sana kwa ajili ya kuliletea heshima Taifa letu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tutaletewa taarifa lini watakuja watakaporejea kutoka huko kwenye hayo mashindano. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**MHE. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba Madelu aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2021/2022 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu nane ya Wizara, pamoja na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine tena kujadili

Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika**,** kipekee napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango. Napenda kumhakikishia kwa mara nyingine kuwa nitaendelea kutumikia dhamana aliyonipa kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa. Ni dhahiri kwamba, katika kipindi cha takribani mwaka mmoja na miezi mitatu ya uongozi wake, nchi yetu imepata mafanikio mengi ambayo kila mmoja wetu anapaswa kujivunia. Mwenyezi Mungu amjalie afya njema, hekima, busara katika kuliongoza Taifa letu kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** nitumie fursa hii pia kwa kukushukuru wewe binafsi pamoja na Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Waheshimiwa Wabunge kuliongoza Bunge letu tukufu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimwa Daniel Baran Sillo - Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu wake Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua - Mbunge wa Kilindi kwa maoni na ushauri wao mzuri katika kuboresha utendaji wa Wizara pamoja na maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/2023. *(Makofi)*

Pamoja na pongezi hizo natoa pole kwa Bunge lako tukufu kwa kuondokewa na Mheshimiwa Irene Ndyamukama, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Rukwa, ambaye ametangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa naomba nijielekeze katika hoja yangu inayohusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022; maeneo ya vipaumbele pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti imezingatia majukumu ya Wizara na vipaumbele vya mwaka 2021/2022 kama ilivyoanishwa kata aya ya 7 na ya 11 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2022 Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 689. 5 sawa na asilimia 74.9 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 920.38. Aidha, katika kipindi hicho Mafungu ya Wizara pamoja na Fungu 45 yaani Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi yametumia jumla ya shilingi trilioni 9.64 sawa na asilimia 72.6 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 9.04 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 597.55 ni matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizotumika kwa kila Fungu umeainishwa katika kitabu cha hotuba kiambatisho namba 1 hadi namba 3.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa ufafanuzi kwa Bunge lako tukufu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia Sera za Uchumi Jumla, kuweka malengo na shabaha kama msingi na kanuni wa kutunga sera na mwelekeo wa kujenga uchumi jumuishi, himilivu na endelevu.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 ulikuwa kwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la ukuaji limetokana na jitihada zilizochukuliwa na Wizara chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii

kurejea katika hali yake ya kawaida baada ya kuathirika na UVIKO–19. Miongoni mwa hatua mahsusi zilizochukuliwa na wizara ni kuwezesha upatikanaji wa mikopo isiyo na masharti kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *IMF* wa shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi UVIKO-19 ambapo Mheshimiwa Rais alikuwa kinara wa mazungumzo hayo.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.3 kwa mwaka 2020. Aidha, katika kipindi kama hicho Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho 2021. Ongezeko la mfumuko wa bei lilitokana naongezeko la gharama za uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma, hususan bidhaa ya petroli, mafuta ya kula, mbolea, chuma na malighafi za viwandani katika soko la dunia. Pamoja na ongezeko hilo, kiwango hicho bado kipo ndani ya matarajio ya wigo wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambacho ni asilimia 3.0 hadi asilimia 5.0 na lengo la nchi za Jumuiya ya Afrika ya *SADC* ambayo ni asilimia 8.0.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2022, wastani wa fedha taslimu uliongezeka kwa asilimia 13.8 ikilinganishwa na asilimia 2.7 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021. Ujazo wa fedha kwa tafasiri pana yaani *M3* ulikuwa kwa wastani wa asilimia 13.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021 na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 8.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.3 kwa mwaka 2021.

Aidha, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za kimarekani bilioni 5.46 kiasi ambacho kinatosheleza uingizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 4.8 ikilinganishwa na lengo la miezi 4.0 isiyopungua miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mipango ya Maendeleo ya Taifa; hadi Aprili, 2022 katika usimamizi wa Mipango ya

Maendeleo ya Taifa Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kukamilisha maandalizi ya nyaraka za mapitio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025;

(ii) Kufanya uchambuzi wa maombi ya fedha kwa miradi ya kimkakati 38 kutoka Halmashauri 28 yenye thamani ya shilingi bilioni 288.06 ambapo Wizara iliridhia maombi ya shilingi bilioni 201.80 yaliyokidhi vigezo;

(iii) Kukamilisha na kusambaza Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu mbalimbali za Maendeleo; na mafanikio mengine kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ujenzi wa madarasa 15,000 na mabweni 50 yaliyojengwa chini ya Mpango wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa pamoja na Mapambano ya athari za Kiuchumi na Kijamii UVIKO-19.

(iv) Mengine ni kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi 173 ya maendeleo katika sekta za kilimo, viwanda, utawala bora, ujenzi, uchukuzi, maji, elimu, afya, biashara na mifugo katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Geita, Kagera, Mara pamoja na Simiyu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato hadi Aprili, 2022 ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa umefikia shilingi trilioni 19.99, sawa na asilimia 93.3 ya makadirio ya kukusanya shilingi trilioni 21.42 katika kipindi kama hicho. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yamefikia shilingi trilioni 17.20, sawa na asilimia 94.5 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 18.2. Mapato ya Sera ya Kodi yamefikia shilingi trilioni 2.03, sawa na asilimia 81.2 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 2.5 na Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yamefikia shilingi bilioni 759.0, ikiwa ni asilimia 104.8 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 724.1 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2022 Wizara imeratibu upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi trilioni 4.12 kutoka

katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya bajeti. Aidha, Wizara imefanikisha upatikanaji wa mkopo wa jumla ya shilingi trilioni 1.81 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo; vilevile shilingi trilioni 3.93 zimepokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 106.1 ya makadirio ya kupokea shilingi trilioni 3.70 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi hadi Aprili, 2022 jumla ya shilingi trilioni 29.40 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango pamoja na Bajeti ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 10.61 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na shilingi trilioni 7.27 kwa ajili ya kuhudumia Deni la Serikali, shilingi trilioni 6.73 kwa ajili ya Mishahara na shilingi trilioni 4.79 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Wizara imefanya uhakiki wa taarifa mbalimbali za malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma 76,404. Aidha, baada ya uhakiki kukamilika jumla ya shilingi bilioni 124.32 zimelipwa kwa watumishi 74,670 ambapo watumishi hao utumishi wao haujakoma na shilingi bilioni 5.98 zimetumika kulipa watumishi 1,734 ambao wamestaafu. Vilevile madeni ya jumla ya shilingi bilioni 772.87 yalihakikiwa na kulipwa. Kati ya kiasi hicho, madai ya wakandarasi ni shilingi bilioni 4.24 na wazabuni shilingi bilioni 81.67, watumishi shilingi bilioni 25.71 na watoa huduma shilingi bilioni 52.74 na madeni mengineyo shilingi bilioni 608.51.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Usimamizi wa Mifumo hadi Aprili, 2022 Wizara imefanikiwa kuhuisha na kufungamanisha Mfumo wa Ulipaji wa Serikalini na mifumo ya Hazina pamoja na hayo mafanikio mengine yaliyopatikana ni kufungamanisha mfumo wa *GBMES* pamoja na *GePG* na kuunganisha watoa huduma za malipo 853, benki 28 na mitandao saba ya simu katika mfumo wa *GePG*. Aidha, Wizara imefanya ukaguzi wa mali za Serikali katika vituo 126 na kufanya uhakiki maalum wa mali na madeni ya Hospitali ya *Dar Group* ili kurejesha hospitali hiyo Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeboresha mifumo ya taarifa za fedha kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa za kifedha za makampuni tanzu na kurahisha usimamizi wake. Aidha, mwongozo wa uanzishwaji na uendeshaji na usimamizi wa kampuni tanzu na taaasisi za mashirika ya umma umekamilika na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, vilevile ufuatiliaji na tathimini umefanyika katika mashirika 98 yaliyobinafsishwa, ikijumuisha hoteli 10, kampuni 31, mashamba 15, viwanda 42 na matokeo ya ufuatiliaji huo yamebaini kiwango kidogo cha uzalishaji wa zao la mkonge katika baadhi ya mashamba na kutoendelezwa na mengine kutelekezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usimamizi wa sekta ya fedha Wizara imefanikiwa kuhuisha Rasimu ya Sera ya Taifa ya Bima; kuzindua Mpango wa Kutoa Elimu ya Fedha kwa Umma wa mwaka 2020/2021 - 2024/2025 pamoja na nyenzo ya kufundishia; kuandaa Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Sekta ya Benki na Mkakati wake; kuandaa Mkakati wa Upatikanaji wa Fedha za Wajasiriamali Wadogo na wa Kati; na kuzindua Mkakati wa Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Njia Mbadala yaani *Alternative Project Financing a Strategy*.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara iliahidi kuendelea na zoezi la kutenga maeneo ya kuhesabia watu wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti, 2022. Hadi Aprili, 2022 vitongoji vyote 64,318 na mitaa 4,670 Tanzania Bara imetengwa ikiwa ni ufanisi wa asilimia 100. Aidha, jumla ya maeneo ya kuhesabia watu 4,313 kutoka katika Sheia zote 388 yametengwa kwa upande Tanzania Zanzibar sawa na asilimia 100 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizokamilika ni kuandaa madodoso ya Sensa ya Watu na Makazi, Sensa ya Majengo na Sensa ya Anuani za Makazi, miongozo ya fomu za kudhibiti ubora, kuandaa mfumo wa ufuatiliaji, kufanya

Sensa ya Majaribio Agosti, 2021 katika Mikoa 18 ya Tanzania Bara na Zanzibar na kuendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya sensa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; hadi Aprili, 2022 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kufanya ukaguzi wa Wizara, Idara zinazojitegemea 66, Wakala 31, Hospitali za Rufaa na Maalum 33, Mfuko Maalum wa Serikali 17, Mamlaka za Maji Daraja C pamoja na mabonde ya maji 29, Taasisi za Serikali 64, Balozi 43, Mikoa 26, Mamlaka 185, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma 195, ukaguzi wa Vyama vya Siasa 19 vyenye usajili wa kudumu ikiwemo Chama cha Mapinduzi.

Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kufanya ukaguzi 12 za ufanisi na nane za kiufundi. Vilevile jumla ya ukaguzi maalum 56 zimefanyika ambapo 37 ni kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, 12 za Serikali Kuu, sita za Mashirika ya Umma na moja kwenye Mfumo wa TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake yanapatikana katika kitabu cha hotuba ukurasa wa sita hadi 33. Naomba hotuba yangu yote kwenye kitabu iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa changamoto; mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii yalikumbwa na changamoto zifuatazo:-

1. Kuvurugika kwa mfumo wa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia kutokana na athari za UVIKO-19 na vita baina ya Urusi na Ukraine ilikuwa moja ya changamoto kubwa ambayo imesababisha ongezeko la mfumuko wa bei katika soko la ndani pamoja na kasi ndogo ya ukuaji wa pato la Taifa.

2. Kusitishwa kwa baadhi ya mikataba ya ununuzi na ugavi na vitendea kazi, hususan magari kutokana na athari za UVIKO-19.

3. Kasi kubwa ya mabadiliko ya teknolojia ya habari na mawasiliano ikilinganishwa na uwezo wa ndani wa kuimarisha na kujenga mifumo ya TEHAMA pamoja na mifumo ya kielektroniki na usimamizi wa fedha.

4. Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ununuzi wa vitendea kazi kutokana na athari za mfumuko wa bei vilivyoathiri mwelekeo wa Bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, namna ya kukabiliana na changamoto hizo; Wizara imeendelea kuchukua hatua za kisera, hususan kutoa ruzuku kwa bidhaa za petroli ili kupunguza kasi ya ongezeko la mfumuko wa bei na gharama za Maisha; kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya baadhi ya mazao kama njia mbadala kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje, hususan ngano na mafuta ya kula ili kudhibiti mfumuko wa bei; na hatua nyingine ni kuongeza uwekezaji katika ujuzi na utafiti wa masuala ya TEHAMA na mifumo ya kielektroniki ili kupunguza athari za utegemezi wa mifumo ya kutoka nje na kutoa kipaumbele kwa majukumu na kazi zenye maslahi mapana kwa Taifa, hususan miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Fedha na Mipango kupitia mafungu yake nane inatarajia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia malengo, shabaha na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati wa kila Fungu na Taasisi zake. Aidha, malengo, shabaha na vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023 vimeibuliwa kutoka kwenye Mpango Mkakati wa Wizara 2021/2022 – 2025/2026, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama ambavyo nimetoka kuielezea.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya matumizi ni kama ifuatavyo; kukusanya, kutafuta na kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali; kuhudumia kwa wakati deni la Serikali pindi linapoiva; kufanya tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ikiwa ni maandalizi mahusus ya Dira Mpya

ya Taifa ya Maendeleo ya 2050; kufanya tathmini ya mfumo na muundo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuwezesha kutungwa kwa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo; kurejesha bahati nasibu ya Taifa; kufanya tafiti katika sekta ya uzalishaji ili kuibua fursa ya uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya Serikali katika muda mfupi, kati na mrefu; kuendelea na utekelezaji wa maagizo ya Serikali ya kutafsiri sheria za Wizara na taasisi zake kwa lugha ya Kiswahili; na kuhuisha Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi.

Mheshimiwa Spika, kati ya vipaumbele kwenye matumizi mojawapo ni kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita; kuandaa na kujenga ghala la takwimu; kuratibu na kusimamia zoezi la Sensa ya Watu na Makazi; kuwezesha taasisi na Wizara hususan taasisi za mafunzo na elimu ya juu; kuboresha miundombinu ya kujifunza na kufundishia; kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli, kule Mtumba Dodoma; ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mhakikimali wa Hazina Ndogo katika Mkoa wa Geita, Njombe na Songwe; na kukarabati jengo la Wizara lililopo Jijini Dar es Salaam, Hazina Ndogo ya Morogoro, Kigoma pamoja na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vipaumbele vya taasisi ikiwemo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni kama ambavyo inaonekana katika aya ya 86 hadi 106 katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makadirio ya mapato; katika mwaka 2022/2023 Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi trilioni 1.05 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, mauzo ya leseni za udalali. Mchanganuo wa maduhuli yaliyokadiriwa inaonekana katika jedwali namba mbili katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, kwa upande watumizi, ili kutekeleza kwa ufanisi vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ninawasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maombi ya kuridhiwa jumla ya shilingi trilioni 14.94 kwa mafungu yote nane ili kugharamia matumuzi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 13.62 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.32 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 85.52 kwa ajili ya Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; kiasi cha shilingi bilioni 74.59 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 10.93 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa kiasi kilichoombwa kwa kila fungu umeainishwa katika jedwali namba tatu katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushauri na ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake wakiongozwa na Bwana Emmanuel Tutuba - Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Shaaban, Bwana Lawrence Mafuru na Bi. Jenifa Omolo kwa ushauri na usimamizi thabiti wa majukumu na kazi za kila siku za Wizara na Taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru Wakuu wa Idara, vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Taasisi zake kwa utekelezaji mzuri wa mikakati ya maendeleo, ushauri pamoja na ushirikiano wao mahiri katika kufanikisha majukumu yangu ya kila siku. Ahsanteni sana na Kazi Iendelee.

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali inaendelea na maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Zoezi hili ni muhimu sana kwa nchi ili kupata

taarifa za msingi zitakazosaidia katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa Taifa letu. Hivyo, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa tuendelea kuelimisha na kuhamasisha wapiga kura wetu na watanzania wote kwa ujumla kushiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi litakalofanyika Agosti 23, 2022.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda nikushukuru wewe tena pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii mbele yenu na umma wa Watanzania kwa ujumla. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara yetu ya Fedha www.mof.go.tz.

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya Wizara ya Fedha. Bajeti ya Serikali, bajeti ya Mama Samia Suluhu Hassan itakuja tarehe 14 Juni, 2022 na hiyo ndiyo ambayo itakuwa imebeba matumaini ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2022/23 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**1. *Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2021/22 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu nane (8) ya Wizara, pamoja na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2022/23.

***2. Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema, na

kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine tena kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2021/22 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2022/23.

***3. Mheshimiwa Spika***, kipekee, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango. Napenda kumhakikishia, kwa mara nyingine kuwa nitaendelea kutumikia dhamana aliyonipa kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa. Ni dhahiri kwamba, katika kipindi cha takribani mwaka mmoja na miezi mitatu (3) ya uongozi wake, nchi yetu imepata mafanikio mengi ambayo kila mmoja wetu anapaswa kujivunia. Mwenyezi Mungu amjalie afya njema, hekima na busara katika kuliongoza Taifa letu.

***4. Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii adhimu kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa A. Zungu (Mb) kwa kuchaguliwa kwa kishindo na waheshimiwa wabunge kuliongoza Bunge letu Tukufu. Ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na hekima ili kutekeleza majukumu yenu ya kibunge kwa ufanisi. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kwake na Mheshiwa Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na pongezi hizo, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na Mheshimiwa Irene A. Ndyamukama, Mbunge Viti Maalumu Mkoa wa Rukwa, ambaye ametangulia mbele ya haki. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

***5. Mheshimiwa Spika,*** kwa muktadha wa tukio la leo, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Daniel Baran Sillo – Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Omari Mohamed Kigua - Mbunge wa Kilindi kwa maoni na ushauri wao mzuri katika kuboresha utendaji wa Wizara pamoja na maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23. Kwa niaba ya Wizara na taasisi zake,

napenda kuihakikishia Kamati kuwa tutaendelea kushirikiana kwa karibu ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi waliotupa dhamana ya kusimamia masuala ya mipango, uchumi na fedha kwa Taifa letu.

***6. Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo, sasa naomba nijielekeze katika hoja yangu yenye maeneo makuu manne (4) ambayo ni: majukumu ya Wizara; mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2021/22; vipaumbele vya Wizara na taasisi zake kwa Mwaka 2022/23; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2022/23.

**2.0 MAJUKUMU YA WIZARA**

***7. Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 534 la tarehe 02 Julai 2021, majukumu ya kisera na kiutendaji ya Wizara ya Fedha na Mipango ni pamoja na:

i) usimamizi wa sera za uchumi jumla, fedha, ununuzi wa umma na ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi:

ii) usimamizi mipango, mikakati na miongozo ya kitaifa ya maendeleo;

iii) usimamizi wa bajeti ya Serikali;

iv) kuratibu upatikanaji wa fedha kutoka taasisi za fedha za kikanda na kimataifa kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;

v) udhibiti utakasishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi;

vi) usimamizi na udhibiti wa mali za umma;

vii) usimamizi uendeshaji wa Mashirika ya Umma pamoja na vitega uchumi vya Serikali;

viii) usimamizi wa masuala ya pamoja ya fedha kati ya Tanzania Bara na Zanzibar;

ix) usimamizi wa mafao na pensheni kwa wastaafu wasio wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

x) usimamizi wa Deni la Serikali;

xi) usimamizi wa michezo ya kubahatisha ;

xii) usimamizi wa maendeleo ya Sekta ya Fedha; na

xiii) usimamizi wa takwimu rasmi za kitaifa.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2021/22

### 3.1 Mapitio ya Mapato na Matumizi

#### 3.1.1 Mapato

***8. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 920.38 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwemo gawio, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, marejesho ya mikopo, kodi za pango, mauzo ya leseni za udalali na nyaraka za zabuni. Hadi Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 689.5, sawa na asilimia 74.9 ya lengo la mwaka. Mchanganuo wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na.1: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli kati ya Julai 2021 na Aprili 2022**

| Fungu | Jina la Fungu | Kiasi |
|---|---|---|
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 629,041,408,131.00 |
| 23 | IdarayaMhasibuMkuuwaSerikali | 60,126,687,875.95 |
| 50 | Wizara ya Fedha naMipango | 396,549,202.00 |
| **JUMLA** | | **689,564,645,208.95** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

### 3.1.2 Matumizi

***9. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ya Fedha na Mipango iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 13.26 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu yake saba (7) ya kibajeti pamoja na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 11.99 ni matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.27 ni matumizi ya maendeleo.

***10. Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2022, mafungu ya Wizara pamoja na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi yametumia jumla ya shilingi trilioni 9.64 sawa na asilimia 72.6 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 9.04 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 597.55 ni matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizotumika kwa kila Fungu ni kama inavyoonekana katika kiambatisho Na. 1– 3.

### 3.2 Utekelezaji wa Majukumu

***11. Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2021/22 unaendelea kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

i) kufanya mapitio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 – 2025/26) na kuanza maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050;

ii) kufanya tafiti za kiuchumi na modeli za fedha ili kubaini fursa fiche za uwekezaji na vyanzo vipya vya mapato, ikiwa ni pamoja na mapato ya kugharamia shughuli za Muungano;

iii) kufanya tathmini ya kina ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali ili kubaini maeneo yenye upungufu au changamoto na kupendekeza hatua stahiki za kuchukua;

iv) kufanya tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali;

v) kuratibu mipango na mikakati ya upatikanaji wa misaada, mikopo yenye masharti nafuu pamoja na mikopo yenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali;

vi) kutunga Sera ya Maendeleo ya Sekta ya Benki na Mkakati wake;

vii) kuandaa Mwongozo wa Usimamizi, Tathmini na Ufuatiliaji wa Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma;

viii) kufanya ufuatiliaji, tathmini, ukaguzi, udhibiti na uhakiki wa mapato, matumizi, miradi ya maendeleo,mali za umma; na miamala ya utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;

ix) kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya PPP;

x) kukamilisha maandalizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Programu na Miradi ya Maendeleo;

xi) kufanya maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022;

xii) kuhuisha Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu na Mkakati wa utekelezaji wake;

xiii) kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Bahari (*National Strategy for Blue Economy*);

xiv) kuwajengea uwezo watumishi kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu matumizi ya mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mapato, matumizi na mali za Serikali, hususan MUSE, GEPG na GAMIS;

xv) kuimarisha usalama na ulinzi wa mifumo ya TEHAMA pamoja na mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mapato, matumizi na mali za Serikali; na

xvi) ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli pamoja na maandalizi ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Usimamizi wa Mali za Serikali, Geita.

***12. Mheshimiwa Spika,*** kati ya Julai 2021 na Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

**3.2.1 Usimamizi wa Sera za Uchumi Jumla**

***13. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliweka malengo na shabaha za uchumi jumla kama msingi wa kubuni na kutunga sera zenye mwelekeo wa kujenga uchumi jumuishi, himilivu na endelevu. Ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 ulikua kwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la ukuaji wa uchumi limetokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Wizara ikiwemo: Kuwezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kurejea katika hali ya kawaida baada ya kuathirika na UVIKO -19; na kuwezesha upatikanaji wa mkopo nafuu usio na masharti kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wa shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi UVIKO-19.

***14. Mheshimiwa Spika,*** mfumuko wa bei umeendelea kubaki chini ya asilimia 5.0 kama ilivyotarajiwa katika kipindi cha muda wa kati. Mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2020. Aidha, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Ongezeko la mfumuko wa bei limetokana na: kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia kutokana na athari za UVIKO-19 na vita baina ya Urusi na Ukraine; kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma, hususan bidhaa ya petroli, mafuta ya kula, mbolea, chuma na malighafi za viwandani katika soko la dunia; na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya ndani kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Pamoja na ongezeko hilo, kiwango hicho bado kipo ndani ya matarajio ya wigo wa nchi wa kati ya asilimia 3.0 – 5.0 na lengo la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki la asilimia 8.0.

#### 3.2.2 Usimamizi wa Mpango na Bajeti ya Serikali

#### 3.2.2.1 Mpango wa Maendeleo wa Taifa

***15. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambao uliidhinishwa na Bunge lako Tukufu Aprili 2021. Mpango huo ni mwendelezo wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na mipango na mikakati ya maendeleo ya kikanda na kimataifa.

***16. Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kukamilisha maandalizi ya nyaraka za mapitio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025;

(ii) kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ambao uliwasilishwa katika Bunge lako Tukufu Machi 2022, na baadaye utawasilishwa tena mbele ya Bunge lako Juni 2022 kwa idhini;

(iii) kufanya uchambuzi wa maombi ya fedha kwa miradi ya kimkakati 38 kutoka halmashauri 28 yenye thamani ya shilingi bilioni 288.06, ambapo Wizara iliridhia maombi ya shilingi bilioni 201.80 yaliyokidhi vigezo;

(iv) kukamilisha na kusambaza Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu za Maendeleo;

(v) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ujenzi wa madarasa 15,000 na mabweni 50 yaliyojengwa chini ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya athari za Kiuchumi na Kijamii za UVIKO-19, mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kati kwa *Standard Gauge,* mradi wa Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi (M 3,200) na Barabara Unganishi (Km 1.66), Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115; na

(vi) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi 173 ya maendeleo katika sekta za; Kilimo, Viwanda, Utawala bora, Ujenzi, Uchukuzi, Maji, Elimu, Afya, Biashara na Mifugo katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Geita, Kagera, Mara na Simiyu. Sekta hizo zimepewa kipaumbele kwa kuwa sehemu kubwa ya fedha za maendeleo zimeelekezwa katika maeneo hayo.

**3.2.2.2 Usimamizi wa Bajeti ya Serikali**
**3.2.2.2.1 Mapato ya ndani**

***17. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilikadiriwa kuwezesha na kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 25.69, ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Aprili 2022, ukusanyaji wa mapato ya Serikali umefikia shilingi trilioni 19.99, sawa na asilimia 93.3 ya makadirio ya kukusanya shilingi trilioni 21.42 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yamefikia shilingi trilioni 17.20, sawa na asilimia 94.5 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 18.2. Aidha, Wizara imewezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali kukusanya mapato yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 2.03, sawa na asilimia 81.2 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 2.5 na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi bilioni 759.0, ikiwa ni asilimia 104.8 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 724.1 katika kipindi hicho.

**3.2.2.2.2. Misaada na Mikopo**

***18. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kuratibu upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi trilioni 4.99 kutoka katika soko la fedha la ndani na shilingi trilioni 3.05 kutoka katika masoko ya nje yenye masharti ya kibiashara ili kuziba nakisi ya bajeti. Hadi Aprili 2022, Wizara imefanikisha upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi trilioni 4.12 kutoka katika soko la fedha la ndani, sawa na asilimia 98.11 ya makadirio ya kukopa shilingi trilioni 4.20 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 2.63 zimegharamia mikopo ya ndani iliyoiva na shilingi trilioni 1.49 zimegharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara

imefanikisha upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi trilioni 1.81 kutoka katika masoko ya nje yenye masharti ya kibiashara, sawa na asilimia 79 ya makadirio ya kukopa shilingi trilioni 2.28 katika kipindi hicho.

***19. Mheshimiwa Spika***, Washirika wa Maendeleo waliahidi kuchangia katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/22 shilingi trilioni 4.25, ikijumuisha misaada shilingi trilioni 1.14 na mikopo nafuu shilingi trilioni 3.11. Aidha, kati ya shilingi trilioni 4.25 zilizoahidiwa, misaada na mikopo nafuu ya kibajeti ni shilingi trilioni 1.31, Mifuko ya Pamoja ya Kisekta ni shilingi bilioni 270.4; na miradi ya maendeleo ni shilingi trilioni 2.67.

***20. Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2022, shilingi trilioni 3.93 zimepokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 106.1 ya makadirio ya kupokea shilingi trilioni 3.70 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, misaada na mikopo nafuu ya bajeti ni shilingi trilioni 1.36, sawa na ufanisi wa asilimia 104.0, misaada na mikopo nafuu ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta ni shilingi bilioni 92.4, sawa na ufanisi wa asilimia 34.8 na misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ni shilingi trilioni 2.47, sawa na ufanisi wa asilimia 116.3 ya makadirio ya kipindi hicho. Aidha, misaada na mikopo nafuu ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta haikufikia lengo kutokana na kutokamilika kwa wakati kwa taratibu za utoaji fedha kwa baadhi ya Washirika wa Maendeleo, kuchelewa kukamilika kwa taratibu za ununuzi kwa baadhi ya programu na baadhi ya Washirika wa Maendelo kubadilisha taratibu za utoaji fedha.

**3.2.2.2.3 Utoaji fedha, ufuatiliaji na uhakiki wa malipo, madai, malimbikizo ya mishahara na madeni**

***21. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2022, jumla ya shilingi trilioni 29.40 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 10.61 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, shilingi trilioni 7.27 kwa ajili ya kuhudumia deni la Serikali, shilingi trilioni 6.73 kwa ajili ya mishahara na shilingi trilioni 4.79 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

***22. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2022, Wizara imefanya ufuatiliaji na uhakiki wa matumizi ya fedha zilizovuka mwaka 2020/21 katika maeneo yafuatayo: Sekretarieti za Mikoa tisa (9) na Halmashauri 36; Bohari Kuu ya Dawa (MSD); Miradi ya Maji inayotekelezwa na RUWASA na Ofisi za Mamlaka za Maji za Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Dar-es-Salaam, Shinyanga, Kagera, Arusha, Manyara na Songwe; vyuo vya kilimo; na fidia ya Bararaba ya Mzunguko Dodoma, Reli ya kisasa (SGR) katika njia ya kuingia Bandarini, Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Awamu ya Pili - Barabara ya Kilwa na Kiwanja cha Ndege Shinyanga, Tanga na Manyara, Kituo cha Kitaifa cha Maafa, na maeneo yanayotwaliwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania Kaboya (Muleba), Nyamisangura (Tarime), Usule (Tabora) na Nyangungulu (Mwanza).

***23. Mheshimiwa Spika,*** kati ya Julai 2021 na Aprili 2022, Wizara imefanya uhakiki wa taarifa mbalimbali za malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma 76,404 ambapo kati ya hao, 74,670 utumishi wao haujakoma na 1,734 ni wale ambao utumishi wao umekoma. Baada ya uhakiki kukamilika, jumla ya shilingi bilioni 124.32 zimelipwa kwa watumishi ambao utumishi wao haujakoma na shilingi bilioni 5.98 kwa watumishi waliostaafu. Vilevile, madeni ya jumla ya shilingi bilioni 772.87 yalihakikiwa na kulipwa. Kati ya kiasi hicho, madai ya wakandarasi ni shilingi bilioni 4.24, wazabuni shilingi bilioni 81.67, watumishi (yasiyo ya kimshahara) shilingi bilioni 25.71, watoa huduma shilingi bilioni 52.74 na madeni mengineyo shilingi bilioni 608.51.

**3.2.3 Usimamizi wa Deni la Serikali**

***24. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia deni la Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134. Kati ya Julai 2021 na Aprili 2022, Wizara imelipa deni lote lililoiva katika kipindi hicho la jumla ya shilingi trilioni 6.81. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 4.21, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.72 na mtaji shiling trilioni 2.49. Aidha, deni la nje ni shilingi trilioni 2.60, ikijumuisha riba shilingi trilioni 0.572 na mtaji shilingi trilioni 2.02.

***25. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni kufanya tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali kwa miaka 20 ijayo, kuanzia 2021/22 hadi 2040/41. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wakati na mrefu. Aidha, Taarifa inaonesha kuwa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 31.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, wananchi na wadau wote wa maendeleo kuwa Taarifa kamili ya tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *www.mof.go.tz.*

### 3.2.4 Usimamizi wa Mafao ya Wastaafu na Mirathi

***26. Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha mfumo wa huduma ya pensheni, mirathi, utunzaji wa kumbukumbu, uhakiki wa wastaafu na ulipaji wa mafao na pensheni kwa watumishi wa Serikali ambao siyo wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii, pamoja na mirathi na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio katika mikataba na viongozi wa kisiasa. Hadi Aprili 2022, Wizara imelipa mafao na pensheni kwa wastani wa wastaafu 59,825 kila mwezi, mirathi kwa warithi 1,038, malipo ya malezi kwa walezi 1,246 na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio kwenye mikataba 500. Aidha, Wizara inaendelea kufanya uhakiki wa wastaafu wote wanaopata malipo ya pensheni kupitia Hazina

### 3.2.5 Usimamizi wa Mifumo ya Fedha na Mali za Serikali

***27. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kuhuisha na kufungamanisha mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha na mali za Serikali ili kudhibiti upotevu wa mapato na matumizi yasiyo ya lazima pamoja na kurahisisha upatikanaji na usuluhishi wa taarifa za fedha kwa wakati. Aidha, Wizara ilipanga kuimarisha usalama na ulinzi wa mifumo ya TEHAMA pamoja na mifumo ya usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali na kufanya uhakiki wa mali katika vituo 180 katika Taasisi za Umma, Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa.

***28. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kuhuisha na kufungamanisha Mfumo wa Ulipaji Serikalini (*MUSE*) na mifumo ya *PlanRep I* (TAMISEMI), *PlanRep II* (Msajili wa Hazina) na *GePG*. Mafanikio mengine ni kufungamanisha mfumo wa *GAMIS* na *GePG* na kuunganisha watoa huduma za malipo 853, benki 28 na mitandao saba ya simu katika mfumo wa *GePG*. Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha usalama na ulinzi wa mifumo ya TEHAMA kwa kuanzisha kituo cha utafiti na usimamizi wa usalama wa mifumo ya fedha.

***29. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni pamoja na: kufanya ukaguzi wa mali za Serikali katika vituo 126 kwa lengo la kudhibiti na kuimarisha matumizi ya mali husika; uhakiki maalumu wa mali na madeni ya Hospitali ya DAR *Group* ili kurejesha hospitali hiyo serikalini; na ukaguzi wa mali za mradi wa ECO - *Village adaptation of Climatic Change in Central Zone (Eco ACT*) zenye thamani ya shilingi bilioni 1.033, ikijumuisha ardhi ekari 270, majengo mawili, vyombo vya moto, mitambo na vifaa 256 ili kuzitambua na kuzigawanya kwa matumizi mengine baada ya mradi kukamilika.

**3.2.6 Usimamizi wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi**

***30. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara ilipanga kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Ubia 2021/22-2025/26, kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu miradi inayoibuliwa na kuandaliwa na Mamlaka za Serikali na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa Mamlaka za Serikali. Hadi Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Ubia kama ilivyopangwa na ushauri wa kitaalamu kwa miradi ya PPP 32 iliyowasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi mbalimbali za Serikali. Kati ya miradi hiyo, mradi wa Uendeshaji wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza umepata mbia na maandalizi ya majadiliano ya uendeshaji wa mradi yanaendelea. Aidha, miradi minne (4) ambayo ni Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne, ujenzi wa Jengo la biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere, Ujenzi wa Kiwanda cha kuzalisha Dawa na Vifaa Tiba na Kiwanda cha

Kutengeneza Simu ipo katika hatua za ununuzi; mradi mmoja (1) upo kwenye hatua ya mwisho ya upembuzi yakinifu; miradi saba (7) ipo kwenye hatua ya upembuzi yakinifu wa awali; na miradi 19 ipo katika hatua ya andiko dhana.

### 3.2.7 Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma

***31. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji wa kampuni tanzu za mashirika na taasisi za umma pamoja na mashirika 120 yaliyobinafsishwa. Hadi Aprili 2022, ufuatiliaji umefanyika na kubaini kuwa mashirika na taasisi zote za Serikali zina miliki jumla ya kampuni tanzu 57. Aidha, Mfumo wa Taarifa za Fedha wa Ofisi ya Msajili wa Hazina (OTRMIS) umeboreshwa ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa za kifedha za kampuni tanzu na kurahisisha usimamizi wake. Vilevile, Mwongozo wa uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa kampuni tanzu za Taasisi na Mashirika ya Umma umekamilika na kuanza kutumika. Pia, ufuatiliaji na tathmini imefanyika katika mashirika 98 yaliyobinafsishwa, ikijumuisha hoteli 10, kampuni 31, mashamba 15 na viwanda 42. Matokeo ya ufuatiliaji huo yamebaini kiwango kidogo cha uzalishaji wa zao la mkonge, baadhi ya mashamba kutoendelezwa na mengine kutelekezwa.

### 3.2.8 Usimamizi wa Sekta ya Fedha

#### 3.2.8.1 Mifumo ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha

***32. Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kushirikiana na taasisi na mamlaka za usimamizi na udhibiti katika kusimamia na kuendeleza sekta ya fedha. Hadi Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kuhuisha rasimu ya Sera ya Taifa ya Bima; kuzindua Mpango wa Kutoa Elimu ya Fedha kwa Umma wa mwaka 2020/21 - 2024/25 pamoja na nyenzo ya kufundishia; kuandaa wiki ya Huduma za Fedha kitaifa kwa lengo la kutoa elimu ya fedha kwa umma; kuandaa rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Sekta ya Benki na Mkakati wake; kuandaa Mkakati wa Upatikanaji wa Fedha kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati; na kuzindua Mkakati

wa Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Njia Mbadala (*Alternative Project Financing – APF Strategy)*.

***33. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni kuandaa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Mali Zinazohamishika Sura 210, kwa lengo la kujumuisha masuala ya mikopo salama na masijala ya dhamana pamoja na mapendekezo ya uendelevu wa Mifuko ya Dhamana kwa Wajasiriamali Wadogo na Mauzo Nje ya Nchi (SME na Export Credit Guarantee Scheme).

### 3.2.8.2 Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

***34. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/22, Wizara kupitia Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipanga kuongeza bidhaa 38 ili kuimarisha ukwasi katika masoko ya mitaji; kuboresha kanuni za soko la hisa; kutoa leseni 150 kwa watendaji na washauri wa uwekezaji katika masoko ya mitaji; kuongeza idadi ya wataalamu wa masoko ya mitaji wanaokidhi viwango vya kimataifa kutoka 601 hadi 650; na kutoa elimu kwa umma. Hadi Aprili 2022, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imefanikiwa kutoa leseni 154 ikilinganishwa na leseni 144 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia 7 na kuongeza idadi ya watendaji wa masoko ya mitaji wanaotambulika kimataifa kutoka 601 hadi 667, sawa na ongezeko la asilimia 11. Aidha, idadi ya bidhaa katika masoko ya mitaji ambazo zinajumuisha hisa; hatifungani; na mifuko ya uwekezaji wa pamoja zimeongezeka kutoka 599 na kufikia 637, sawa na ongezeko la asilimia 6.

***35. Mheshimiwa Spika,*** Soko la Bidhaa Tanzania – TMX lilipanga kuboresha Mfumo wa Uuzaji na Malipo kwa Njia ya Kielektroniki, kuandaa Sera ya TEHAMA, Sera ya usalama wa Mifumo ya TEHAMA na kuandaa miongozo ya mauzo ya bidhaa. Hadi Aprili 2022, imefanikiwa kuboresha Mfumo wa Mauzo kwa Njia ya Kielektroniki na hivyo kuwa na uwezo wa kuuza mazao zaidi ya saba; kuandaa Sera ya TEHAMA na Sera ya Usalama ya TEHAMA kama sehemu ya kulinda mifumo inayotumika katika soko la bidhaa kwa ujumla; na kuandaa

miongozo ya mauzo ya zao la chai, mifugo hai, ngozi, viazi, vitunguu na pilipili manga ambayo itaanza kutumika kuuza mazao hayo kupitia Soko la bidhaa mara baada ya maandalizi ya Stakabadhi za Ghala kukamilika.

**3.2.8.3 Taasisi za Benki**

***36. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia taasisi za benki ili kukuza mitaji, amana na ukwasi na hivyo kuchochea kasi ya utoaji wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji na biashara katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kama ifuatavyo:

**3.2.8.3.1 Benki Kuu ya Tanzania**

***37. Mheshimiwa Spika***, shabaha ya ukuaji wa Pato la Taifa ilikuwa ni asilimia 5.0 mwaka 2021 na mfumuko wa bei kubaki ndani ya wigo wa kati ya asilimia 3.0 na 5.0. Ili kufikia azma hiyo, Benki Kuu ilipanga kukuza wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kwa asilimia 10.0; ukuaji wa fedha taslimu (M0) wa wastani wa asilimia 9.9; wastani wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa asilimia 10.6; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

***38. Mheshimiwa Spika**,* hadi Aprili 2022 wastani wa fedha taslimu uliongezeka kwa asilimia 13.8 ikilinganishwa na asilimia 2.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2021; ujazi wafedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 13.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021; na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 8.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.3 kwa mwaka 2021. Aidha, akiba za fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 5.46 kiasi ambacho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.8 ikilinganishwa na lengo la nchi la miezi 4.0 na miezi isiyopungua 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**3.2.8.3.2 Benki za Maendeleo**

***39. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia benki mbili (2) za maendeleo ambazo ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB na Benki ya Maendeleo TIB. Kwa mwaka 2021/22, TADB ilipanga kutoa mikopo ya kiasi cha shilingi bilioni 203.50 kwa miradi ya uchakataji wa mazao, ununuzi wa mazao, ununuzi wa pembejeo, uwezeshaji wa wakulima wadogo kupitia vyama vya msingi (AMCOS); ununuzi wa zana za kilimo; kutoa dhamana kwa wakulima wadogo na SMEs; na kufungua Ofisi ya Kanda ya kusini na ofisi ndogo Morogoro. Hadi Aprili 2022, TADB imetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 116.36 kwa miradi 181 iliyowanufaisha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa 1,527,175 na kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa toka benki ilipoanza kufikia shilingi bilioni 364.50.

***40. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na TADB ni pamoja na: kutoa mikopo ya shilingi bilioni 54.37 kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (SCGS) na kufanya mikopo iliyotolewa na mfuko huo kufikia shilingi bilioni 144.04 tangu ulipoanza rasmi udhamini wa mikopo mwaka 2018. Mikopo hiyo imewanufaisha wakulima 987, biashara ndogo na za kati za kilimo (SMEs), na vyama vya msingi (AMCOS) katika mikoa 26 nchini. Vilevile, TADB imefungua Ofisi ya kanda ya Kusini iliyopo mkoani Mtwara na Ofisi ndogo Mkoani Morogoro. Ofisi ya Kanda ya Kusini itahudumia Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma.

***41. Mheshimiwa Spika,*** benki ya Maendeleo TIB ilipanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 54.59 katika sekta ya kilimo, viwanda, maji, nishati, utalii, na elimu; na kukuza mizania ya benki kufikia shilingi 775.5. Hadi Aprili 2022, Benki ya Maendeleo TIB imefanikiwa kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 17.91. Sekta zilizonufaika na mikopo hiyo ni maji, utalii, madini ya dhahabu na ujenzi. Aidha mizania ya benki ilikua na kufikia shilingi bilioni 625.78.

**3.2.8.3.3 Benki ya TCB**

***42. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Benki ya TCB ilipanga kuboresha mifumo ya benki ya kuzalisha mapato na

utoaji huduma. Hadi Aprili 2022, benki imefungua akaunti 29,488 za vikundi vya kawaida na kusajili vikundi 43,236 kupitia simu za mkononi kwa kushirikiana na Vodacom. Aidha, benki imebuni mradi wa vikundi vilivyombali na huduma za kifedha, ambapo jumla ya akaunti 16,558 zimefunguliwa. Vilevile, benki imefanikiwa kukusanya amana zenye thamani ya shilingi bilioni 937 na kutoa mikopo ya shilingi bilioni 736, ambapo shilingi bilioni 1.4 ni mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali.

**3.2.8.3.4 Taasisi za Bima**

***43. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima - TIRA ilipanga kufanya ukaguzi wa vyombo vya moto barabarani kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, kusimamia vipindi 10 vya redio vya utoaji elimu na kutoa elimu kwa makundi maalumu ya Bodaboda, Bajaji, Vyama vya wafanyabiashara, vyama vya wasafirishaji pamoja na Jeshi la Polisi. Hadi Aprili 2022,TIRA imefanya ukaguzi wa vyombo vya moto barabarani 19,221; kutoa elimu ya bima kwa umma kupitia vipindi 9 vya redio na luninga na makundi mbalimbali ya kijamii ambapo zaidi ya wananchi 514,112 wamefikiwa. Kati ya hao, 3,214 ni askari polisi wa usalama barabarani, 344 watumishi wa Serikali, 75 waandishi wa habari na watumishi wa vyombo vya Habari na 510,479 madereva wa bodaboda, watu wenye ulemavu wa usikivu, wakulima na vyama vya ushirika.

***44. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Shirika la Bima la Taifa lilipanga kujenga mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Bima ili kuweka mazingira wezeshi na shindani. Hadi Aprili 2022, Shirika limefanikiwa kuanza kuunda na kujenga Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Bima na kuanza kusimika mfumo wa *Enterprise Resource Management System (ERMS)* kwa ajili ya kusimamia taarifa za kihasibu. Mifumo hiyo kwa pamoja inatarajiwa kuongeza ufanisi na uwazi katika utunzaji wa taarifa za wateja, ulipaji wa madai, utunzaji sahihi wa taarifa za kihasibu pamoja na kuwezesha wateja kukata bima na kuwasilisha madai yao kwa njia ya kielektroniki.

**3.2.8.3.5 Taasisi za Uwekezaji na Uwezeshaji**

***45. Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia taasisi mbili (2) za Uwekezaji na Uwezeshaji ambazo ni Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS na Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha (Self Microfinace Fund). Katika mwaka 2021/22, UTT AMIS ilipanga kuongeza rasilimali za mifuko kwa asilimia 15, kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia tano (5) na kutoa huduma kwa wawekezaji kwa kutumia mifumo ya kidijitali. Hadi Aprili 2022, UTT AMIS ilifanikiwa kuongeza rasilimali za mifuko pamoja na huduma ya usimamizi wa mitaji binafsi kutoka shilingi bilioni 619.57 mwezi Julai 2021 hadi shilingi bilioni 927.45 mwezi Aprili 2022, sawa na ongezeko la asilimia 49.69. Katika kipindi hicho, idadi ya wawekezaji katika mifuko iliongezeka kutoka 172,242 hadi 194,632, sawa na ongezeko la asilimia 12.99. Kutokana na maboresho ya mifumo ya TEHAMA, asilimia 46.10 ya mauzo ya vipande katika kipindi hicho yalifanyika kwa njia ya kidijitali.

***46. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF ulipanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 34.32 kwa wajasiriamali wadogo 17,852 na kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo wapatao 265. Hadi Aprili 2021, Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 32.97, sawa na asilimia 96 ya lengo na kunufaisha wajasiriamali wadogo 13,744 na kutoa mafunzo kwa wajasiriamli wadogo 2,397.

**3.2.6 Taasisi za Mafunzo, Elimu ya Juu na Bodi za Kitaaluma**

***47. Mheshimiwa Spika****,* Wizara inasimamia Taasisi za mafunzo ya elimu ya juu na bodi za kitaaluma kwa lengo la kuendeleza wataalamu na kufanya tafiti katika fani ya fedha na uhasibu, mipango, takwimu, ununuzi na ugavi na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu fani hizo. Taasisi hizo ni: Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini – IRDP; Chuo cha Usimamizi wa Fedha - IFM; Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – EASTC; Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA; Chuo cha Uhasibu Arusha – IAA; Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA.

#### 3.2.6.1 Taasisi za Mfunzo na Elimu ya Juu

#### 3.2.6.1.1 Chuo cha Usimamizi wa Fedha

***48. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kilipanga kutekeleza yafuatayo: Kudahili wanafunzi 14,500; kujenga uwezo wa Chuo wa kutoa huduma elekezi; kuendelea na ujenzi wa Kampasi za Kanda ya Ziwa – Simiyu na Chato na kuendeleza kampasi ya Mwanza. Hadi Aprili 2022, Chuo kimedahili wanafunzi 15,528, sawa na asilimia 107 ya lengo; kuwezesha wahadhiri kuchapisha jumla ya tafiti 18; na kutoa huduma elekezi nne (4) zenye thamani ya shilingi milioni 136.50 kwa taasisi mbalimbali, ikiwemo taasisi za Serikali.

***49. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Chuo kimekamilisha ujenzi wa majengo manne (4) katika Kampasi ya Chato mkoani Geita, ikiwemo Jengo la Utawala, Madarasa, Bwalo la Chakula na Ukumbi wa Mihadhara, ambapo ujenzi wa kampasi hiyo umefikia asilimia 78. Aidha, Chuo kimefanikiwa kununua ekari 37.42 katika eneo la Kiseke kwa ajili ya kampasi ya Mwanza, ambapo ujenzi umeanza kwa jengo la ghorofa nne (4) litakalokuwa na ofisi, madarasa, maabara ya kompyuta na maktaba.

#### 3.2.6.1.2 Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini – IRDP

***50. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kilipanga kudahili wanafunzi 15,011 katika kozi 27 za muda mrefu; kutoa udhamini wa masomo kwa watumishi katika ngazi ya uzamili na uzamivu; na kuanza ujenzi wa jengo la ukumbi wa mihadhara na bweni la wanafunzi katika kampasi ya Kanda ya Ziwa (Kisesa) – Mwanza. Hadi Aprili 2022, Chuo kimefanikiwa kudahili jumla ya wanafunzi 14,417, sawa na asilimia 96 ya lengo. Aidha, Chuo kimetoa udhamini wa masomo kwa watumishi 62 ambapo kati ya hao, 34 ni ngazi ya uzamivu, 16 uzamili, nane (8) shahada na wanne (4) stashahada. Vilevile, Chuo kimefanikiwa kufanya tafiti 7 katika masuala ya ukuaji wa uchumi na hali ya umaskini; usambazaji wa umeme vijijini na maendeleo ya viwanda vidogo; mchango na uhusiano wa

kijinsia katika upatikanaji wa maji vijijini; na shughuli za ujasiliamali vijijini.

***51. Mheshimiwa Spika***, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Chuo kinaendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara na bweni la wanafunzi katika Kampasi ya Kanda ya Ziwa (Kisesa) – Mwanza. Hadi Aprili 2022, ujenzi wa ukumbi wa mihadhara umefikia asilimia 80 na bweni la wanafunzi asilimia 20. Aidha, katika kipindi hicho, Chuo kimekamilisha ujenzi wa jengo la maktaba, jengo la utawala na bwalo la chakula katika Kampasi ya Kanda ya Ziwa, Kisesa.

### 3.2.6.1.3 Chuo cha Uhasibu Arusha – IAA

***52. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Chuo cha Uhasibu Arusha- IAA kilipanga kudahili jumla ya wanafunzi 9,870, ikiwemo ngazi ya cheti 2,646, stashahada 2,678, shahada 3,767 na uzamili 779. Aidha, Chuo kilipanga kuendeleza shughuli za utafiti pamoja na mafunzo kwa watumishi, kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu na kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa vyenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 4,800 katika kampasi kuu Arusha, mabweni manne (4), jengo la uzamili, ujenzi wa madarasa na jengo la utawala katika kampasi ya Babati.

***53. Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2022, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 7,483, sawa na ufanisi wa asilimia 75.8, ambapo ngazi ya cheti wamedahiliwa wanafunzi 2,646, stashahada wanafunzi 1,762, shahada wanafunzi 2,160 na shahada ya uzamili 915. Kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Chuo kimekamilisha ujenzi wa madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 4,800 katika kampasi kuu Arusha.

### 3.2.6.1.4 Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA

***54. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Taasisi ya Uhasibu Tanzania ilipanga kudahili jumla ya wanafunzi 24,866 na kuendeleza ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali ya Taasisi katika kampasi kuu Dar es Salaam, Mtwara, Mbeya na Mwanza. Hadi Aprili 2022, Taasisi imefanikiwa kudahili jumla

ya wanafunzi 23,621, sawa na ufanisi wa asilimia 95, ambapo ngazi ya cheti wamedahiliwa wanafunzi 4,954, ngazi ya stashahada 7,499, shahada11,106, stashahada ya uzamili 10 na shahada ya uzamili 52.

***55. Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Taasisi imekamilisha ujenzi wa jengo la taaluma na kuendelea na ukarabati wa jengo la utawala kampasi ya Makao Makuu, Dar es salaam, kuendelea na ujenzi wa hosteli mbili (2), vyumba vinne (4) vya madarasa, nyumba moja (1) ya wafanyakazi, maktaba moja (1) na maabara moja (1) ya kompyuta katika kampasi ya Mtwara na kuanza ujenzi wa jengo la taaluma linalojumuisha maabara ya kompyuta, maktaba na ofisi za utawala katika kampasi ya Mwanza.

### 3.2.6.1.5 Chuo cha Takwimu Mashariki Mwa Afrika – EASTC

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kilipanga kudahili jumla ya wanafunzi 500, kuendeleza wahadhiri 37, kutoa mafunzo ya muda mfupi kulingana na mahitaji ya wadau, kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza, kupitia upya na kutengeneza mitaala mipya ya programu za chuo na kuboresha mfumo wa kutoa mafunzo kwa njia ya masafa au kidijitali.

***57. Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2022, Chuo kimefanikiwa kudahili jumla ya wanafunzi 439, sawa na ufanisi wa asilimia 88, ambapo ngazi ya astashahada wamedahiliwa wanafunzi 38, stashahada 106, shahada 267 na 26 katika ngazi ya uzamili. Aidha, katika kipindi hicho, Chuo kimetoa udhamini wa masomo kwa wahadhiri 37, kuboresha miundombinu ya madarasa kwa kufunga viti vyenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 180 badala ya wanafunzi 80 wa awali, kukamilisha maandalizi ya mitaala mipya kwa ngazi ya cheti, Stashahada na Shahada ili kukidhi mahitaji ya muda wa kati na mrefu ya wataalamu wa fani ya takwimu rasmi, uchumi na TEHAMA na kuanza kutoa mafunzo kwa njia ya mtandao kwa waalimu na wanafunzi.

#### 3.2.6.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu

***58. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia Bodi mbili (2) za kitaaluma na kitaalamu ambazo ni Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi - PSPTB na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA. Katika mwaka 2021/22, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ilipanga kudahili watahiniwa 4,000 na kuendesha mitihani ya kitaaluma na kitaalamu, kujenga uwezo wa wataalamu, kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi, kusimamia ubora wa kazi za wataalamu na wanataaluma pamoja na kufanya usajili wa wataalamu wa fani ya Ununuzi na Ugavi. Hadi Aprili 2022, PSPTB imefanikiwa kudahili watahiniwa 1,376 katika ngazi mbalimbali za mitihani, kuwajengea uwezo wataalamu 1,185 katika fani ya ununuzi na ugavi na kusajili wataalamu 1,444 wa ununuzi na ugavi katika ngazi mbalimbali za kitaalamu.

***59. Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA ilipanga kudahili watahiniwa 11,720, kufanya ukaguzi kwa taasisi 75 kuhusu uandaaji wa taarifa za fedha, kuendesha semina 30 na kutoa mafunzo ya diploma ya viwango vya uandaaji wa taarifa kwa watahiniwa 460. Hadi Aprili 2022, Bodi ilifanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha katika taasisi 81, kuendesha semina 21 kwa taasisi za Serikali, asasi za kiraia na sekta binafsi kuhusu matumizi vya viwango vya kimataifa (IPSAS na IFRS) katika utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za fedha, kutunga, kusimamia na kusahihisha mitihani kwa watahiniwa 7,008, ambapo 44 walifaulu mitihani ya Cheti cha Utunzaji wa Hesabu na 428 Shahada ya Juu ya Uhasibu na kutoa mafunzo ya diploma ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha serikalini kwa wahitimu 178.

***60. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ya NBAA ni pamoja na: Kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi kwa taasisi za umma na binafsi 12 Tanzania Bara; kufanya ukaguzi wa kampuni 50 za uandaaji na ukaguzi wa hesabu; na kusajili watunza vitabu wawili (2), wahasibu wahitimu 622 waliopata uzoefu wa kazi, wahasibu 85 ngazi ya ACPA, wakaguzi hesabu

36 katika ngazi ya CPA-PP, kampuni tatu (3) za ukaguzi wa hesabu na kampuni moja (1) ya uhasibu.

#### 3.2.7 Usimamizi wa Kodi na Rufaa za kodi

***61. Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia taasisi moja (1) ya ukusanyaji wa mapato ya kodi na taasisi mbili (2) za usimamizi na utatuzi wa mashauri ya kodi. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA, Bodi ya Rufaa za Kodi- TRAB na Baraza la Rufaa za Kodi-TRAT.

#### 3.2.7.1 Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA

***62. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Wizara kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania ilipanga kuanzisha mfumo wa ukaguzi wa mizigo uliofungamanishwa wa "Scanner", kujenga Mfumo wa Kielektroniki wa Dirisha Moja la Forodha, kujenga Mfumo Unganifu wa Kusimamia Mapato ya Ndani na kujenga Mfumo wa Utoaji Taarifa za Mrejesho kwa Walipakodi.

***63. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2022, TRA imefanikiwa kujenga mfumo uliofungamanishwa na *Scanner* na kuunganishwa na mfumo wa *TANCIS.* Mfumo huo unatumika katika uondoshaji wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Aidha, *scanner* nne (4) zimesimikwa katika Bandari ya Dar es Salaam na mbili (2) katika Bandari ya Tanga. Vilevile, Mamlaka imefanikiwa kujenga Mfumo wa Kielektroniki wa Dirisha Moja na kuunganisha mawakala wa forodha 545 pamoja na Taasisi za Udhibiti nne (4), ambapo hadi sasa unatumika katika Bandari ya Dar es Salaam na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

***64. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na TRA ni pamoja na: Kuendelea na ujenzi wa mfumo Unganifu wa Kusimamia Mapato ya Ndani (*Integrated Domestic Tax Administration System – IDRAS*) ili kurahisisha au kuwezesha uwasilishaji wa ritani za kodi, makisio ya kodi na malipo ya kodi. Aidha, moduli za Usimamizi wa Madeni na Kodi ya Ongezeko la Thamani -VAT ziko katika hatua mbalimbali za

uundwaji. Vilevile, Mfumo wa Utoaji Taarifa za Mrejesho kwa Walipakodi umekamilika na mafunzo yametolewa kwa wataalamu 201 kuhusu matumizi ya mfumo huo. Mfumo huo umeonesha mafanikio makubwa baada ya kufanyiwa majaribio katika Mikoa ya Geita na Njombe.

**3.2.7.2 Bodi ya Rufaa za Kodi – TRAB**

***65. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Bodi ya Rufaa za Kodi ilipanga kusikiliza mashauri ya kodi kwa wakati ili kuiwezesha Serikali kufanikisha azma yake ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara. Hadi Aprili 2022, Bodi imesajili maombi mapya 36 na mashauri mapya 394. Aidha, katika kipindi hicho, Bodi imesikiliza na kutolea maamuzi jumla ya maombi 65 na mashauri 510.

**3.2.7.3 Baraza la Rufani za Kodi – TRAT**

***66. Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Rufani za Kodi - TRAT lilipanga kusikiliza na kutolea maamuzi rufaa zote za kodi, kuandaa Mfumo wa Takwimu za Mashauri na kuchapisha vitabu vya rejea kwa kesi zilizoamuliwa kuanzia mwaka 2013 hadi 2020. Hadi Aprili, 2022, Baraza limefanikiwa kusikiliza mashauri 161 na kutolea maamuzi mashauri 142. Aidha, Mfumo wa Takwimu za Mashauri umekamilika na zoezi la kuchambua takwimu kwa ajili ya kuziingiza kwenye mfumo linaendelea. Vilevile, uchambuzi wa mashauri yaliyotolewa maamuzi mwaka 2013 umekamilika na kupelekwa kwa Mhariri kwa hatua ya uchapishaji.

**3.2.8 Usimamizi wa Masuala ya Pamoja ya Fedha kati ya Tanzania Bara na Zanzibar**

***67. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Tume ya Pamoja ya Fedha ilipanga kufanya stadi za masuala ya fedha ya pamoja kati ya Tanzania Bara na Zanzibar na kutoa ushauri stahiki kwa pande zote za Muungano. Hadi Aprili 2022, Wizara kupitia Tume imefanya Stadi kuhusu ukusanyaji wa mapato ya Muungano katika huduma za mawasiliano ya simu, fedha na bima kwa kampuni zilizosajiliwa upande mmoja wa

Muungano na kufanya biashara katika pande mbili za Muungano.

***68. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni pamoja na uchambuzi wa takwimu za mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa shughuli za Muungano kwa kipindi cha mwaka 2012/13 hadi 2021/22. Uchambuzi huo umeonesha kuwa, matumizi ya Muungano yalikuwa ya wastani wa asilimia 25.4 ikilinganishwa na matumizi ya Serikali (SMT). Aidha, uwiano wa mapato ya Muungano na mapato ya ndani ya SMT kwa kipindi cha kuanzia 2012/13 hadi 2021/22 yalikuwa ya wastani wa asilimia 49.8 na asilimia 35.8 kwa SMZ. Vilevile, Tume imetoa elimu kwa wadau kuhusu masuala ya uhusiano wa kifedha kati ya SMT na SMZ. Wadau waliopewa elimu hiyo ni wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ya SMT na wajumbe wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, Makatibu Wakuu wa Wizara na Wakuu wa Taasisi za SMZ.

**3.2.9 Michezo ya kubahatisha**

***69. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ilipanga kutoa leseni 11,367 kwa waendesha michezo ya kubahatisha, ambapo kati ya hizo 7,408 ni leseni mpya na 3,959 ni leseni zitakazohuishwa na kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 76 waliosajiliwa ili kudhibiti uvunjifu wa sheria na taratibu. Hadi Aprili 2022, Bodi imefanikiwa kutoa jumla ya leseni 6,974, ambapo leseni 4,799 ni mpya na 2,175 zimehuishwa. Vilevile, Bodi imeweza kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 65 na kuunganisha mifumo ya michezo ya kubahatisha na mfumo wa GEPG, BRELA na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA.

**3.2.10 Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi**

***70. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi ilipanga kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku, fedha taslimu, utumaji na upokeaji wa fedha

kwa njia za kielektroniki, usafirishaji wa fedha taslimu na hati za malipo kutoka na kuingia nchini kupitia mipakani, kuwasilisha taarifa fiche kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria na kushirikiana na wadau katika kuimarisha mifumo ya kupambana na utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi. Hadi Aprili 2022, Kitengo kilipokea na kuchambua taarifa fiche 658 za miamala shuku yenye thamani ya shilingi trilioni 1.568, taarifa 4,301 za fedha taslimu zenye thamani ya shilingi trilioni 36.15, taarifa 8,350 za usafirishaji fedha kwa njia ya kielektroniki zenye thamani ya shilingi trilioni 86.35 na taarifa 2,332 zenye thamani ya shilingi trilioni 2.482 zinazohusu usafirishaji wa fedha taslimu na hati za malipo kupitia mipakani. Aidha, taarifa fiche 32 ziliwasilishwa kwenye taasisi za utekelezaji wa sheria.

***71. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni pamoja na: Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu, SURA 423; kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 8 na Kasino 4 juu ya utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Udhibiti Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi; kuandaa miongozo ya usimamizi wa sekta ya bima na sekta ya masoko na mitaji ya dhamana; na kuunganisha *server* za Mamlaka ya Usajili wa Matukio ya Kijamii ya Zanzibar na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ili kubadilishana taarifa kwa urahisi na uharaka.

### 3.2.11 Taasisi za Ununuzi wa Umma

***72. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inajukumu la kusimamia na kudhibiti tasnia ya Ununuzi wa Umma na Ugavi kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma – PPRA, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini – GPSA na Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma - PPAA.

***73. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini ulipanga kusimika Mfumo wa Kielektroniki wa Uratibu wa Ununuzi wa Magari ya Serikali na kujenga matenki manne katika mikoa ya Shinyanga, Tabora, Kagera na Morogoro na kukarabati matenki mawili katika

mikoa ya Mwanza na Tanga. Hadi Aprili 2022, Wakala umefanikiwa kuunda Mfumo wa Kielektroniki wa Uratibu wa Ununuzi wa Magari ya Serikali, ugomboaji na uondoshwaji, pamoja na mfumo wa utoaji wa hati za madai, usimamizi na udhibiti wa vifaa na maghala (GIMIS), ambao umeanza kutumika rasmi Machi 2022. Aidha, Wakala umekamilisha Ujenzi wa matanki mawili (2) yenye uwezo wa kuhifadhi lita 40,000 za mafuta kila moja katika mikoa ya Tabora na Kagera na ujenzi unaendelea katika mikoa ya Lindi, Geita na Morogoro. Vilevile, wakala umekarabati matanki mawili katika mikoa ya Tanga na Mwanza.

***74. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ilipanga kufanya ukaguzi wa ununuzi katika taasisi 180, kutoa mafunzo kwa watumishi 1,200 kutoka kwa taasisi nunuzi 300 ambao wamesajiliwa katika mfumo wa ununuzi (TANePS) na kufuatilia uzingatiaji kwa taasisi nunuzi 120. Hadi Aprili 2022, PPRA imetoa mafunzo ya matumizi ya mfumo kwa watumishi 736, ambapo jumla ya Taasisi Nunuzi 530 zimeunganishwa na mfumo, kuunganisha wazabuni 26,691 kwenye Mfumo wa TANePS, kutoa mafunzo maalumu ya Sheria ya Ununuzi, SURA 410 kwa watumishi 346 kutoka Taasisi Nunuzi 11 na kuandaa warsha saba (7) kuhusu ununuzi wa umma, ambapo jumla ya washiriki 575 kutoka Taasisi Nunuzi walihudhuria. Aidha, Mamlaka ilifanya kaguzi za ununuzi kwa Taasisi Nunuzi 105 kwa miamala iliyofanyika mwaka 2020/21.

***75. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni - PPAA ilipanga kusikiliza na kutolea maamuzi rufaa 30 pamoja na kuendelea kuimarisha utawala bora katika masuala ya ununuzi wa umma. Hadi Aprili 2022, Mamlaka imepokea jumla ya mashauri 30 ambayo ni sawa na asilimia 100 ya rufaa zilizokadiriwa kwa mwaka. Mashauri 22 yaliyowasilishwa yamesikilizwa na kutolewa maamuzi ndani ya kipindi cha siku 45 zilizowekwa kisheria, mashauri manne (4) yako katika hatua ya kusikilizwa na mashauri manne (4) yaliondolewa na walalamikaji.

### 3.2.12 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

***76. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/22, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipanga kuendelea na zoezi la kutenga maeneo ya kuhesabia watu wakati wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 2022. Shabaha nyingine ni kutoa takwimu za Pato la Taifa za robo mwaka na takwimu za mfumuko wa bei kila mwezi. Hadi Aprili 2022, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanikiwa kuandaa na kutoa takwimu za Pato la Taifa za mwezi Julai hadi Desemba 2021 na mfumuko wa bei hadi Machi 2022.

***77. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Taifa ya Takwimu imekamilisha kazi ya kutenga maeneo ya kuhesabia watu kwa Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar ambapo vitongoji vyote 64,318 na mitaa 4,670 Tanzania Bara imetengwa, ikiwa ni ufanisi wa asilimia 100. Aidha, jumla ya maeneo ya kuhesabia watu 4,313 kutoka katika Shehia zote 388 yametengwa kwa upande wa Zanzibar, sawa na asilimia 100 ya lengo. Kazi nyingine zilizokamilika ni kuandaa madodoso ya Sensa ya Watu na Makazi, Sensa ya Majengo na Sensa ya Anwani za Makazi, miongozo na fomu za kudhibiti ubora; kuandaa mfumo wa ufuatiliaji (census Dash Board), kufanya Sensa ya Majaribio Agosti, 2021 katika mikoa 18 ya Tanzania Bara na Zanzibar na kuendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya Sensa.

### 3.2.6 Utekelezaji wa Maagizo ya Serikali

***78. Mheshimiwa Spika***, kama utakavyokumbuka, Serikali ilitoa maagizo kwa Wizara na taasisi za kisekta kutafsiri sheria zote katika lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi wa kawaida kusoma na kushiriki ipasavyo katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Hadi Aprili 2022, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kutafsiri jumla ya sheria 20 zinazohusiana na masuala ya fedha, takwimu, ununuzi na ugavi, kodi, bima, michezo ya kubahatisha, ukaguzi, masoko ya mitaji na dhamana, forodha na mafunzo kwa taasisi za elimu za Wizara.

### 3.2.7 Usimamizi wa Programu ya Maboresho ya Fedha za Umma

***79. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kufanya tathmini ya utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Fedha za Umma Awamu ya Tano -PFMRP V inayotarajiwa kufikia ukomo Juni 30, 2022 na kuandaa Mpango Mkakati wa Awamu ya Sita. Hadi Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kukamilisha tathmini ya Programu na kuandaa Mpango Mkakati wa Awamu ya Sita ambao utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka 2022/23. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imefanikiwa kuratibu zoezi la Tathmini ya Nchi kuhusu Uwajibikaji katika Usimamizi wa Fedha za Umma. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuimarika kwa mifumo ya usimamizi wa fedha za umma, hususan katika eneo la uchambuzi, udhibiti, utekelezaji na usimamizi wa bajeti na mali za Serikali.

### 3.2.8 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

***80. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipanga kukagua mapato na matumizi ya mafungu yote ya Serikali Kuu, ikiwemo mafungu 66, wakala 31 na balozi 42. Kazi nyingine ni kufanya ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa 185, Mikoa 26 na Mashirika ya Umma 192, kufanya kaguzi za Ufanisi 12 na kaguzi 8 za kiufundi, kufanya ukaguzi wa kina wa usimamizi wa Mikataba ya ujenzi katika Mamlaka 37 za Serikali za Mitaa, kukagua Miradi ya Maendeleo 442 inayotekelezwa kwa fedha za ndani pamoja na Washirika wa Maendeleo na kufanya kaguzi maalumu 15 katika maeneo au miradi mahsusi.

***81. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2022, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kufanya ukaguzi kwa Wizara, Idara za Zinazojitegemea 66; Wakala 31; Hospitali za Rufaa na Maalumu 33; Mifuko Maalumu ya Serikali 17; Mamlaka za Maji (Daraja C) pamoja na mabonde ya maji 29; Taasisi za Serikali 64; Balozi 43; Mikoa 26; Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa; Mashirika ya Umma 195; na ukaguzi wa Vyama vya Siasa 19

vyenye usajili wa kudumu. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kufanya kaguzi 12 za ufanisi na 8 za kiufundi. Pia, jumla ya kaguzi maalum 56 zimefanyika, ambapo 37 ni kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 12 Serikali Kuu, 6 Mashirika ya Umma na Moja kwenye Mifumo ya Tehama.

***82. Mheshimiwa Spika***, mafanikio mengine ni kufanya ukaguzi kwa Miradi ya Maendeleo 302, ikijumuisha Miradi 199 chini ya Sekta ya Afya, 11 Sekta ya Elimu, 16 Sekta ya Usafirishaji, 19 Sekta ya Nishati na Madini, 14 Sekta ya Jamii, 11 Sekta ya Maji na 32 kutoka katika sekta nyingine. Aidha, ulifanyika ukaguzi wa kina wa usimamizi wa mikataba ya RUWASA katika Mikoa 25.

### 3.3 Changamoto na Mikakati ya Kukabiliana nazo

#### 3.3.1 Changamoto

***83. Mheshimiwa Spika***, pamoja mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na taasisi zake, changamoto zifuatazo zilijitokeza:

i) kuvurugika kwa mfumo na mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia kutokana na athari za UVIKO-19 na vita baina ya Urusi na Ukraine na hivyo kusababisha ongezeko la mfumuko wa bei katika soko la ndani pamoja na kasi ndogo ya ukuaji wa Pato la Taifa;

ii) kusitishwa kwa baadhi ya mikataba ya ununuzi na ugavi wa vitendea kazi, hususan magari kutokana na athari za UVIKO – 19;

iii) kasi kubwa ya mabadiliko ya teknolojia ya habari na mawasiliano ikilinganishwa na uwezo wa ndani wa kuimarisha na kujenga mifumo ya TEHAMA pamoja na mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha; na

iv) kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ununuzi wa vitendea kazi kutokana na athari

za mfumuko wa bei na hivyo kuathiri utekelezaji wa Mpango na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

### 3.3.2 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto

***84. Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kuchukua hatua zifuatazo katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza:

i) kuchukua hatua za kisera, hususan kutoa ruzuku kwa bidhaa za petroli ili kupunguza kasi ya ongezeko la mfumuko wa bei na gharama za maisha;

ii) kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya baadhi ya mazao kama njia mbadala kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, hususan ngano na mafuta ya kula ili kudhibiti msukumo wa mfumuko wa bei kutoka nje;

iii) kufanya mazungumzo na wazalishaji na wauzaji mbalimbali wa magari na mitambo ili kuepuka au kupunguza athari zinazoweza kujitokeza;

iv) kuongeza uwekezaji katika ujuzi na utafiti wa masuala ya TEHAMA na mifumo ya kielektroniki ili kupunguza athari za utegemezi wa mifumo ya nje; na

v) kutoa kipaumbele kwa majukumu au kazi zenye maslahi mapana kwa Taifa, hususan miradi ya maendeleo na matumizi yaliyolindwa.

## 4.0 VIPAUMBELE KWA MWAKA 2022/23

### 4.1 Vipaumbele vya Wizara

***85. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango kupitia mafungu yake nane (8) inatarajia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia malengo, shabaha na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) wa kila Fungu na Taasisi zake. Aidha, malengo, shabaha na vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/23 vimeibuliwa kutoka kwenye

Mpango Mkakati wa Wizara 2021/22 – 2025/26, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 na Ilani ya Chama Tawala – CCM kama ifuatavyo:

i) kukusanya, kutafuta na kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali;

ii) kuhudumia kwa wakati deni la Serikali pindi linapoiva;

iii) kufanya tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ikiwa ni maandalizi mahsusi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo 2050;

iv) kufanya tathmini ya mfumo na muundo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ili kuwezesha kutungwa kwa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo;

v) kurejesha Bahati Nasibu ya Taifa;

vi) kufanya tafiti katika sekta za uzalishaji ili kuibua fursa za uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya Serikali katika muda mfupi, kati na mrefu;

vii) kuendelea kutekeleza maagizo ya Serikali ya kutafsiri sheria za Wizara na taasisi zake kwa lugha ya Kiswahili; na

viii) kuhuisha Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi.

***86. Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Wizara inatarajia kujielekeza katika maeneo yafuatayo:

i) kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI);

ii) kuandaa na kujenga ghala la takwimu (*Data warehouse*);

iii) kuratibu na kusimamia zoezi la Sensa ya Watu na Makazi;

iv) kuziwezesha taasisi za Wizara, hususan taasisi za elimu na mafunzo kuboresha miundombinu ya kujifunza na kufundishia;

v) kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli, Mtumba Dodoma;

vi) ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mhakikimali na Hazina Ndogo katika mkoa wa Geita, Njombe na Songwe; na vii)ukarabati wa jengo la Wizara lililopo Jijini Dar es Salaam, Hazina Ndogo Morogoro, Kigoma na Ruvuma.

**4.2 Vipaumbele vya Taasisi**

***87. Mheshimiwa Spika*,** Wizara inatekeleza baadhi ya majukumu yake kupitia taasisi za elimu na mafunzo na elimu ya juu, bodi za kitaalamu na kitaaluma, usimamizi wa fedha, kodi, bima, ununuzi na ugavi, michezo ya kubahatisha, uwekezaji na uwezeshaji pamoja na takwimu.

**Taasisi za Mafunzo ya Elimu ya Juu**

***88. Mheshimiwa Spika,*** taasisi za Mafunzo ya Elimu ya Juu zinatarajia kudahili jumla ya wanafunzi 73,074, ikiwemo ngazi ya cheti 14,017, stashahada 19,427, shahada 37,450 na uzamili 2,180. Aidha, Chuo kinatarajia kuendeleza wahadhiri 196, ambapo ngazi ya uzamivu ni 158 na Uzamili 38 pamoja na kuendeleza shughuli za ushauri na utafiti.

***89. Mheshimiwa Spika,*** shabaha za Chuo cha Usimamizi wa Fedha - IFM ni pamoja na: Kukamilisha ujenzi wa mabweni manne (4) yenye ghorofa moja moja yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400, nyumba nne (4) zenye uwezo wa kuhudumia familia nane (4) za wafanyakazi pamoja na maktaba moja (1) katika kampasi ya Gieta; kuendelea na ukarabati wa miundombinu katika kampasi ya Dar es Salaam na ujenzi wa jengo la taaluma likijumuisha ofisi zenye uwezo wa kuhudumia wahadhiri 40 na madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,520 kwa wakati mmoja katika kampasi ya Mwanza.

***90. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Chuo cha Uhasibu Arusha - IAA kinatarajia kutekeleza yafuatayo: kukamilisha ujenzi wa mabweni manne (4) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,000 katika kampasi kuu Arusha; kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala linalojumuisha madarasa 16, mabweni mawili yenye uwezo wa wakuchukua wanafunzi 1,000 na jengo moja (1) la utawala katika kampasi ya Babati; na kufanya mapitio ya mitaala kumi (10).

***91. Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2022/23, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - IRDP kimepanga kufanya tafiti saba (7) na kutoa huduma za ushauri elekezi kwa kuzingatia mahitaji ya wadau; kuwezesha mafunzo kwa watumishi 396; kukarabati nyumba 13 za watumishi katika kampasi kuu ya Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi na Maktaba katika Kituo cha Mafunzo, Kanda ya Ziwa Mwanza.

***92. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA imepanga kujenga jengo moja la utawala katika kampasi ya Misungwi, Mwanza na kampasi ya Kigoma; kujenga ukumbi moja (1) wa mihadhara, maabara ya Kompyuta moja (1) na Maktaba moja (1) katika Kampasi ya Mbeya; na kuboresha miundombinu na huduma mtandao (*internet service*) katika maktaba za kampasi zote.

***93. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika - EASTC kipanga kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala, kuendeleza wahadhiri 28 na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 20.

**Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu**

***94. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi inatarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi, kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 6,500 na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000. Aidha, Bodi ya NBAA inatarajia kusajili wahasibu 1,125 katika ngazi mbalimbali, kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma, kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa

za fedha kwa taasisi 75 na kutoa mafunzo ya diploma ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha serikalini kwa wahitimu 500.

**Taasisi za Usimamizi wa Kodi na Rufaa za Kodi**

***95. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA inatarajiwa kufanya yafuatayo: Kuhuisha Mkakati wa Muda wa Kati na Mrefu wa Ukusanyaji Mapato; kutunga upya Sheria na Kanuni za Ushuru wa Stempu na Bidhaa; kuanzisha Maabara ya Forodha; kutengeneza na kutekeleza Mfumo Unganifu wa Kusimamia Mapato ya Ndani na kuboresha Kituo cha Udhibiti na Ufuatiliaji wa Mifumo. Aidha, taasisi za rufaa za kodi zitaendelea kusajili, kusikiliza na kutoa maamuzi ya maombi, mashauri na rufaa za kodi ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini.

**Bodi ya Michezo ya kubahatisha**

***96. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha inatarajia kutoa leseni 7,697 kwa waendesha michezo ya kubahatisha, ambapo 1,923 ni leseni mpya na 5,774 ni leseni zitakazohuishwa; kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 83; kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Michezo ya kubahatisha; na kurejesha Bahati Nasibu ya Taifa.

**Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa**

***97. Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2022/23, Mamlaka ya Mosoko ya Mitaji na Dhamana – CMSA inatarajia kuanza kusimamia masoko ya mitaji kwa kutumia mfumo wa vihatarishi (*Risk Based Supervision*), kupanua wigo wa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa pamoja na kuongeza idadi ya bidhaa katika soko, hususan hisa, hatifungani na vipande katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja.

**Taasisi za Benki**

***98. Mheshimiwa Spika,*** ili kuchochea na kudhibiti ustawi wa viashiria vya uchumi jumla***,*** Benki Kuu ya Tanzania imepanga katika mwaka 2022/23 kukuza wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ili kuendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi, kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kudhibiti na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu pamoja na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

***99. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Benki ya TADB imepanga kutoa mikopo ya takribani shilingi bilioni 78 kwa sekta ya viwanda, hususan viwanda vya mafuta ya kula na sukari katika mkoa wa Kigoma, Shinyanga na Manyara. Mikopo hiyo inatarajia kupunguza upungufu wa mafuta ya kula na sukari hapa nchini.

Aidha, benki imepanga kutoa mkopo wa takribani shilingi bilioni 130 kwa ajili ya ununuzi wa pamba na kahawa.

***100. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Benki ya TIB imepanga kutoa mikopo ya takribani shilingi bilioni 47 kwa sekta ya viwanda, maji, nishati, madini, mafuta na gesi, huduma na utalii pamoja na kilimo; kukuza mizania ya benki kufikia shilingi billioni 902.63; kupunguza ukwasi kwa kuongeza mtaji wa benki kwa shilingi billioni 373; na kuuza hati fungani zenye thamani ya shilingi billioni 300.

***101. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Benki ya Biashara Tanzania – TCB imepanga pamoja na mambo mengine: Kuboresha uwezo wa benki wa kuzalisha mapato ili kufikia shilingi bilioni 185.6; kukuza faida ya benki kabla ya kodi ili kufikia shilingi bilioni 21.4; kutoa mikopo salama ya shilingi bilioni 709; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 974; kukuza mali za benki ili kufikia shilingi bilioni 1,257; na kukuza thamani ya hisa na kufikia shilingi bilioni 128.

**Taasisi za Bima**

***102. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania- *TIRA* inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kufanya uchambuzi wa mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 30 za bima nchini; kufanya ukaguzi wa kampuni 30 za bima, madalali 70, benki wakala 26 na mawakala 278; kufanya upekuzi wa kina ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato kwa kampuni 10; kutoa elimu ya bima kwa watu takribani milioni 1.5 kuhusu huduma za bima; na kuhamasisha kampuni za bima kuandaa bidhaa za bima kwenye sekta ya kilimo.

***103. Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Taifa la Bima linatarajia kupanua wigo wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa huduma za bima; kubuni bidhaa mpya nne (4) za bima; kuhamasisha na kufuatilia uandikishaji wa bima kwa Taasisi za Umma 100 ambazo hazijakata bima na NIC na kuandaa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (*Enterprise Risk Management Framework*).

**Taasisi za Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

***104. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kuongeza rasilimali za mifuko kwa kiwango cha asilimia 15; kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5; na kuhamasisha Taasisi za Serikali, Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS kujiunga na mifuko ya UTT AMIS. Aidha, Mfuko wa SELF unatarajia kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shillingi bilioni 43.5 kwa wajasiriamali 28,255 na kuhakikisha kiwango cha urejeshaji wa mikopo kinafikia asilimia 95; na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa 4,000.

**Usimamizi wa Takwimu Rasmi**

***105. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inatarajia kuratibu na kuwezesha Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, 2022, kufanya utafiti wa

Sekta isiyo rasmi na utafiti wa Afya ya Mama na Mtoto na kuendelea kutoa takwimu za msingi za uchumi kila mwezi, robo mwaka na nusu mwaka kulingana na aina ya takwimu.

**Usimamizi na Udhibiti wa Ununuzi wa Umma**

***106. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma - PPRA inatarajia kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma na ofisi ya kanda Jijini Dar es Salaam, kuwezesha mafunzo kwa watumishi 940 kutoka katika Taasisi Nunuzi 170 na wazabuni 1,200 ambao wamejisajili katika mfumo wa TANePS, kufanya mapitio na ujenzi wa mfumo mpya wa usimamizi wa ununuzi wa umma na kufuatilia utekelezaji wa Mikataba ya Ununuzi katika Taasisi Nunuzi 530.

***107. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini – *GPSA* unatarajia kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Kigoma, kituo cha mafuta katika mikoa ya Njombe, Pwani, Arusha na Wilaya ya Kahama na ujenzi wa ghala katika Wilaya ya Korogwe, Masasi na Dodoma. Aidha, PPAA imepanga kuandaa mfumo wa kielektroniki wa usajili na usimamizi wa rufaa za ununuzi wa umma na kufanya mapitio ya kanuni za rufaa.

**5.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2022/23**

**Maduhuli**

***108. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi trilioni 1.05 kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma na mauzo ya leseni za udalali. Mchanganuo wa maduhuli yanayokadiriwa kukusanywa kwa mafungu ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na.2: Maduhuli Yanayokadiriwa Kukusanywa na Mafungu ya Wizara kwa mwaka 2022/23**

| Fungu | Jina la Fungu | Kiasi |
|---|---|---|
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 988,254,978,000.00 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 60,100,000,000.00 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 1,000,000,000.00 |
| **JUMLA** | | **1,049,354,978,000.00** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

**Matumizi**

***109. Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Fedha na Mipango inawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maombi ya kuidhinishiwa jumla ya **shilingi trilioni 14.94** kwa mafungu yake nane (8), ili kugharamia matumuzi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka 2022/23. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 13.62** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 1.32** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi bilioni 85.52** kwa ajili ya Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 74.59** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 10.93** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa kila fungu umeainishwa katika **Jedwali Na.3.**

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2022/23.**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA | | | MATUMIZI YA MAENDELEO | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | MATUMIZI YA KAWAIDA | NDANI | NJE | JUMLA-MAENDELEO | |
| 1 | Deni la Serikali | - | 9,093,984,694,000 | 9,093,984,694,000 | - | - | - | 9,093,984,694,000 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 5,142,226,000 | 37,229,786,000 | 42,372,012,000 | 940,000,000 | 650,000,000 | 1,590,000,000 | 43,962,012,000 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 934,163,000 | 2,048,142,000 | 2,982,305,000 | | - | - | 2,982,305,000 |
| 13 | Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu | - | 2,915,586,000 | 2,915,586,000 | - | 470,000,000 | 470,000,000 | 3,385,586,000 |
| 21 | HAZINA | 945,178,117,000 | 1,181,695,401,000 | 2,126,873,518,000 | 1,257,970,257,000 | 29,784,942,000 | 1,287,755,199,000 | 3,414,628,717,000 |
| 22 | Huduma Nyinginezo | 9,452,132,000 | 2,214,379,800,000 | 2,223,831,932,000 | - | - | - | 2,223,831,932,000 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 6,361,101,000 | 39,551,734,000 | 45,912,835,000 | 1,880,000,000 | 964,792,000 | 2,844,792,000 | 48,757,627,000 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 48,267,019,000 | 40,657,910,000 | 88,924,929,000 | 22,118,347,000 | 4,640,863,000 | 26,759,210,000 | 115,684,139,000 |
| **JUMLA - MAFUNGU YOTE** | | **1,015,334,758,000** | **12,612,463,053,000** | **13,627,797,811,000** | **1,282,908,604,000** | **36,510,597,000** | **1,319,419,201,000** | **14,947,217,012,000** |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 14,757,479,000 | 59,838,739,000 | 74,596,218,000 | 7,828,000,000 | 3,098,935,000 | 10,926,935,000 | **85,523,153,000** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

## 5.0 HITIMISHO.

***110. Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), kwa ushauri na ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru watendaji wakuu wa Wizara na Taasisi zake wakiongozwa na Bw. Emmanuel M. Tutuba, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bw. Lawrence N. Mafuru na Bi. Jenifa C. Omolo kwa ushauri na usimamizi thabiti majukumu na kazi za kila siku za Wizara na Taasisi zake. Vilevile, nawashukuru wakuu wa Idara, vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa utekelezaji mzuri wa mikakati ya maendeleo, ushauri pamoja na ushirikiano wao mahiri katika kufanikisha majukumu yangu ya kila siku. Asanteni sana na Kazi Iendelee.

***111. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali inaendelea na maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Zoezi hili ni muhimu kwa nchi ili kupata taarifa za msingi zitakazosaidia katika uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo kwa Taifa letu. Hivyo, napenda kutoa wito

kwa waheshimiwa wabunge wenzangu kuwa tuendelea kuelimisha na kuhamasisha wapiga kura wetu na watanzania wote kwa ujumla kushiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi litakalofanyika Agosti 23, 2022.

***112. Mheshimiwa Spika***, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena pamoja na waheshimiwa wabunge kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii mbele yenu na umma wa watanzania kwa ujumla. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *www.mof.go.tz.*

***113. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**Kiambatisho Na.1: Fedha zilizotumika kwa Mishahara hadi Aprili 2022**

| Fungu | Jina la Fungu | | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 | Kiasi kilichotumika hadi aprili, 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | Mishahara ya Idara/Vitengo | 7,799,526,000.00 | 6,720,059,417.00 | 86 |
| | | Ruzuku ya Mishahara Taasisi | 33,103,343,000 | 28,939,670,022.00 | 87 |
| 21 | HAZINA | Mishahara ya idara na vitengo | 5,244,144,000.00 | 3,723,584,180.18 | 71 |
| | | Ruzuku ya Mishahara ya Taasisi | 204,701,306,000.00 | 155,473,998,294.73 | 76 |
| | | Marekebisho ya Mishahara ya Watumishi wa Umma | 209,982,200,000.00 | 130,297,631,258.00 | 62 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | | 3,859,834,000.00 | 3,444,170,944.04 | 89 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | | 716,795,000.00 | 632,324,023.70 | 88 |
| 22 | Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo | | 9,275,296,000.00 | 6,206,719,070.01 | 67 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | | 5,967,732,000.00 | 4,581,062,518.00 | 77 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | | 13,346,294,000.00 | 12,017,153,517.00 | 90 |
| **Jumla - Mishahara** | | | **493,996,470,000.00** | **352,036,373,244.66** | **71** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

## Kiambatisho Na. 2: Fedha zilizotumika kwa Matumizi Mengineyo hadi Aprili 2022

| Fungu | Jina la Fungu | | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 | Jumla ya kiasi kilichotumika hadi aprili 2021/2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 22 | Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo | | 10,664,243,143,000.00 | 8,020,037,321,971.81 | 75 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | Uendeshaji wa Ofisi | 10,229,786,000.00 | 7,256,306,040.72 | 71 |
| | | Matumizi Maalum | 47,000,000,000.00 | 35,293,961,681.16 | 75 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | | 2,048,142,000.00 | 1,627,720,622.88 | 79 |
| 13 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | | 2,915,586,000.00 | 2,029,599,454.60 | 70 |
| 21 | HAZINA | Idara/Vitengo | 89,413,455,000.00 | 39,669,560,810.80 | 44 |
| | | Ruzuku - Taasisi | 143,131,818,000.00 | 121,224,818,815.96 | 85 |
| | | Matumizi Maalum | 411,655,292,000.00 | 368,591,241,200.87 | 90 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | Idara/Vitengo | 30,421,168,000.00 | 20,081,840,915.90 | 66 |
| | | Ruzuku - Taasisi | 7,179,346,000 | 6,299,580,078.25 | 88 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | | 38,551,734,000.00 | 26,120,071,084.00 | 68 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | | 54,838,739,000.00 | 42,821,817,189.00 | 78 |
| **Jumla - Matumizi Mengineyo** | | | **11,501,628,209,000** | **8,691,053,839,865.95** | **76** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

## Kiambatisho Na.3: Fedha zilizotumika kwa Miradi ya Maendeleo hadi Aprili 2022

| | | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 | | Jumla ya kiasi kilichotumika hadi aprili 2022 | | Asilimia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fungu | Jina la Fungu | Ndani | Nje | Ndani | Nje | Ndani | Nje |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 1,000,000,000.00 | 1,300,000,000.00 | 621,706,000.00 | 429,170,000.00 | 62 | 33 |
| 13 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | - | 400,000,000.00 | - | 64,691,515.48 | 0 | 16 |
| 21 | HAZINA | 975,013,499,000.00 | 258,774,036,000.00 | 343,613,616,879.17 | 240,644,076,747.41 | 35 | 93 |
| 23 | Mhasibu Mkuu wa Serikali | 2,000,000,000 | 1,669,650,000.00 | 371,350,000 | 705,310,300.00 | 19 | 42 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 14,208,880,000.00 | 6,002,386,000.00 | 4,948,561,684.00 | 3,262,524,600.00 | 35 | 54 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 9,200,000,000.00 | 2,714,902,000.00 | 2,709,138,362.00 | 189,267,500.00 | 29 | 7.0 |
| **Jumla - Maendeleo** | | **1,001,422,379,000.00** | **270,860,974,000** | **352,264,372,925.17** | **245,295,040,662.89** | **35** | **91** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Tunaendelea na utaratibu wetu, nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na kwa niaba yake atasoma Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Omari Kigua. *(Makofi)*

**MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(1) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yaliyoko chini yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu nane yaliyoko chini ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanawasilishwa na Kamati hii kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 ambacho kinaipa mamlaka ya Kamati kuchambua, kushauri na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipitia na kuchambua taarifa za Wizara ya Fedha na Mipango zilizojumuisha mafungu nane pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kuwa ni sharti la Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na mafungu hayo ni kama ifuatavyo:-

i) Fungu 001 – Deni la Serikali;
ii) Fungu 007 – Ofisi ya Msajili wa Hazina;
iii) Fungu 010 – Tume ya Pamoja ya Fedha;
iv) Fungu 013 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu;

v) Fungu 021 – Hazina;
vi) Fungu 022 – Huduma za Mfuko Mkuu;
vii) Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali;
viii) Fungu 050 – Wizara ya Fedha na Mipango; na
ix) Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati imegawanyika katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo: -

Moja, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, mafungu yaliyo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; pili, makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023; na tatu, maoni na Mapendekezo ya ujumla ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; Wizara ya Fedha na Mipango ina mafungu nane pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Fungu 45. Jedwali namba moja linaonesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti za mafungu saba yaliyoko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mafungu saba; kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya mafungu yote saba ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Katika mwaka 2021/2022 mafungu saba ya Wizara ya Fedha na Mipango yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 12.95 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 11.93 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.03 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kati ya shilingi trilioni 11.93 za matumizi ya kawaida malipo ya deni la Serikali yalikuwa ni shilingi trilioni 8.834 na shilingi trilioni 3.096 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na mishahara kwa Idara,

Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mipango. Aidha, kiasi hicho kilijumuisha michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii na stahili za viongozi wakuu wa Serikali pamoja na shilingi bilioni 480.72 kwa ajili ya marekebisho ya mishahara ya watumishi wa umma, Majaji na viongozi wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo zilitengwa jumla ya shilingi trilioni 1.24 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 992.22 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 244.11 ni fedha za nje. Jedwali namba moja hapo chini linaonesha utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu saba ya Wizara ya Fedha na Mipango bila kuhusisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa utekelezaji wa bajeti na masuala yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 07 – Msajili wa Hazina; mwaka wa fedha 2021/2022 Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 63.39 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.86 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 10.23 kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi na shilingi bilioni 47 ni kwa ajili ya matumizi maalumu kama vile kulipa madeni ya mashirika ya umma na taasisi za umma na kurekebisha mashirika yenye matatizo ya mitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo zilitengwa shilingi bilioni 2.3, kati ya fedha hizo shilingi bilioni moja ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1.3 ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Aprili fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 65.33 sawa na asilimia 103.06 fedha hizo zimezidi kiwango cha bajeti kutokana na fedha za uhamisho kujumuishwa kwenye bajeti ya Fungu husika pamoja na malipo kwenda Benki ya *Exim China* kuhusu Kiwanda cha Nguo cha Urafiki. Utekelezaji wa matumizi ni kama unavyoonekana kwenye jedwali namba moja.

Kamati ina maoni yafuatayo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Fungu hili tukianza na matumizi maalum; matumizi maalum ni muhimu sana kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa sababu ndiyo hutumika kurekebisha mitaji kwa Mashirika ya Umma yenye changamoto ya mitaji pamoja na kulipa madeni ya Serikali iliyorithi kutoka iliyokuwa *Consolidated Holding Corporation (CHC)*. Hadi kufikia mwezi Aprili zilikuwa zimetolewa jumla ya shilingi bilioni 25.4 kati ya shilingi bilioni 47.0 zilizokuwa zimetengwa ni sawa na asilimia 54.14.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho kilichotengwa mbali na kwamba kilikuwa kidogo ukilinganisha na mahitaji imesababisha Serikali kuendelea kutolipa madeni kikamilifu inayodaiwa na wananchi katika maeneo mbalimbali na kuwezesha Taasisi zake kimtaji. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inawezesha Ofisi ya Msajili wa Hazina kifedha ili iweze kutoa mitaji kwa makampuni na taasisi za umma kama vile Benki ya Kilimo na Benki ya Uwekezaji ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inaamini kuiwezesha ofisi hii ni kuongeza mapato ya Serikali yasiyotokana na kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhaba wa watumishi; utofauti wa ofisi hii na ofisi nyingine za umma ni kwamba ofisi hii inasimamia uwekezaji wa mitaji ya Umma na inakusanya marejesho ya mitaji ya hiyo. Hivyo si sawa Ofisi hii kutokuwa na watumishi wa kutosha. Mathalani kati ya watumishi 185 wanaohitajika, watumishi waliopo ni 145 tu, hivyo kuna upungufu wa watumishi 40. Hali hii inaathiri utendaji kazi wa ofisi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba ofisi hii inapata watumishi wa kutosha ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Fungu 10 – Tume ya Taifa ya Fedha ya Pamoja; Tume ya Fedha ipo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Tume ilitengewa shilingi bilioni 2.84 ambapo, shilingi bilioni 2.12 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi milioni 716.7 ni kwa ajili ya mishahara. Hadi mwezi Aprili, 2022 Fungu hili lilikuwa limepokea jumla ya

shilingi bilioni 2.26 sawa na asilimia 81.84 ya bajeti yake ya mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 632.32 ni mishahara na shilingi bilioni 1.63 ni fedha za matumizi mengineyo. Kamati ina maoni na ushauri ufuatao katika fungu hili.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha imekwishafanya tafiti kwenye maeneo makuu mawili; moja ni kuhusu ukusanyaji wa mapato ya Muungano yanayotokana na huduma za mawasiliano ya simu, fedha za bima na kwa kampuni, mashirika yaliyosajiliwa upande mmoja wa Muungano na kufanya biashara katika pande zote mbili za Muungano na uanzishwaji wa akaunti jumuifu ya fedha. Kwa kuwa tafiti hizi zimekamilika Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi kikamilifu ili kuondoa kero za Muungano zinazojitokeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 013 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Fungu 13 liliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 3.88 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.48 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 400 ni fedha za nje kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilifanya uhamisho na kuongezea fedha fungu hili kiasi cha shilingi milioni 707.365 na kufanya bajeti ya Fungu hili kuwa na jumla ya shilingi bilioni 4.023.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2021 kitengo kilikuwa kimepokea shilingi bilioni 2.871 sawa na asilimia 71.38 ya Bajeti yote ya Fungu. Aidha, Fungu hili halikupokea fedha yoyote ya maendeleo kutoka nje licha ya kwamba zilitengwa kiasi cha shilingi milioni 400 fedha za nje. Vilevile Fungu hili limepokea kiasi cha shilingi milioni 143.14 fedha za ndani ambazo hazikuwa zimetengwa awali. Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo kuhusu utekelezaji wa bajeti ya fungu hili.

Kwanza, kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Fedha Haramu; ili kitengo hiki kifanye kazi yake kwa ufanisi; Kamati

inaishauri Serikali kitengo hiki kipewe hadhi ya kuwa Mamlaka Kamili kuliko ilivyo hivi sasa ambapo asilimia 90 ya watumishi wake ni wa kuazima kutoka mafungu na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Fungu 21 – Hazina; katika mwaka wa fedha 2021/2022, Fungu 21 liliidhinishiwa kiasi cha shilingi trilioni 2.06, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 1.06 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 999.35 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, matumizi ya kawaida ambayo ni shilingi trilioni 1.06 yamegawanywa katika matumizi yafuatayo shilingi bilioni 419.93 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Idara na Vitengo vya Hazina, shilingi bilioni 209.98 ilikuwa ni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma na shilingi bilioni 644.2 kwa ajili ya matumizi maalumu ya kitaifa na mahitaji ya dharura yanayojitokeza katika mafungu mbalimbali wakati wa utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo kati ya shilingi bilioni 999.345 zilizotengwa shilingi bilioni 975.01 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 24.33 ni fedha za nje. Aidha, Wizara ya Fedha ilifanya uhamisho wa kiasi cha shilingi bilioni 392.926 kwa ajili ya marekebisho ya mishahara na kupandishwa vyeo watumishi kutoka katika fungu hili na kufanya fungu hili kuwa na bajeti ya shilingi trilioni 1.904.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2022 Fungu 21 limepokea jumla ya shilingi bilioni 904.39 sawa na asilimia 47.47 ya makadirio ya shilingi trilioni 1.904. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 175.84 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 305.902 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo zilizopokelewa jumla ya shilingi bilioni 422.64, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 181.593 ndani na shilingi bilioni 241.051. Jedwali namba 1 limeonesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti. Pamoja na mwenendo huo uchambuzi wa Kamati imebaini masuala mbalimbali na Kamati inaushauri ufuatayo:-

(a) Changamoto za Watumishi katika Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara ya Fedha; Kamati imebaini Mamlaka ya Mapato Tanzania inahitaji jumla ya watumishi 8,374 watumishi waliopo ni 6,055 sawa na upungufu wa watumishi 2,319. Kamati inaishauri Serikali kuiangalia Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa jicho la kipekee kwa sababu hapa ndipo mapato yanapokusanywa na kutumika maeneo mengine. Aidha, Kamati inatambua juhudi ambazo Serikali imeendelea kuchukua za kuongeza watumishi sehemu ambazo inakusanya mapato, kama ilivyofanya Mamlaka ya Mapato kwa kuajiri watumishi takribani 2000.

(b) Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura *(Contigency Fund);* Mfuko wa Dharura umeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 140 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Aidha, ibara hiyo inatoa fursa kwa Bunge kutunga sheria ya uanzishwaji wa mfuko huo. Bunge lilitekeleza majukumu yake na likatunga Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na katika kifungu cha 35 hadi 38 kinaweka utaratibu wa vyanzo vya mapato vya mfuko na namna ya kuutumia. Hivi sasa Fedha za dharura zimekuwa zikitengwa kupitia Fungu 21 na hivyo matumizi yake hayafuati sheria ya Bajeti kwa sababu sio mfuko. Kamati inaitaka Serikali kuanzisha mara moja mfuko huo ili utusaidie tunapokuwa na dharura kama vile za ugonjwa wa UVIKO-19 na maafa pamoja na hili linalotukabili sasa la upandaji wa bei za mafuta.

(c) Kuimarisha Kitengo cha Ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuimarisha kitengo hiki kwa kukiongezea bajeti ili kiweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa pamoja na kuanzisha mfuko wa kusaidia kuandaa na kuendeleza miradi ya *PPP (PPP Facilitation Fund).*

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 22 - Deni la Serikali; Fungu 22 katika mwaka wa fedha 2021/2022 liliidhinishiwa kutumia kiasi shilingi trilioni 10.67 kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 9.275 ni kwa ajili ya mishahara ya maafisa wa umma wanaolipwa kupitia Fungu 22, shilingi trilioni 4.90 ni kwa ajili ya malipo ya deni la ndani, shilingi trilioni 3.931 kwa ajili ya

deni la Nje na shilingi trilioni 1.829 ni kwa ajili Huduma za Mfuko Mkuu. Aidha, Wizara ya Fedha ilifanya uhamisho wa kiasi cha shilingi bilioni 3.6 kutoka katika fungu hili na kwenda Fungu 23 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na kufanya fungu hili kuwa na bajeti ya shilingi trilioni 10.669.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili, 2022 jumla ya shilingi trilioni 8.76 zilitolewa ikiwa ni asilimia 82.03 ya bajeti. Mchanganuo wa matumizi ni kama ifuatavyo; shilingi bilioni 7.97 ni mishahara ya maafisa wa umma wanaolipiwa kupitia fungu hili; shilingi trilioni 8.75 ni kwa ajili ya malipo ya Deni la Serikali pamoja na michango ya mwajiri kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, Bima ya Afya, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na malipo ya pensheni kwa wastaafu wanaolipwa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaushauri ufuatao kuhusiana na malipo ya Deni la Serikali:-

(a) Maombi ya kuahirisha ulipaji wa deni *(Debt Suspension).* Hivi sasa Serikali yetu iko kwenye mazungumzo na nchi wanachama wa Paris *(Paris Club)* na wasio wanachama *(Non Paris)* pamoja na zile zilizotukopesha kwa njia ya *bilateral* ili kuangalia uwezekano wa kuahirisha ulipaji wa madeni. Jambo hili lina mitazamo miwili mtazamo wa kwanza ni hatua hii inatoa ahueni kwenye bajeti *(fiscal space)* ya kufanya miradi mingine kutokana na ahirisho hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini upande mwingine ambao ni lazima uangaliwe ni muda utakapofika wa kulipa lazima mapato yawe na uwezo wa kubeba madeni yaliyoiva wakati huo na yaliyoahirishwa. Hivyo basi, lazima Serikali ifanye tathmini ya kina na kuangalia endapo mapato yataweza kubeba mzigo huo kabla ya kuomba ahirisho. Vilevile Serikali itafute namna ambavyo itasaidia kuongeza mapato ya fedha za kigeni ili kufanya deni la Serikali kuendelea kuwa himilivu mfano kutumia vyanzo bunifu vya fedha kama vile *infrastructure bonds*, mfuko wa mazingira kupitia *carbon credit.*

Mheshimiwa Spika, Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 48.189 kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.67 ni fedha za Maendeleo na shilingi bilioni 44.519 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, fungu hili liliongezewa kiasi cha shilingi bilioni 3.6 kutoka Fungu 22 Deni la Serikali na kufanya fungu hili kuwa na jumla ya bajeti ya shilingi bilioni 51.789.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili, 2022 jumla ya shilingi bilioni 41.526 zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo sawa na asilimia 86.1 ya Bajeti ya Mwaka. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5.07 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 33.334 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3.122 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa utekelezaji wa bajeti kwa fungu hili ni kama unavyoonekana katika jedwali namba 1.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba fungu hili lina Ofisi za Mikoa yote Tanzania Bara lakini ndilo fungu ambalo lina Bajeti ndogo ukilinganisha na majukumu yake. Fungu hili lina majukumu makubwa yafuatayo:- usimamizi wa Sheria ya Fedha za Umma Sura 348; Kuandaa Miongozo ya Uhasibu *(Accounting Manual)*, Nyaraka za Uhasibu *(Accounting Circulars)* na Nyaraka za Hazina *(Treasury Circulars);* kutathmini utekelezaji wake katika uhasibu na mapato, matumizi na mali za Serikali na kuratibu maboresho ya Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 na kanuni zake; kushauri na kutoa ufafanuzi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa maana ya *PAC* na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusiana na masuala mbalimbali ya usimamizi wa Fedha za Umma pamoja na kulipa kiinua mgongo cha pensheni kwa wastaafu wanaolipwa kupitia Hazina.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza azma hiyo baada ya majadiliano baina ya Kamati na Serikali, ilibainika kwamba fungu hili lina mahitaji makubwa ya kufanya mafunzo kwa Halmashauri zote nchini kuhusiana na mifumo mbalimbali ya kiuhasibu. Hivyo, Kamati iliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango

kupunguza kiasi cha shilingi bilioni moja kutoka kwenye vifungu vya Fungu 21 ili ziende kuwezesha utolewaji wa mafunzo na utekelezaji wa majukumu ya fungu hili. Wizara ilikubali na fedha hizo zilihamishwa kutoka Fungu 21 kwenda Fungu 23.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mifumo mingi ya Serikali imekuwa ikijengwa na vijana wa Kitanzania, ni jambo la kupongeza, hata hivyo Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuwekeza kwenye mifumo na kuhakikisha mifumo hiyo inasomana.

Mheshimiwa Spika, Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango; katika mwaka wa fedha 2021/2022, Fungu 50 liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 98.714 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 78.503 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Idara na taasisi zilizo chini ya Fungu 50 na shilingi bilioni 20.211 ni kwa ajili ya mradi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilifanya uhamisho wa fedha na kuliongezea fungu hili kiasi cha shilingi bilioni 10.333 na kulifanya fungu hili kuwa na bajeti ya shilingi bilioni 109.048.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022 fedha zilizokuwa zimepokelewa ni shilingi bilioni 83.887 sawa asilimia 76.93 ya makadiro ya mwaka 2021/2022. Kati ya kiasi kilichopokelewa shilingi bilioni 35.59 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 37.924 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi bilioni 3.562 fedha za nje na shilingi bilioni 6.086 fedha za ndani za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya Fungu hili kwa kulinganisha na majukumu ya Fungu hili na ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuna haja ya kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ili kuleta tija kwenye Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Changamoto zinazosababishwa na sheria ilivyo hivi sasa ni kama ifuatavyo:-

(a) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinawasilisha taarifa yake kwenye Kamati ya Ukaguzi ambayo ina wajumbe watano, watatu kutoka Taasisi husika na wawili kutoka nje ambao wote wanateuliwa na Afisa Masuuli wa Fungu husika. Taratibu za kimataifa zinahitaji walau watatu kutoka nje ya Fungu au Taasisi husika;

Mheshimiwa Spika, na mbili Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kiko chini ya Afisa Masuuli na kinapata bajeti chini ya fungu husika hivyo inaondoa uhuru wa ukaguzi; na tatu kitengo kushindwa kufanya ukaguzi stahiki kutokana na kuwa mifumo hafifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba kwanza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ukaguzi ili wakaguzi wa ndani wawajibike kwa Mkaguzi Mkuu wa ndani na Wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi wabadilishwe watatu watoke nje na wawili watoke ndani. Na endapo itatokea kwamba Kamati haijakubalina na majibu ya Menejimenti, Mkaguzi wa Ndani aruhusiwe kuwasilisha taarifa yake kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani moja kwa moja kwa hatua zaidi. Aidha, inashauriwa kwamba Idara ya Mkaguzi Mkuu wa ndani iwe na fungu lake peke yake ili iwe na uhuru wa kukagua na kutoa maoni.

Pili, Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali; kuna changamoto kubwa katika uuzaji wa mali za Serikali ambazo ama zimechakaa au Serikali inahitaji kuziuza kwa sababu mbalimbali. Ofisi za umma maeneo mengi nchini zina mali za umma ambazo hazitumiki, lakini imekuwa vigumu ama kuziuza au kuziharibu. Matokeo yake ofisi za umma zimekuwa kama maeneo ya maegesho ya magari machakavu, samani na vifaa vya TEHAMA. Changamoto hii ni kubwa zaidi kwa balozi zetu ambapo haziwezi ama kuharibu au kuuza mali ambazo hazitumiki mpaka wataalam kutoka idara hii watakapothibitisha. Jambo la kushangaza ni pale ambapo wakati mwingine gharama inayotumika kuhakiki mali hizo chakavu ni kubwa kuliko thamani ya mali zinazohakikiwa. Hivyo kuna haja ya Serikali kupitia upya sheria na utaratibu

wake wa kuuza na kuharibu mali chakavu ili ufanyike kwa ufanisi na kwa gharama ndogo.

Tatu, Idara ya Usimamizi wa Mifumo ya Serikali; pamoja na kwamba Serikali inaendelea kuhuisha mifumo yake ili kuondoa changamoto za kupanga na kutumia fedha za umma, bado kwa kiasi kikubwa mifumo hii haijawa na ufanisi uliotarajiwa kutokana na kutofungamanishwa na mifumo mingine na kukosekana kwa mtandao wa uhakika. Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kufungamanisha mifumo hii hata hivyo suala hili limekuwa linatekelezwa polepole. Hivyo, ni vyema Serikali ikaongeza kasi katika kuhuisha mifumo yake ili isomane na ifanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022; jukumu la kujadili kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo inatekelezwa na Kamati ya Bajeti kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu hili.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa Fungu 45; Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilitengewa shilingi bilioni 80.09 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 13.35 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 54.84 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi bilioni 11.91 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Aprili Fungu hilo lilikuwa limepokea jumla ya Shilingi bilioni 61.03 sawa na asilimia 76.19 ya bajeti mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 2 hapo chini.

Mheshimiwa Spika, masuala ya msingi yaliyobainika katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Serikali; katika majadiliano masuala yafuatayo yalibainika ambayo Kamati iliyatolea maelekezo kwa Serikali; moja, Ofisi ya Mdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ina changamoto ya watumishi na hivyo kuathiri utendaji wake; mbili, ujenzi wa Ofisi za *CAG* mikoani ili kuwaondoa wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka kwenye majengo ya wakaguliwa unaendelea kwa kusua sua.

**SPIKA:** Dakika tatu malizia.

**MHE. OMARI M. KIGUA - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**: Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati; baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Fungu Jipya Namba 01 - Deni la Serikali; kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti naomba kuwasilisha pongezi za dhati kwa Serikali kwa kukubali kuazisha Fungu jipya litakalokuwa linahusika na ulipaji wa Deni la Serikali tu. Hatua hii itaondoa mkanganyiko uliokuwepo wa kujumuisha madeni ya Serikali na huduma za mfuko wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma; kama kuna haja ya njia nzuri na rahisi ya kujenga miundombinu ya mawasiliano, huduma, usafiri na usafirishaji ni kwa kutumia njia ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Pamoja na uwepo wa sheria tangu mwaka 2010 njia hii haijaweza kulinufaisha Taifa hili kwa zaidi ya miaka 12.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa kazi wa Kikosi Kazi cha Mabadiliko ya Kodi *(Task Force on Tax Reform);* kikosi kazi cha mabadiliko ya kodi kimeanzishwa kwa mujibu wa Kanuni ya

9 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti na majukumu yake yamebainishwa katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukuwa nafasi hii kwamba taarifa yote ya Kamati iingie katika *Hansard. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye hitimisho; naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge hili la Bajeti. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba - Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande - Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. *(Makofi)*

Vilevile nimshukuru Katibu Mkuu - Ndugu Emmanuel Tutuba, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao. Kamati inatambua mchango wa Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango katika kujadili kuchambua na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - Ndugu Charles Kichere kwa ushirikiano wake na ufafanuzi alioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho si kwa umuhimu naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba majina yote ya Wajumbe yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati katika kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inatambua na kuenzi mchango wa Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe kwa kuipatia ushauri wa kitaalam Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango yanayojumisha Mafungu nane yaliyo chini yake pamoja na Fungu 45 ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA MAFUNGU YALIYO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 118(1) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yaliyoko chini yake kwa mwaka wa fedha 2021/22 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu 8 yaliyoko chini ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23. Makadirio ya mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanawasilishwa na kamati hii kwa mujibu wa kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 ambacho kinaipa

mamlaka ya Kamati kuchambua, kushauri na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipitia na kuchambua taarifa za Wizara ya Fedha na Mipango zilizojumuisha mafungu 8 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kuwa ni sharti la Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na Mafungu hayo ni kama ifuatavyo:-

**i) Fungu 001** – Deni la Serikali
**ii) Fungu 007 –** Ofisi ya Msajili wa Hazina
**iii) Fungu 010 –** Tume ya Pamoja ya Fedha
**iv) Fungu 013 –** Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu
**v) Fungu 021 –** Hazina
**vi) Fungu 022 –** Huduma za Mfuko Mkuu
**vii) Fungu 023 –** Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali
**viii) Fungu 050 –** Wizara ya Fedha na Mipango
**ix) Fungu 045** – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati imegawanyika katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo: -

i. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, Mafungu yaliyo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/22;

ii. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23;

iii. Maoni na Mapendekezo ya Ujumla ya Kamati.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya fedha na Mipango ina Mafungu 8 pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi fungu 45. Jedwali Na 1

linaonyesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti za mafungu 7 yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango

**2.1. Uchambuzi wa mafungu 7**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya mafungu yote yaliyo 7 ya Wizara ya Fedha Mwaka wa Fedha 2021/22. Katika mwaka 2021/22, mafungu saba (7) ya Wizara ya Fedha na Mipango yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi trilioni 12.95** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi trilioni 11.93** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi trilioni 1.03** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, kati ya **Shilingi trilioni 11.93** za matumizi ya kawaida malipo ya Deni la Serikali yalikuwa ni **Shilingi trilioni 8.834** na shilingi **trilioni 3.096** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na mishahara kwa Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara na mipango. Aidha, kiasi hicho kilijumuisha michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii; na stahili za Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na **Shilingi bilioni 480.72** kwa ajili ya Marekebisho ya mishahara ya watumishi wa umma Majaji; na Viongozi Wakuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi ya maendeleo zilitengwa jumla ya **Shilingi trilioni 1.24 kati ya fedha hizo** Shilingi **bilioni 992.22 ni fedha za ndani** na Shilingi **bilioni 244.11** ni fedha za nje. Jedwali na 1 hapo chini linaonyesha utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu 7 ya Wizara ya Fedha na Mipango bila kuhusisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali

**Jedwali Na. 1 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango Mafungu 8 pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi fungu 45 kwa mwaka 2021/22**

| Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 | Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2022 | Asilimia ya Bajeti Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| **07. Msajili wa Hazina** | | | |
| Mshahara | 3,859,834,000.00 | 3,444,170,944.04 | 89.23 |
| Matumizi mengineyo | 57,229,786,002.00 | 60,453,820,683.91 | 105.63 |
| Maendeleo Ndani | 1,000,000,000.00 | 1,000,000,000.00 | 100 |
| Maendeleo Nje | 1,300,000,000.00 | 429,170,000.00 | 33.01 |
| **Jumla Ndogo** | **63,389,620,002.00** | **65,327,161,627.95** | **103.06** |
| **10 Tume ya Pamoja ya Fedha** | | | |
| Mshahara | 716,795,000.00 | 632,324,023.70 | 88.2 |
| Matumizi mengineyo | 2,119,104,828.00 | 1,630,581,391.34 | 79.6 |
| **Jumla Ndogo** | **2,835,899,828.00** | **2,262,905,415.04** | **81.84** |
| **013 Kitengo cha udhibiti fedha haramu** | | | |
| Matumizi mengineyo | 2,915,586,000 | 2,728,374,500.85 | **93.5** |
| Maendeleo Ndani | - | 143,137,292.93 | **-** |
| Maendeleo Nje | 400,000,000 | - | **-** |
| **Jumla Ndogo** | **3,315,586,000** | **2,871,511,793.78** | **86.6** |
| **021Hazina** | | | |
| Mshahara | 419,927,650,000.00 | 175,838,201,949.97 | 41.8 |
| Matumizi mengineyo | 644,200,565,000.00 | 305,901,979,090.80 | 47.4 |
| Maendeleo Ndani | 975,013,499,000.00 | 181,593,127,142.57 | 18.6 |
| Maendeleo Nje | 234,740,000,000.00 | 241,051,506,129.21 | 102.6 |
| **Jumla Ndogo** | **2,063,473,550,000.00** | **904,384,814,312.55** | **43.8** |
| **022 Huduma ya mfuko mkuu** | | | |
| Mshahara | 9,275,296,000.00 | 7,968,686,073.96 | 85.91 |
| Matumizi mengineyo | 10,664,243,143,000 | 8,752,805,801,479.54 | 82.08 |
| **Jumla Ndogo** | **10,673,518,439,000** | **8,760,774,487,553.50** | **82.08** |
| **23.Idara ya mhasibu mkuu** | | | |
| Mshahara | 5,967,732,000 | 5,070,382,975.07 | 84.9 |
| Matumizi mengineyo | 38,551,734,000 | 33,334,078,662.20 | 86.4 |
| Maendeleo Ndani | 2,000,000,000 | 2,000,000,000.00 | 100 |
| Maendeleo Nje | 1,669,650,000 | 1,122,200,000.00 | 67.2 |
| **Jumla ndogo** | **48,189,116,000** | **41,526,661,637.27** | **86.1** |
| **50.Wizara ya fedha na mipango** | | | |
| Mshahara | 40,902,869,000.00 | 35,595,272,724.40 | 87.02 |
| Matumizi mengineyo | 37,600,514,000.00 | 37,924,991,536.73 | 100.86 |
| Maendeleo Ndani | 14,208,880,000.00 | 6,805,977,391.73 | 47.89 |
| Maendeleo Nje | 6,002,386,000.00 | 3,561,145,000.00 | 59.33 |
| **Jumla Ndogo** | **98,714,649,000** | **83,887,386,652.86** | **84.98** |
| **Jumla Kuu** | **12,953,365,897,002.00** | **9,861,034,928,992.95** | **76.12** |

*Chanzo:Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa fedha 2021/22*

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa utekelezaji wa Bajeti na masuala yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

### 2.2.1. Fungu 07 – Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Msajili wa Hazina, iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi bilioni 63.39** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 3.86** zilitengwa kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 10.23** kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi na **Shilingi bilioni 47**. kwa ajili ya matumizi maalumu kama vile kulipa madeni ya Mashirika na Taasisi za Umma na kurekebisha Mashirika yenye matatizo ya mitaji. Kwa upande wa fedha za maendeleo zilitengwa **Shilingi Bilioni 2.3**, kati ya hizo **Shilingi bilioni 1.0** fedha za ndani na **Shilingi Bilioni 1.3** fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Aprili fungu hili lilipokea jumla ya **Shilingi bilioni 65.33** sawa na **asiilimia 103.06** fedha hizo zimezidi kiwango cha Bajeti kutokana na fedha za uhamisho kujumuishwa kwenye Bajeti ya Fungu husika pamoja na malipo kwenda Benki ya Exim China kuhusu kiwanda cha nguo cha Urafiki. Utekelezaji wa matumizi ni kama unavyoonekana kwenye jedwali Na 1. Kamati ina maoni yafuatayo kuhusu utekelezaji wa Bajeti wa Fungu hili:-

#### a) Matumizi Maalum

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi maalum ni muhimu sana kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa sababu ndiyo hutumika kurekebisha mitaji kwa mashirika ya umma yenye changamoto ya mitaji pamoja na kulipa madeni ya Serikali iliyoyarithi kutoka iliyokuwa CHC-Consolidated Holding Corporation. Hadi kufika mwezi Aprili zilikuwa zimetolewa jumla ya **Shilingi bilioni 25.4** kati ya shilingi **bilioni 47.0** zilizokuwa zimetengwa sawa na **asilimia 54.14**. Kiasi hicho kilichotengwa mbali na kwamba kilikuwa kidogo ukilinganisha na mahitaji imesababisha Serikali kuendelea kutolipa madeni kikamilifu inayodaiwa na Wananchi katika maeneo mbalimbali na kuwezesha Taasisi zake kimtaji. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inawezesha Ofisi msajili wa hazina kifedha ili iweze kutoa mitaji kwa Makampuni na Taasisi za umma kama vile Benki ya Kilimo na Benki ya Uwekezaji ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inaamini kuiwezesha ofisi hii ni kuongeza mapato ya Serikali yasiyotokana na kodi.

**b) Uhaba wa Watumishi**

**Mheshimiwa Spika,** Utofauti wa Ofisi hii na Ofisi nyingine za Umma ni kwamba Ofisi hii inasimamia uwekezaji wa mitaji ya Umma na inakusanya marejesho ya mitaji ya hiyo. Hivyo si sawa Ofisi hii kutokuwa na watumishi wa kutosha. Mathalani kati ya watumishi 185 wanaohitajika Ofisi watumishi waliopo ni 145 tu hivyo kuna upungufu wa watumishi 40. Hali hii inaathiri utendaji kazi wa Ofisi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Ofisi hii inapata watumishi wa kutosha ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

**2.2.2. Fungu 10: Tume ya Fedha ya Pamoja**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Fedha ipo kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Tume ilitengewa jumla ya **Shilingi bilioni 2.84** ambapo, **Shilingi bilioni 2.12** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na **Shilingi milioni 716.7** ni kwa ajili ya Mishahara. Hadi mwezi Aprili 2022 Fungu hili lilikuwa limepokea jumla ya **Shilingi bilioni 2.26** sawa na **asilimia 81.84** ya Bajeti yake ya Mwaka wa Fedha 2021/22. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 632.32** ni mishahara na **Shilingi bilioni 1.630** ni fedha za Matumizi Mengineyo. Kamati ina maoni na ushauri ufuatao katika fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya pamoja ya Fedha imekwisha fanya tafiti kwenye maeneo makuu mawili moja ni kuhusu Ukusanyaji wa Mapato ya Muungano yanayotokana na Huduma za Mawasiliano ya Simu, Fedha na Bima kwa kampuni/mashirika yaliyosajiliwa upande mmoja wa Muungano na kufanya Biashara katika Pande zote Mbili za Muungano na uanzishwaji wa Akaunti jumuifu ya fedha. Kwakuwa, tafiti hizi zimekamilika Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi kikamilifu ili kuondoa kero za Muungano zinazojitokeza katika maeneo hayo.

**2.2.3. Fungu 13: Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/22, Fungu 13 liliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 3.88** kwa ajili

ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 3.48** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi milioni 400** ni fedha za nje kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilifanya uhamisho na kuliongezea fungu hili kiasi cha **Shilingi milioni 707.365** na kufanya bajeti kwa fungu hili kuwa jumla ya **Shilingi bilioni 4.023**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi mwezi Aprili 2021 kitengo kilikuwa kimepokea Shilingi **Bilioni 2.871** sawa na **asilimia 71.38** ya Bajeti yote ya Fungu. Aidha, fungu hili halikupokea fedha yoyote ya maendeleo kutoka nje licha ya kwamba zilitengwa kiasi cha **Shilingi milioni 400** fedha za nje. Vilevile fungu hili limepokea kiasi cha **Shilingi milioni 143.14** fedha za ndani ambazo hazikuwa zimetengwa awali. Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya fungu hili.

**a) Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Fedha haramu**

**Mheshimiwa Spika,** ili kitengo hiki kifanye kazi yake kwa ufanisi Kamati inaishauri Serikali kitengo hiki kipewe hadhi ya kuwa Mamlaka Kamili kuliko ilivyo hivi sasa ambapo asilimia karibia 90 ya watumishi wake ni wa kuazima kutoka mafungu na Taasisi nyingine.

**b) Kuhakikisha kwamba Kitengo kinakuwa na rasilimali fedha na rasilimali watu toshelezi**

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Aprili, 2022 kitengo kilikuwa kimepokea Taarifa ya jumla ya miamala **Shuku 12,840** kati ya miamala hiyo **miamala 2,186** ilihusu usafirishaji wa fedha kutoka na kuingia nchini; **Miamala 5,251** ilihusu fedha taslimu, **Miamala ya 5,403** ilihusu kutuma fedha kwa njia ya kielektroniki. Jambo ambalo linasikitisha ni kwamba miamala ambayo uchunguzi umekamilika na kuwasilishwa taarifa zake fiche za fedha kwa vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria ni **101** tu sawa na **asilimia 0.78**. Madhara yake ni fedha za wananchi kuendelea kushikiliwa katika mabenki na Taasisi za fedha na hivyo kuleta taharuki. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kitengo hikii kinawezehswa kifedha na rasilimali watu ili kuondoa taharuki hiyo.

### 2.2.4. Fungu 21: Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/22, Fungu 21 liliidhinishiwa kiasi cha **shilingi trilioni 2.06**, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi trilioni 1.06** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 999.35** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, matumizi ya kawaida ambayo ni **Shilingi** trilioni **1.06** yamegawanywa katika matumizi yafuatayo **Shilingi bilioni 419.93** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Idara na Vitengo vya Hazina, **Shilingi bilioni 209.98** ilikuwa ni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma na **Shilingi bilioni 644.2** kwa ajili ya matumizi maalumu ya kitaifa na mahitaji ya dharura yanayojitokeza katika mafungu mbalimbali wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Kwa upande wa maendeleo Kati ya **Shilingi bilioni 999.345** zilizotengwa **Shilingi bilioni 975.01** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 24.33** ni fedha za nje. Aidha, Wizara ya Fedha ilifanya uhamisho wa kiasi cha **Shilingi bilioni 392.926** kwa ajili ya marekebisho ya mishahara na kupandishwa vyeo watumishi kutoka katika fungu hili na kufanya fungu hili kuwa na bajeti ya **Silingi trilioni 1.904.**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi Aprili 2022, Fungu 21 limepokea jumla ya **Shilingi bilioni 904.39** sawa na **asilimia 47.47** ya makadirio ya **Shilingi trilioni 1.904.** Kati ya kiasi hicho, **Shilingi bilioni 175.84** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi bilioni 305.902** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo zilipokelewa jumla ya **Shilingi bilioni 422.64**, kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 181.593** ndani na **Shilingi bilioni 241.051**. Jedwali namba 1 limeonyesha mwendo wa utekelezaji wa Bajeti. Pamoja na mwenendo huo uchambuzi wa kamati imebaini masuala mbalimbali na inaushauri ufuatayo:-

**a) Changamoto za Watumishi katika Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini Mamlaka ya Mapato Tanzania inahitaji jumla ya **watumishi 8,374** watumishi waliopo ni **6,055,** Sawa na upungufu wa **watumishi 2,319.** Kamati

inaishauri Serikali kuiangalia Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa jicho la kipekee kwa sababu hapa ndipo mapato yanapokusanywa na kutumika maeneo mengine. Aidha, Kamati inatambua juhudi ambazo Serikali imeendelea kuchukua za kuongeza watumishi sehemu ambazo inakusanya mapato, kama ilivyofanya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuajiri watumishi takriban 2000.

**b) Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura *"Contigency Fund"***

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Dharura umeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 140 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Aidha, ibara hiyo inatoa fursa kwa Bunge kutunga sheria ya uanzishwaji wa mfuko huo. Bunge lilitekeleza majukumu yake na likatunga Sheria ya Bajeti sura ya 439 na katika kifungu cha 35 hadi 38 kinaweka utaratibu wa vyanzo vya mapato vya mfuko na namna ya kuutumia. Hivi sasa Fedha za dharura zimekuwa zikitengwa kupitia fungu 21 na hivyo matumizi yake hayafuati sheria ya Bajeti kwa sababu si mfuko. Kamati inataka Serikali kuanzisha mara moja mfuko huo ili utusaidie tunapokuwa na dharura kama vile za ugonjwa wa UVIKO-19 na maafa pamoja na hili linalotukabili sasa la upandaji wa bei za mafuta.

**c) Kuimarisha kitengo cha ubia kati ya sekta ya umma na sekta Binafsi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuimarisha kitengo hiki kwa kukiongezea bajeti ili kiweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa pamoja na kuanzisha mfuko wa kusaidia kuandaa na kuendeleza miradi ya PPP "PPP Facilitation Fund".

**2.2.5. Fungu 22: Deni la Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 022 katika mwaka wa fedha 2021/ 22 liliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 10.67** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 9.275** ni kwa ajili ya mishahara ya maafisa wa umma wanaolipwa kupitia Fungu 022, **Shilingi trilioni 4.90** ni kwa ajili ya malipo ya deni la Ndani, **Shilingi**

**trilioni 3.931** kwa ajili ya deni la Nje na **Shilingi trilioni 1.829** ni kwa ajili Huduma za Mfuko Mkuu. Aidha, Wizara ya Fedha ilifanya uhamisho wa kiasi cha **Shilingi bilioni 3.6** kutoka katika fungu hili na kwenda fungu 23 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na kufanya fungu hili kuwa na bajeti ya **Shilingi trilioni 10.669.**

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Aprili, 2022 jumla ya **Shilingi trilioni 8.76** zilitolewa ikiwa ni **asilimia 82.03** ya bajeti. Mchanganuo wa matumizi ni kama ifuatavyo; **Shilingi bilioni 7.97** ni mishahara ya maafisa wa umma wanaolipiwa Fungu kupitia fungu hili, **Shilingi trilioni 8.75** ni kwa ajili ya malipo ya Deni la Serikali pamoja na michango ya mwajiri kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, bima ya afya, mfuko wa fidia kwa wafanyakazi na malipo ya pensheni kwa wastaafu wanaolipwa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaushauri ufuatao kuhusiana na malipo ya Deni la serikali:-

**a) Maombi ya Kuahirisha ulipaji wa Deni "Debt Suspension"**

**Mheshimiwa Spika,** Hivi sasa Serikali yetu iko kwenye mazungumzo na nchi wanachama wa Paris (Paris Club) na wasio wanachama (Non Paris) pamoja na zile zilizotukopesha kwa njia ya *Bilateral* ili kuangalia uwezekano wa kuahirisha ulipaji wa madeni. Jambo hili lina mitazamo miwili mtazamo wa kwanza ni hatua hii inatoa ahueni kwenye Bajeti *"Fiscal space"* ya kufanya miradi mingine kutokana na ahirisho hilo. Lakini upande mwingine ambao ni lazima uangaliwe muda utakapofika wa kulipa lazima mapato yawe na uwezo wa kubeba madeni yaliyoiva wakati huo na yaliyoahirishwa. Hivyo basi, lazima Serikali ifanye tathmini ya kina na kuangalia endapo mapato yataweza kubeba mzigo huo kabla ya kuomba ahirisho. Vilevile, Serikali itafute namna ambavyo itasaidia kuongeza mapato ya fedha za kigeni ili kufanya deni la Serikali kuendelea kuwa himilivu mfano kutumia vyanzo bunifu vya fedha kama vile infrastructure bonds, mfuko wa mazingira kupitia "carbon credit".

### 2.2.6. Fungu 23: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi bilioni 48.189** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 3.67** ni fedha za Maendeleo na **Shilingi bilioni 44.519** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, fungu hili liliongezewa kiasi cha Shilingi **bilioni 3.6** kutoka fungu 22 Deni la Serikali na kufanya fungu hili kuwa na jumla ya bajeti ya **Shilingi bilioni 51.789.** Hadi mwezi Aprili, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 41.526** zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo sawa na **asilimia 86.1** ya Bajeti ya Mwaka. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi bilioni 5.07** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 33.334** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 3.122** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa utekelezaji wa bajeti kwa fungu hili ni kama unavyoonekana katika jedwali na 1.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kwamba fungu hili lina ofisi Mikoa yote Tanzania bara lakini ndilo fungu ambalo lina Bajeti ndogo ukilinganisha na majukumu yake. Fungu hili lina majukumu makubwa yafuatayo:- usimamizi wa Sheria ya Fedha za umma SURA 348; Kuandaa Miongozo ya Uhasibu (Accounting Manual), Nyaraka za Uhasibu (Accounting Circulars) na Nyaraka za Hazina (Treasury Circulars), kutathmini utekelezaji wake katika kuhasibu mapato, matumizi na mali za Serikali na kuratibu maboresho ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 na Kanuni zake; Kushauri na kutoa ufafanuzi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusiana na masuala ya usimamizi wa Fedha za Umma pamoja na kulipa kiinua mgongo na pensheni kwa wastaafu wanaolipwa kupitia Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutimiza azma hiyo baada ya majadiliano baina ya Kamati na Serikali, ilibainika kwamba fungu hili lina mahitaji makubwa ya kufanya mafunzo kwa Halmashauri zote nchini kuhusiana Na Mifumo mbalimbali ya kiuhasibu. Hivyo, Kamati iliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kupunguza kiasi cha **Shilingi bilioni 1** kutoka kwenye vifungu

vya Fungu 21 ili ziende kuwezesha utolewaji wa mafunzo na utekelezaji wa majukumu ya fungu hili. Wizara ilikubali na fedha hizo zilihamishwa kutoka fungu 21 kwenda fungu 23.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa mifumo mingi ya Serikali imekuwa ikijengwa na vijana wa Kitanzania ni jambo la kupongeza, hata hivyo Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuwekeza kwenye mifumo na kuhakikisha mifumo hiyo inasomana.

### 2.2.7. Fungu 50: Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/22, fungu 50 liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 98.714** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 78.503** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Idara na taasisi zilizo chini ya Fungu 50 na **Shilingi bilioni 20.211** ni kwa ajili ya mradi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilifanya uhamisho wa fedha na kuliongezea fungu hili kiasi cha **Shilingi bilioni 10.333** na kulifanya fungu hili kuwa na bajeti ya **Shilingi bilioni 109.048.**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi mwezi Aprili 2022 fedha zilizokuwa zimepokelwa ni **Shilingi bilioni 83.887** sawa **asilimia 76.93** ya makadiro ya mwaka 2021/22. Kati ya kiasi kilichopokelewa **Shilingi bilioni 35.59** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 37.924** ni fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi bilioni 3.562** fedha za nje na **Shilingi bilioni 6.806** fedha za ndani za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya fungu hili kwa kulinganisha na majukumu ya Fungu hili na ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

**a) Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, kuna haja ya kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ili kuleta tija kwenye kitengo cha ukaguzi wa ndani. Changamoto zinazosababishwa na sheria ilivyo hivi sasa ni kama ifuatavyo:-

i. Kitengo cha ukaguzi wa ndani kinawasilisha Taarifa yake kwenye Kamati ya ukaguzi ambayo ina wajumbe 5, watatu kutoka Taasisi husika na wawili kutoka nje ambao wote wanateuliwa afisa masuuli wa fungu husika. Taratibu za kimataifa zinahitaji walau watatu watoke nje ya fungu au Taasisi husika;

ii. Kitengo cha ukaguzi wa ndani kiko chini ya Afisa masuuli na kinapata Bajeti chini ya fungu husika hivyo inaondoa uhuru wa ukaguzi;

iii. Kitengo kushindwa kufanya ukaguzi stahiki kutokana na kuwa mifumo hafifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kwamba kwanza kufanya marekebisho kwenye sheria ya ukaguzi ili wakaguzi wa ndani wawajibike kwa mkaguzi Mkuu wa ndani na Kamati ya ukaguzi wajumbe wabadilishwe watatu watoke nje na wawili watoke ndani. Na endapo itatokea kwamba kamati haijakubalina na majibu ya manejimenti mkaguzi wa ndani aruhusiwe kuwasilisha Taarifa yake kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani moja kwa moja kwa hatua zaidi. Aidha, inashauriwa kwamba Idara ya Mkaguzi Mkuu wa ndani iwe na fungu lake peke yake ili iwe na uhuru wa kukagua na kutoa maoni.

**b) Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Kuna changamoto kubwa katika uuzaji wa mali za Serikali ambazo ama zimechakaa au Serikali inahitaji kuziuza kwa sababu mbalimbali. Ofisi za Umma maeneo mengi nchini zina mali za umma ambazo hazitumiki lakini imekuwa vigumu ama kuziuza au kuziharibu. Matokeo yake Ofisi za Umma zimekuwa kama maeneo ya maegesho ya magari machakavu, samani na vifaa vya tehama. Changamoto hii ni kubwa zaidi kwa balozi zetu ambapo haziwezi ama kuharibu au kuuza mali ambazo hazitumiki mpaka wataalam kutoka idara hii watakapothibitisha. Jambo la kushangaza ni pale ambapo wakati mwingine gharama inayotumika kuhakiki mali hizo chakavu ni kubwa kuliko thamani ya mali zinazohakikiwa. Hivyo kuna haja ya

Serikali kupitia upya Sheria na utaratibu wake wa kuuza na kuharibu mali chakavu ili ufanyike kwa ufanisi na kwa gharama ndogo.

**c) Idara ya Usimamizi wa Mifumo ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kwamba Serikali inaendelea kuhuisha mifumo yake ili kuondoa changamoto za kupanga na kutumia fedha za umma. Bado kwa kiasi kikubwa mifumo hii haijawa na ufanisi uliotarajiwa kutokana na kutofungamanishwa na mifumo mingine na kukosekana kwa mtandao wa uhakika. Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kufungamanisha mifumo hii hata hivyo suala hili limekuwa linatekelezwa polepole. Hivyo, ni vyema Serikali ikaongeza kasi katika katika kuhuisha mifumo yake ili isomane na ifanye kazi kwa ufanisi.

**3.0. UCHAMBUZI WA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

**Mheshimiwa Spika,** Jukumu la kujadili kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo linatekelezwa na Kamati ya Bajeti kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele (c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Kaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili.

**3.1. Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Fungu 45**

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ilitengewa Jumla ya **Shilingi bilioni 80.09** kati ya Fedha hizo **Shilingi bilioni 13.35** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi bilioni 54.84** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi bilioni 11.91** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.** Hadi mwezi Aprili Fungu hilo lilikuwa limepokea

jumla ya **Shilingi bilioni 61.03** sawa na **asilimia 76.19** ya Bajeti mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyoonekana kwenye jedwali Na 2 Hapo chini.

**Jedwali Na 2. Mchanganuo wa Fedha za Matumizi zilizotolewa hadi Aprili 2022**

| Aina ya Matumizi | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 | Fedha iliyotolewa hadi Aprili 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 13,346,294,000 | 12,017,153,517 | 90.04 |
| Matumizi Mengineyo | 54,838,739,000 | 45,847,492,216 | 83.60 |
| Maendeleo Ndani | 9,200,000,000 | 2,854,735,166 | 31.03 |
| Maendeleo Nje | 2,714,902,000 | 309,745,000 | 11.4 |
| JUMLA | 80,099,935,000 | 61,029,125,899 | **76.19** |

*Chanzo: Randama Fungu 45*

**3.2. Masuala ya Msingi yaliyobainika katika Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Katika majadiliano masuala yafuatyo yalibainika ambayo kamati iliyatolea maelekezo kwa Serikali:-
i. Ofisi ya mdibiti na mkaguzi mkuu wa Serikali ina changamoto ya watumishi na hivyo kuathiri utendaji kazi wake;

ii. Ujenzi wa Ofisi za CAG mikoani ili kuwaondoa wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka kwenye majengo ya wakaguliwa unaendelea kwa kusua sua kutokana na utengaji na utolewaji hafifu wa fedha;

iii. Bado Ofisi ya CAG haina uhuru wa kuajili wataalamu wenye ujuzi na utaalamu unaotakiwa katika Ofisi hiyo na badala yake ajira bado zinaamuliwa na Tume ya Ajira;

iv. Majukumu ya ukaguzi yanaongezeka kwa kasi kuliko ongezeko la rasilimali fedha; na

v. Upungufu Mkubwa wa magari kwa ajili ya kaguzi mbalimbali kama vile za Ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na changamoto hizo kamati ilishauri Serikali kwanza kuhakikisha inatoa fedha zote za maendeleo zilizosalia kwa fungu hili; Inahakikisha walau kila mwaka Ofisi inaajili watumishi wapya ili kuondoa changamoto ya watumishi na Serikali iwe na jukumu la kutoa kibali tu lakini nani anaajiliwa na kwa taaluma zipi jukumu hili liachiwe Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yenyewe.

## 4.0. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

### 4.1. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu Saba ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2022/ 23

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi trilioni 14.94** kwa mafungu yote nane (8). Kati ya kiasi hicho, **Shilingi trilioni 13.17** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **Shilingi trilioni 1.77** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Jedwali Na. 4: Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mipango Mafungu yaliyochini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2022/23

### 4.2. Maombi ya Fedha ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi trilioni 15,011,348,698,828** kwa mafungu yote nane (8) pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni trilioni 12,300,089,361,000, Shilingi bilioni 940,092,236.828** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 1,782,094,036** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Jedwali Na. 4: Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mipango Mafungu yaliyochini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2022/23 "000"**

| FUNGU | MATUMIZI MENGINEYO | MISHAHARA | MIRADI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | 9,093,984,694 | - | - | 9,093,984,694 |
| 07 | 37,229,786 | 5,142,226 | 1,590,000 | 43,962,012 |
| 10 | 2,048,142 | 934,162.828 | - | 2,982,304,828 |
| 13 | 2,915,586 | - | 470,000 | 3,385,586 |
| 21 | 809,482,970 | 855,178,117 | 1,741,003,099 | 3,405,664,186 |
| 22 | 2,214,380 | 9,452,132 | - | 2,223,831,932 |
| 23 | 39,551,734 | 6,361,101 | 2,844,792 | 48,757,627 |
| 50 | 40,658 | 48,267,019 | 25,259,210 | 114,184,139 |
| **JUMLA** | **12,240,250,622** | **925,334,757,828** | **1,771,167,101** | **14,936,752,481** |
| 45 | 59,838,739 | 14,757,479 | 10,926,935 | 74,596,218 |
| **JUMLA KUU** | **12,300,089,361** | **940,092,236.828** | **1,782,094,036** | **15,011,348,698,828** |

*Chanzo: Randama za Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya CAG.*

## 5.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI FUNGU 45 KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza vipaumbele vyake imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 86,423,153,000** katika mwaka wa fedha 2022/23. Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi milioni 900** fedha za Maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi bilioni 85,523,153,000** fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinazoombwa ni **Shilingi bilioni 74,596,218,000** ambazo zinajumuisha **Shilingi 14,757,479,000** fedha za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi bilioni 59,838,739,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi kinachoombwa ni **shilingi 10,926,935,000** kati ya fedha hizo Shilingi **bilioni 7,828,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,098,935,000** fedha za nje.

**Jedwali Na. 3: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Fungu 45 kwa mwaka 2022/23**

| Maelezo | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 (A) | Mkadirio Mwaka 2022/23 (B) | Tofauti (B-A) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | | | | |
| Mshahara | 13,346,294,000 | 14,757,479,000 | 1,411,185,000 | 10.57 |
| Matumizi Mengineyo | 54,838,739,000 | 59,838,739,000 | 5,000,000,000 | 9.12 |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **68,185,033,000** | **74,596,218,000** | **6,411,185,000** | **9.40** |
| | | | | **1. MATUMIZI YA MAENDELEO** |
| 2.1 Fedha za ndani | 9,200,000,000 | 7,828,000,000 | (1,372,000,000) | -14.91 |
| 2.2 Fedha za nje | 2,714,902,000 | 3,098,935,000 | 384,033,000 | 14.15 |
| **Jumla Matumizi ya Maendeleo** | **11,914,902,000** | **10,926,935,000** | (987,967,000) | **-8.29** |
| **JUMLA FUNGU 45** | **80,099,935,000** | **86,423,153,000** | **6,323,218,000** | **7.89** |

*Chanzo: Randama ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi*

### 5.1. Maamuzi baada ya Mashauriano kuhusu Bajeti ya Fungu 45

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ilikamilisha majadiliano na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango na kubaini masuala yafuatayo: -

i. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliomba nyongeza ya Bajeti ya **Shilingi bilioni 10.8** ili kukidhi mahitaji ya kaguzi. Kutokana na ukomo wa Bajeti Serikali ilikubali kuongeze fungu hilo **Shilingi bilioni 5** tu.

**ii. Shilingi bilioni 5.8** ambazo hazikuongezwa kulingana na maombi zilihusu ujengaji wa mifumo ya ukaguzi na ununuzi wa magari kwa ajili ya ukaguzi wa ufanisi;

iii. Utolewaji wa Fedha za matumizi mengineyo kwa mwaka wa Fedha 2020/21 haukufikia **asilima 100** na badala yake ilikuwa ni **asilimia 80.4** tu. Hivyo ni wazi kwamba ukaguzi haukufanyika kikamilifu.

iv. Fedha za maendeleo zilizotolewa kwa mwaka wa Fedha 2021/22 hadi mwezi Aprili ni **asilimia 66.6** ya Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kubaini masuala hayo Kamati ilielekeza fungu hilo liongezewe jumla ya **Shilingi bilioni 3.9** kwa ajili ya matumizi yafuatayo:-

i. Kiasi cha **Shilingi bilioni 2.5** ili zikajenge na kuimarisha mifumo ya ukaguzi na usimamizi; na

**ii. Shilingi bilioni 1.4** ili zikanunue magari kwa ajili ya shughuli za ukaguzi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza ni vyema fedha hizo ziongezwe kwa Fungu hili hasa ukizingatia umuhimu wa ukaguzi na kuongezeka kwa mawanda ya ukaguzi. Hoja hii itakuwa ni moja ya hoja ambazo kamati ya Bajeti itashauriana na Serikali wakati wa majadiliano kwa mujibu wa kanuni ya 124(1) ili kuhakikisha jambo hili linapatiwa muafaka.

## 6.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2022/23. Kamati inapenda kutoa maoni na Mapendekezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

### 6.1. Kuanzishwa kwa Fungu Jipya Namba 001 Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti naomba kuwasilisha pongezi za dhati kwa Serikali kwa kukubali kuazisha Fungu jipya litakalokuwa linahusika na ulipaji wa Deni la Serikali tu. Hatua hii itaondoa mkanganyiko uliokuwepo wa kujumlisha madeni ya Serikali na huduma za mfuko wa Serikali.

### 6.2. Utekelezaji wa Miradi kwa njia ya Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kama kuna njia nzuri na rahisi ya kujenga miundombinu ya mawasiliano, huduma, usafiri na usafirishaji

ni kwa kutumia njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Pamoja na uwepo wa Sheria tangu mwaka 2010 njia hii haijaweza kulinufaisha Taifa hili kwa zaidi ya miaka 12 hadi hivi sasa. Mara kadhaa kamati imekuwa ikishauri Serikali kwanza kwa kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Ubia ili kupunguza kiwango cha mtaji kutoka dola za marekani **milioni 20** hadi walau kati ya dola za marekani **milioni 2** hadi **milioni 5** kwa Watanzania na kwa wageni kati ya dola **milioni 5** hadi **milioni 10.** Hatua hii si tu itavutia wawekezaji kutoka nje bali watanzania wataweza kushiriki kwenye ujenzi na utoaji wa huduma kwa mfumo wa Ubia.

**6.3. Utendaji wa Kazi wa Kikosi kazi cha Mabadiliko ya Kodi *"Task Force on Tax Reform"***

**Mheshimiwa Spika,** Kikosi kazi cha Mabadiliko ya Kodi kimeanzishwa kwa mujibu wa kanuni ya 9 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti na majukumu yake yamebainishwa katika kanuni ya 10. Kazi kubwa ya kikosi kazi hicho ni kupokea maoni na mapendekezo yanayohusu mabadiliko ama ya sheria za kodi au utaratibu wa kukusanya kodi. Changamoto kubwa ya Kikosi kazi hicho ni kutokutoa mrejesho kwa wadau mbalimbali wanaofika mbele yake ili kuwajulisha ni kwanini mapendekezo yao hayajakubaliwa. Hali hii husababisha masuala yanayowasilishwa katika kikosi kazi kujirudia kila mwaka na hayafanyiwi kazi. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kutoa mrejesho kwa wadau waliofika mbele yake ili hoja zinazowasilishwa zisijirudie mara kwa mara bila majibu. Aidha, kamati inapendekeza kuangalia muundo wa wajumbe wa kikosi kazi hicho na itolewe fursa ya kualika wataalamu wengine pale inapobidi.

**6.4. Kutofautisha majukumu ya Idara za Serikali kati ya ukusanyaji wa mapato na utoaji wa Huduma**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti inatambua umuhimu wa maduhuli katika mapato ya Serikali. Hata hivyo, maduhuli kwa baadhi ya maeneo yanaondoa hamasa ya kutoa huduma na badala yake Wizara, Idara, au Mamlaka za Serikali hasa zile ambazo hazifanyi Biashara zinaanzisha au kutoza viwango

vikubwa vya ada na tozo ili kukusanya maduhuli na kusahau kwamba jukumu lao la kwanza ni kutoa huduma. Mfano, Taasisi yoyote inapotaka kupata Taarifa za mtu kwa matumizi ya rasmi kutoka NIDA zinatozwa shilingi 500 kwa kila taarifa anayoitaka muhusika. Hivyo ni wazi kwamba kazi inayofanywa na NIDA ya kusajili watanzania wote ili watambulike imegeuka kuwa biashara na si huduma tena.

**6.5. Utekelezaji wa Blue Print kwa masuala ya kikodi**

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya changamoto kubwa iliyobainishwa na wafanyabiashara katika Mpango wa Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (Blueprint) ni wingi wa mamlaka za Udhibiti na Usimamizi *"Multiplicity of Regulatory Authoritie"* pamoja Mfumo wa Ulipaji wa Kodi, ada na tozo. Kamati imekuwa ikishauri ni kwanini Serikali isiangalie uwezekano wa kuanzisha Mamlaka moja ya udhibiti katika mamlaka hiyo kuwe na Idara mbalimbali kama vile za Usalama mahala pa kazi, viwango na ubora, uzito na nyinginezo. Aidha, kama ni lazima ziwepo basi mfumo wa malipo ya ada na tozo zao uhuishwe. Mfano badala ya mfanyabiashara mmoja kulipa TBS, OSHA, Wakala wa Vipimo kupitia hati za madai tofauti tofauti aweze kufanya hivyo kupitia dirisha moja. Kwakuwa hizi zote ni Taasisi za Serikali basi mgao ufanyike Serikalini. Hatua hii haiathiri mapato ya Serikali lakini inaleta ufanisi katika ukusanyaji wa fedha za Serikali.

**6.6. Kuangalia uwezekano wa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Manunuzi ya Umma**

**Mheshimiwa Spika,** kuna haja ya kuangalia uwezekano wa kupitia upya sheria ya manunuzi ya umma ili iendane na wakati ili kutanzua changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wake, baadhi ya changamoto ni:-

i. Matumizi ya sheria hiyo kwa mashirika na Taasisi za Umma ambazo zinajiendesha kibiashara imekuwa na changamoto kubwa. Mfano Shirika kama TTCL haliwezi kununua minara

ambayo imetumika lakini bado iko kwenye hali nzuri kwa sababu sheria inahitaji wanunue minara mipya wakati huo huo shirika halina fedha za kutosha kununua minara mipya;

ii. Inachelewesha mchakato wa manunuzi katika mashirika ya umma yanayojindesha kibiashara ambayo maamuzi ya haraka yanatakiwa kufanyika ili biashara iendelee;

iii. Kipengele cha "*lowest evaluated bidder*" au mzabuni aliomba kwa bei ya chini kuliko wote kimekuwa kinatoa mwanya kwa wakandarasi kuungana na kuamua bei ya chini iwe ipi; na

iv. Sheria hii haitoi tofauti ya ununuzi wa vifaa muhimu kama vile dawa na vifaa tiba na ununuzi wa mabati au matofali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kubadilisha sheria hiyo ili iendane na mahitaji ya sasa.

**7.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge hili la Bajeti. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua utekelezaji wa Bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/22. Vilevile nimshukuru Katibu Mkuu Ndugu Emmanuel Tutuba, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao. Kamati inatambua mchango wa Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango katika kujadili kuchambua na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa napenda kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndg. Charles Kichere kwa ushirikiano wake na ufafanuzi

alioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yake kwa mwaka 2021/22 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho si kwa umuhimu naomba kuwapongeza wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Ali Hassan King, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 15. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 16. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb | Mjumbe |
| 17. Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb | Mjumbe |
| 19. Mhe. Halima James Mdee, Mb | Mjumbe |
| 20. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 21. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb | Mjumbe |
| 23. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati katika kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inatambua na kuenzi mchango wa Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti

ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe kwa kuipatia ushauri wa kitaalam Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango yanayojumisha Mafungu nane (8) yaliyochini yake pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo,
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
7 Juni, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge tutaanza uchangiaji. Tunakushukuru sana Makamu Mwenyekiti kwa kuwasilisha maoni ya Waheshimiwa Wabunge Wanakamati ya Bajeti.

Majina niliyonayo hapa tutaanza na Mheshimiwa Jonas William Mbunda, atafatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii niishukuru Serikali kwa jinsi ilivyosimamia na kutekeleza bajeti nzima ya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitachangia katika maeneo machache, lakini mchango wangu sehemu kubwa nitatoa ushauri upande wa Serikali. Nikianza na upande wa *TRA*,

nilikuwa napenda kutoa ushauri *TRA* waweze kufungua Ofisi za Forodha katika mipaka yetu mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tunadhibiti na kusimamia mapato ya Serikali. Pamoja na hilo katika mipaka hiyo hiyo nilikuwa nashauri *TRA* kufunga *scanner* katika maeneo ya mipaka kwa ajili ya kuimarisha na kusimamia uhakiki wa mizigo inayoingia na kutoka nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa pili nataka nichangie kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina; Msajili wa Hazina ni msimamizi mkuu wa mali nyingi za Serikali pamoja na mashirika mbalimbali ambayo yako chini ya Serikali. Kwa upande wa Ofisi ya Msajili wa Hazina nilikuwa nataka nishauri kwenye yale mashirika yaliyofilisiwa viwanda pamoja na taasisi mbalimbali, maeneo mengi utakuwa mashirika hayo na viwanda hivyo vimekuwa *grounded* yaani havifanyi kazi na mali ziko katika maeneo hayo lakini ziko katika hali mbaya.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri sasa ni wakati muafaka katika kuimarisha uchumi wetu tuhakikishe kwamba mashirika hayo yanasimamiwa na yanaanza kufanya kazi, nikitoa mfano wa mashamba ya maua Arusha na viwanda mbalimbali ambavyo viko chini ya Msajili wa Hazina, nilikuwa nashauri viwe *activated* na vifanye kazi ili viweze kutuingizia mapato mbalimbali katika kuchangia kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika upande huu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina yeye ndiyo msimamizi mkuu wa madeni yote yale ambayo yalikuwa kwenye maeneo yaliyofilisiwa. Nataka nitoa mfano, mwaka 1997 kuna Vyama vingi vya Ushirika vilifilisiwa, lakini vyama hivyo vilikuwa vimekopa kwenye benki ya *NBC* na vyama hivi vilibaki vilikuwa na madeni makubwa na madeni hayo baadaye yalikwenda kwenye shirika moja la *Consolidated Holding Cooperation*. Sasa madeni hayo sasa hivi yanasimamiwa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, natolea mfano kuna chama kimoja kule Mbinga kilikuwa kinaitwa *Mbifaco Limited* lakini baadaye kuna chama kingine kimeanzishwa ambacho

kinaendeleza shughuli zile ambazo zilikuwa zinafanywa na *Mbifaco Limited* kinaitwa *Mbinga Farmers' Cooperative Union*. Kwa hiyo madeni yale bado yanashikiliwa na Serikali kupitia Msajili wa Hazina, lakini wakati huo vyama hivi inabidi viendelee na mali zile ambazo hati zake ziko upande wa Serikali ni mali za wakulima. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kupitia Msajili wa Hazina na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba madeni hayo yanasamehewa ili hati zile miliki zirudishwe kwa wananchi na wakulima waweze kuendeleza hivyo Vyama vyao vya Ushirika na kuendelea kufanya masuala ya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie tena kwenye upande wa hii Taasisi yetu ya Manunuzi hii *PPRA*. Ukiangalia katika bajeti za Serikali zaidi ya asilimia 70 fedha nyingi zinakwenda kwenye manunuzi, lakini sheria zilizopo katika hii taasisi ya *PPRA* zinachangia sana kutengeneza urasimu na matatizo mengi kwenye manunuzi ya mali na bidhaa mbalimbali kwa upande wa Serikali. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Wizara kwa kushirikiana na hiki chombo cha *PPRA* kuhakikisha kwamba tunafanya marekebisho ya sheria zetu ili kurahisisha kwenye suala la manunuzi na kuondoa urasimu ambao upo katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa Wizara nataka tena nichangie kwenye suala la mali chakavu. Maeneo mengi yana mali chakavu ambazo zilitakiwa ziwe *disposed,* ziwe zimeuzwa ili Serikali iweze kupata fedha kutokana na mali hizo nyingi. Lakini utaratibu unaotumika kwenye hizi *procedure* za *disposal* zinatuletea shida sana, unakuta kwa mfano mali za Serikali ziko kwenye Ubalozi nchi za nje. Lakini utaratibu ni kwamba huwezi kuuza hizo mali mpaka ufanye uthaminishaji. Sasa unaweza ukakuta afisa anatumwa kwenda nje kufanya uthaminishaji lakini gharama zile anazotumia kwenda nje ni kubwa zaidi kuliko mali ile ambayo itauzwa hapo baadaye.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iangalie uwezekano wa kufanya marekebisho kwenye sheria zetu ili kurahisisha uuzaji wa hizi mali mbalimbali ambazo ni chakavu.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ukienda pale Dar es Salaam utakuta kuna mabehewa mengi ya *TRC* yako mengi na ni chakavu na ni ya muda mrefu, lakini ukiuliza kwa nini hayauzwi utaambiwa kwamba mchakato bado unaendelea kwenye upande wa Serikali. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweka sawa na kuuza hizi mali ili zibaki ziendelee kuwa chakavu Serikali iweze kupata fedha na ziweze kutusaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho naomba nichangie kwenye upande wa ulipaji wa madeni; kwanza nipongeze Serikali ya Awamu ya Sita inayoongezwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusimamia na kuanza kulipa madeni mbalimbali ya Wakandarasi pamoja na wafanyabiashara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwenye upande wa eneo hili nataka niishauri Serikali na niiombe iendelee kusimamia kufanya uhakiki wa madeni hayo na kulipa Wakandarasi pamoja na wafanyabiashara hususan wale wafanyabiashara wa pembejeo ambao walisaidia sana kwa wakulima wetu. Lakini ni kwa muda mrefu sasa madeni yao bado hayajalipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, atafuatiwa na Daniel Baran Sillo, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hotuba hii ya Wizara ya Fedha. Mimi nitakuwa na michango miwili tu kama muda utaniruhusu nitazungumzia ufanisi uliopo katika Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa maana ya *TRA* na baadaye nitagusia haja ya kupanua wigo wa kodi na vilevile kuitaka Serikali au kuiomba Serikali iangalie tena nafasi yake

katika utekelezaji wa *blue print* kwa madhumuni ya kuweza kuchagiza ufanyaji wa biashara katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu ambaye anabisha kwamba Serikali inahitaji kukusanya mapato, hakuna mtu anayebisha katika hilo; na ili tuweze kufanikisha maisha bora ya Watanzania lazima Serikali iweze kufanikiwa na ndiyo kazi yetu sisi kuweza kuishauri Serikali iweze ikafanya vizuri na hata ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri *numbers* ambazo amezionesha kutokana na *performance* ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika kipindi hadi kufikia Aprili inaonesha kwamba wamefanya vizuri. Kwa sababu ni *average* ya asilimia 90 na kwenda juu, hivyo kama ni Chuo Kikuu Mheshimiwa Mwigulu umefanya *performance* ya "A" ama *A plus* na hapa lazima nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa sababu Mheshimiwa Rais ndiyo *captain* wa timu hii ya kina Mwigulu.

Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri kwa sababu naamini hata uwekaji watu sahihi katika maeneo sahihi ya Wizara ya Fedha na *TRA* yameweza kutuletea mafanikio haya ambayo tunayazungumza leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilikuwa naangalia andiko la *ActionAid* ambalo andiko hili limetolewa mwaka 2021 wenyewe wameliita *Sealing the Gaps*. Walikuwa wanaangalia mfumo wetu wa kikodi na kimapato, wakaona kwamba kuna matundu ambayo yanasababisha nchi yetu tusiweze tukafikia ukusanyaji bora wa mapato na wenyewe wanakisia kwamba kuna shilingi trilioni 17.4 yawezekana zinaeleaelea na Serikali hazikusanyi ni fedha nyingi sana. Na wenyewe wanasema kuna changamoto za usimamiaji wa masuala ya kodi, wanasema kuna kodi ambazo hazilipwi na hazikusanywi, watu wachache kwa maana ya wigo ni mdogo mno wa watu ambao wanaotozwa kodi na kwa hali hii wanashabikia utanuzi wa wigo wa ulipaji wa kodi, haya ni maneno mazuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ukiaangalia sisi tunayafahamu naamini hata Serikali inafahamu na kwa kuwa Serikali

inafahamu, ni dhahiri kinachofanyika sasa kwa *performance* hii naweza nikasema tayari tumeanza kuona njia sahihi ya kuweza kwenda.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiiangalia *TRA* hii hakika inafanya kazi nzuri ingawa ina *challenges* kubwa sana, ina changamoto nyingi, kwa mfano miaka mingi *TRA* imekuwa ikipiga kelele kuhusu kuongezewa idadi ya wafanyakazi. Na ni mpaka juzi walikuwa na watu 4,000 na ushee. Nashukuru Serikali kwamba wamewaongezea ajira ya watu 2,000 kama tulivyosikia katika hotuba hapa, lakini hitaji lao sasa hivi ni watu 8,000 na ushee maana yake kwamba bado kuna *deficit,* kuna upungufu wa watu 2,000.

Sasa kutokana na upungufu huo na ukiongezea ukweli kwamba mifumo ambayo ingeweza ku-*support* masuala mazima ya *administration* ya kodi hakika *TRA* wangeweza kufanya vizuri zaidi. Nataka niwape mfano mmoja mdogo tu, katika Bunge lako hili niliwahi kusimama na kuzungumza kuhusu kuongeza au kuweka Maafisa Kodi kwenye kila kata na nikatoa mfano, kama tuna Maafisa Ugani, kama kuna Maafisa wa Ustawi wa Jamii kwa nini tusiwe na Maafisa Kodi kwenye kila Kata. Nashukuru na naipongeza *TRA* walisikia ushauri ule na hata kwenye Kamati yetu tukatoa tena ushauri ule. Walichofanya ni nini, walikusanya vijana 250 kule Dar es Salaam wakawapeleka katika maeneo ya Kinondoni, Ilala, Tegeta na Temeke ili kwenda kuangalia ufanyaji wa biashara na kuweza kuangalia kama kila anayefanya biashara anatambuliwa na amesajiliwa kwa maana ya mlipa kodi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi mmoja ama miezi miwili waligundua wafanyabiashara 27,463 hawakuwemo katika mfumo wa kodi. Sasa hiyo maana yake ni kwamba katika kipindi kirefu kuna watu ambao wanafanya biashara, lakini hawalipi kodi stahiki. Hivyo mimi niwapongeze *TRA* na niipongeze Serikali kwamba kumbe mnaweza mkatusikiliza Wabunge na mkayachukua yale ambayo tunawashauri na mkafanyia kazi, hongereni sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisemee kuhusu mifumo, yawezekana tukawa na watu mahiri, *skilled* katika maeneo mengi *TRA*, lakini bila ya kuwa na mifumo imara hawawezi wakafanikiwa. Hebu angalia kwa mwezi Machi ambapo mfumo wa *e-filing* wa *VAT Returns* zile za kulipia *VAT* walianzisha mfumo wao mwezi wa tatu na ukiongeza idadi ya wafanyakazi ambao wamewapata *performance* imekuwa ni nzuri sana. *Performance* yao ukiiangalia kwa mwezi Machi kodi za ndani zilifikia asilimia 111.5 hongereni sana *TRA* kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Lakini vilevile ukiangalia upande wa *VAT* mwezi Aprili walifikia asilimia 103.8 *performance* yao kuzidi malengo na ukiangaliza namba zote wame *exceed* malengo waliyojiwekea. Maana yake ni kwamba endapo watakuwa na mifumo sahihi kama ilivyo hii ya *VAT* ni dhahiri kabisa Serikali inaweza ikafanya vizuri na hapa nataka niikumbushe Serikali kuna mfumo mmoja unaitwa *IDRAS* nilikuwa nateta na mwananchi mwenzangu pale bigwa Mheshimiwa Mwigulu kwamba *IDRAS* ni mfumo ambao utaisaidia sana Serikali katika kupata fedha kupitia kodi za ndani.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni kengele ya kwangu hiyo?

**SPIKA:** Hapana.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Sawa ahsante.

Mheshimiwa Spika, *IDRAS* ndiyo mwarobaini kwa sababu *IDRAS* itasimamia vizuri sana mifumo ya kodi za ndani kama ilivyo katika *VAT* kiasi kwamba mfumo huu ukiwa mahiri utaweza kuzungumza na mifumo mingine. Serikali imeonesha utayari wenu, sasa huu mfumo tunajua ni ghali na ilikuwepo na juhudi kuupata tangu Serikali ya Awamu ya Tano, lakini ile *tender* ika-*fail.* Sasa msitafute wafadhili, Mheshimiwa Waziri msitafute wafadhili, Serikali igharamie yenyewe mfumo huu, huu mfumo ndiyo utatuondolea matatizo. Angalia mfumo huu unaweza ukajumuishwa na miamala ya simu, mfumo huu unaweza ukajumuishwa na Forodha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia sentensi.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, mifumo ya Forodha na mifumo mingine yote ya *NSSF*. Kiasi kwamba hata *component* ya *pay as you earn* mtaipata ya kutosha kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, hivyo ningeiomba Serikali inapokuja kumalizia na kutoa hitimisho itueleze inajipanga vipi kuhakikisha kodi za ndani zinapata mfumo mahiri ili kuweza kutusaidia kukusanya fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya ajiandae.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara ya Fedha na Mipango kwa bajeti hii ya mwaka 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze mtani wangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba - Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri - Mheshimiwa Hassan Chande, Katibu Mkuu na timu nzima kwa kazi kubwa wanayofanya katika Wizara yetu ya Fedha na Mipango, lakini pia kwa ushirikiano mkubwa sana katika Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwa kusoma taarifa vizuri, lakini na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa sana sana wanaonipa katika kuongoza Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo; eneo la kwanza ni eneo la utendaji kazi kwa *TRA*. Niipongeze *TRA* kwa kazi nzuri, mwaka 2019/2020 tulikusanya wastani wa shilingi trilioni 1.5 kwa mwezi, lakini 2020/2021 tuna wastani wa shilingi trilioni 1.89 ni kazi kubwa tunayofanya. Tunawapongeza sana wenzetu hawa wa *TRA* pamoja na changamoto zote walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha ukusanyaji huu wa mapato ya *TRA* kuna mambo kadhaa ambayo nitayashauri; la kwanza, ni kuimarisha *Block Management System;* hili ni eneo ambalo wafanyakazi wa *TRA* hutembelea wafanyabiashara katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu na katika eneo hili kuna mambo mawili; jambo la kwanza, ni kuwabaini wafanyabiashara wapya ambao bado hawajaingia kwenye mfumo wa kodi na hili likifanikiwa basi tutakuwa tumepanua wigo wa walipakodi katika Taifa letu na hatimaye kuongeza mapato ya *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye eneo hili kuna wafanyabiashara wengi sana wadogo na wa kati ambao bado hawapo kwenye mfumo na ninaamini *TRA* wakati huu imeajiri sasa wafanyakazi wa kutosha, hii itasaidia sana kuwabaini wafanyabiashara wa kati na wadogo ambao pia hawa hawana *access* za mikopo katika benki zetu. Kwa hiyo, niwaombe sana Wizara ya Fedha iwabaini hao wafanyabiashara wa kati na wadogo na pia iwajengee mazingira mazuri ya kupata mitaji katika benki zetu za biashara, kwa maana ya kupata mikopo yenye masharti nafuu na riba nafuu ili kubaini wanaolipa kodi katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili katika hii *Block Management* ni kutoa elimu kwa wafanyabiashara ambao

tayari wamesajiliwa. Tukitoa elimu ya kutosha kwa walipa kodi wetu itaongeza *voluntary tax compliance*, itaongeza umahiri wa kulipa kodi, lakini bila kutumia gharama kubwa kwa maana kwamba ulipaji wa kodi wa hiyari. Kwa hiyo, niombe sana Wizara ya Fedha iwezeshe *TRA* katika eneo hili ili waweze kutoa elimu ya kutosha na hatimaye kupata kodi katika maeneo yetu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kufanya marejeo katika mikataba ya kutotoza kodi mara mbili yaani *Double Taxation Agreement*. Nchi yetu iliridhia mikataba na nchi mbalimbali katika kutotoza kodi mara mbili na nchi hizo ni kama ifuatavyo na naomba noisome; Mkataba wa kwanza ni Tanzania na Zambia mwaka 1968; Tanzania na Italy mwaka 1973; Tanzania na Norway 1976; Tanzania na Sweden 1976; Tanzania na Finland 1976; Tanzania na Denmark 1976; Tanzania na India 1979; Tanzania na Canada 1995; na Tanzania na nchi ya Afrika Kusini mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikataba hii yote ilikuwa na nia njema kabisa ya kuvutia wawekezaji *(Foreign Direct Investment),* kubadilishana teknolojia pamoja na huduma mbalimbali. Lakini mikataba yote hii ni ya muda mrefu sana mkataba wa kwanza wa mwaka 1968 ni miaka mingi karibia miaka 50 na kitu lakini hata wa mwaka 2005 ni miaka 17. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naliomba sana kwa kuwa suala hili ni la kisera naiomba sana Wizara ya Fedha, ni muda muafaka wa kufanya marejeo katika mikataba hii. Katika eneo hili kuna uwezekano mkubwa sana wa kupoteza mapato, kwa hiyo, niishauri sana Wizara ya Fedha iridhie ifanye marejeo ya mikataba hii ya muda mrefu ili tupate mapato ambayo tunastahili katika maeneo hayo ya mikataba ya kodi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni mafunzo kwa watumishi wa *TRA*. Mafunzo kwa watumishi wa *TRA* ni jambo la msingi sana hasa kwenye mawanda ya ukaguzi wa kodi, natambua kule kwa Idara ya Walipakodi Wakubwa kuna

Kitengo cha *International Taxation Unit*. Naomba sana bila kuwekeza kwenye elimu na mafunzo kwa watumishi wa *TRA* itakuwa ni jambo gumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *International Taxation Unit* kama nilivyosema, lakini kuna mambo ya *digital economic* sasa, kuna *transfer of pricing*, kuna *base oration and profit shift*. Kwa hiyo, kuna haja kubwa ya kuhakikisha watumishi wa *TRA* wanapata mafunzo ya ndani na pamoja na nje ya nchi. Sio vibaya pia wakaenda hata wakafanya *field attachment* kwenye nchi ambazo zimefanya vizuri kwenye maeneo ya ukaguzi ili na sisi kama Taifa tuwe na wabobezi wa kodi waweze kukagua maeneo mbalimbali ikiwemo na maeneo hayo ambayo nimesema ambayo ni ya kwenye biashara za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili linakwenda sambamba pia na ukaguzi wa kodi za ndani, najua wanafanya kazi nzuri, lakini bado kuna haja ya kuongeza mafunzo kwa wafanyakazi wa *TRA* katika ukaguzi wa ndani. *Tax Audit* huwa ni *a very good tool* ya *Voluntary Tax Compliance,* kwa hiyo, ni vizuri wenzetu hawa wakapata elimu ya kutosha, ili waweze kuwafikia walipakodi wetu na hatimaye waweze kukagua kodi mbalimbali katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, nitazungumza kwa ufupi eneo la mfumo wa kodi za ndani; tunaipongeza *TRA* kwa kuwa na mfumo imara sana wa Kodi ya Forodha unaitwa *Tanzania Customs Integrated System (TANCIS)* unafanya kazi nzuri ya kuonesha mizigo bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye kodi za ndani kuna changamoto ya mifumo, mara nyingi utaona mfumo haufanyi kazi. Kwa hiyo, niombe sana Wizara ya Fedha iwezeshe *TRA* kupata mfumo wa kisasa kabisa wa kodi za ndani kama alivyosema Mheshimiwa Tarimba. Ule kama nilivyosema ni mfumo mzuri, lakini ni lazima iwezeshwe ili tuwe na uhakika mfumo huu kufanya kazi, masaa yote na walipakodi wetu waweze kupata urahisi wa kulipa kodi kama ambavyo inatarajiwa.

Mimi baada ya kusema hayo nishukuru sana niipongeze tena Wizara na niiombe tu Wizara iiwezeshe *TRA,* ili iweze kukusanya makusanyo ya kutosha ili kuweza kufadhili miradi yetu ya maendeleo na huduma kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia kwenye hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo kusimama asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kwa kuipongeza Wizara ya Fedha na Mipango katika utekelezaji wa kazi zake na kazi ambazo ningependa leo kuwapongeza mahususi ni usimamizi wa bajeti ya Serikali na kuratibu upatikanaji wa fedha kutoka taasisi za fedha za kikanda na kimataifa. Kwa nini naipongeza kwenye usimamizi wa bajeti za Serikali, bajeti hii ni ya kwanza kwa Serikali ya Awamu ya Sita, lakini tumeshuhudia Wizara mbalimbali zilivyowasilisha bajeti yao hapa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022, zimeonesha Wizara nyingi zimepata kiwango kikubwa cha mafungu yaliyokadiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata hali ya makusanyo, lakini pia na matarajio. Lakini pia katika uwasilishaji wa bajeti za Wizara tumeziona zile Wizara za kimkakati za kuchangia katika kuona mapato ya Serikali yanapatikana mfano Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara zingine namna gani Waziri wa Fedha na Naibu wake...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara zingine zilivyojikita katika majadiliano ya kuona ongezeko la bajeti ya Wizara hizo mahususi ili zitoe mchango katika ukusanyaji wa mapato.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nilikuwa nataka nimpe taarifa tu kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita hii ni bajeti yake ya pili sio ya kwanza kama alivyosema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ni bajeti yake ya kwanza kwa sababu ile nyingine maandalizi yake yalianza tangu Novemba, 2020 huko. Kwa hiyo yuko sahihi Mheshimiwa Mbunge. Ndio maana jamani si kifo kilitokea Machi na Machi tulikuwa tuko kwenye Kamati, huwezi kusema hii ni Kamati yake ya pili kwa hiyo, yuko sawa sawa huwezi kusema hii ni bajeti yake ya pili.

Mheshimiwa Subira Mgalu endelea na mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunisaidia.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka niseme tulivyosikiliza bajeti za Wizara mbalimbali tumeona namna Wizara hii ya Fedha na Mipango ilivyowezesha Wizara hizo, kutekeleza bajeti ya mwaka 2021/2022 lakini na mipango thabiti ya bajeti ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nimeona pia nipongeze kwa namna ambavyo imeratibu upatikanaji wa fedha kutokana na Taasisi za Kimataifa na za Kikanda na mahususi mkopo wa shilingi trilioni 1.3 ambao hauna riba na utalipwa baada ya miaka 10 na tija iliyopatikana kutokana na mkopo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nimpongeze kipekee Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan kwa kuongoza mazungumzo yanayowezesha Taasisi hizi za fedha, kutoa fedha/mkopo wa bei nafuu kwa Serikali yetu na hivi karibuni pia tumesikia kazi nzuri tunatarajia kupata shilingi trilioni 1.2 kutoka kwa *IMF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo lakini pia naomba mchango wangu utajielekeza kwenye Mamlaka ya Mapato *(TRA).* Naomba niipongeze sana kwa kazi nzuri, mpaka Aprili, 2022 imekusanya zaidi ya asilimia 97 na hapa naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa uteuzi wako wa kuniteua mimi kuwa Balozi, Mamlaka ya *TRA* imekuwa ikitutumia kikamilifu kuhamasisha kulipa kodi kwa hiari. *(Makofi)*

Niipongeze Idara ya Mawasiliano kwa Umma na Elimu kwa Mlipakodi kwa kazi inayofanywa mikoa mbalimbali na kampeni ya Mlango kwa Mlango Kamata wote Matumizi ya *EFD*. Lakini niishauri Serikali tunapopita kuhamasisha malipo ya kulipa kodi kwa hiari kwanza Watanzania au wafanyabiashara wanaishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Wizara ya Fedha kwa kuifanya *TRA* kuwa kimbilio na kwamba wanawa-*engage* katika mazungumzo na mipango mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wanaomba ikiwezekana *TRA* au Serikali iangalie utoaji wa mashine hizi za *EFD* iwe bure ili ishawishi Watanzania wengi kuwa na hizo mashine, lakini itasaidia kuongeza kwa kiwango kikubwa malipo ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo niishauri Serikali itumie Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Idara za Biashara na Serikali za Mitaa na wale Wakuu wa Idara kwa sababu mfanyabiashara lazima apate leseni, kwa hiyo kupitia leseni Serikali itakuwa na uhakika wa kupata mapato yake.

Mheshimiwa Spika, lakini nishukuru sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu amevunja rekodi kwa kutoa vibali

vya ajira. *TRA* imeajiri wafanyakazi zaidi ya 1,000 kuelekea 2,000 wamepata semina nzuri, tuna matarajio na sisi Mabalozi tutaungana nao mlango kwa mlango kuhamasisha malipo ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nichangie kwenye Idara nzima ya Ukaguzi wa Ndani. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na jitihada za Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Wizara hii ya Fedha kutafuta fedha, lakini kama haitaimarisha kwa nguvu Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Ndani kwa kweli matumizi mahususi ya fedha hizi ili yafanye *value for money* tunaomba idara hii iwezeshwe. Lakini hata hizi Kamati za Ukaguzi *(Audit Committee)* kama ambavyo imeshauriwa na Kamati yetu naunga mkono maoni yote ya Kamati na kazi nzuri iliyofanywa, kupitia uwezeshaji wako tunaomba muundo wa *Audit Committee* utazamwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kati ya wajumbe watano watatu wanatoka ndani ya Taasisi na wanateuliwa na Afisa Masuhuli na kwa kuwa kikao kinaweza kikafanywa na wajumbe watatu tu, ambao ripoti yao inapelekwa kwa Afisa Masuhuli hapo Serikali itazame hili kwa nia ya kurahisisha utendaji wa kazi. Lakini kwa kuwa pia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, anaweza aka-*rely* katika kazi ya Mkaguzi wa Ndani na inaweza ikarahisisha pia kazi ya Mkaguzi wa Nje naiomba Serikali iimarishe ofisi hii kwa fedha, kwa vitendea kazi, lakini ikiwapendeza iwape *vote* yao ili iwe huru na ifanye kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo naomba nichangie Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali *(CAG).* Naishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha imekuwa ikiipatia fedha, lakini naomba iendelee kuiwezesha kutokana na kazi zilizoongezeka, miradi mbalimbali ya kimkakati na kaguzi mpya mfano *real time audit* (ukaguzi wa ufanisi) iwezeshwe fedha ili iweze kufanya kaguzi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali iwasimamie Maafisa Masuuli Serikali mnapata doa, kutokana na uzembe wa baadhi ya Maafisa Masuuli. Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anapokwenda kukagua anafanya *interest conference* anaeleza atakagua kwa mawanda ya aina gani *(sampling* yake) na anapoondoka anafanya *exit conference* anaacha hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na sheria imetaka ndani ya siku 21 hoja zijibiwe, lakini leo Maafisa Masuuli, wahasibu) wanachukua muda mrefu na hatimaye, hoja zinaendelea na kuwepo kwenye *CAG Report* inaonesha kwamba kuna upotevu mkubwa wa fedha, kumbe si kweli. Kwa hiyo, Serikali chukueni hatua kali katika hawa ambao hawatimizi wajibu wao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninakushukuru kwa kunipa fursa hii, ahsante sana kwa uongozi wako uliotukuka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali niweze kusimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwani siku ya jana sisi wananchi wa Jimbo la Meatu na wananchi wa Wilaya ya Meatu kwa ujumla, ilikuwa ni faraja kubwa kwetu sana kutokana na ule utiaji saini wa miradi 28 ya maji. Lakini Mheshimiwa Waziri aliendelea

kusisitiza kwamba mradi ule wa kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi ya kutoa maji Ziwa Victoria utatekelezwa mpaka Wilaya ya Meatu, Jimbo la Meatu. Kutekelezwa kwa mradi huu kutaokoa fedha nyingi inayotumika kufanya utafiti na maji yasipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nijielekeze katika hoja iliyopo mbele yetu na niishukuru Wizara ya Fedha na niunge mkono hoja. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa mwaka huu katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Fedha kazi kubwa sana mmeifanya. Kazi kubwa mmeifanya ya kupeleka fedha katika Halmashauri zetu, nadhani mwaka huu mmeweka historia katika upelekaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Tumezoea kuona miradi ya maendeleo ikipelekewa fedha kwa asilimia 36 mpaka 40 kwa mwaka mzima, lakini kwa mwaka huu hadi mwezi Aprili, 2022 miradi mingi imepelekewa fedha kwa asilimia 80 na kuendelea. Mimi nishukuru sana na niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zilizopelekwa nyingi tunategemea Serikali ya Chama cha Mapinduzi itatekeleza miradi hii ili kuwe na manufaa yaliyokusudiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo utajikita katika Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali hususani katika katika *level* ya Halmashauri. Fedha nyingi zinapelekwa, lakini sasa ni wakati muafaka Mkaguzi wa Ndani akawezeshwa kwa ufasaha ili aweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kwa mfano, Halmashauri ya Meatu yenye Majimbo mawili mpaka sasa hivi imepelekewa shilingi bilioni tisa za kutekeleza miradi ya maendeleo upande wa Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiongelea katika Jimbo la Meatu nasema shilingi 10,500,000,000 kwa sababu fedha zingine tunazipata katika Wakala wa Barabara na Wakala wa Maji. Lakini ukiangalia sasa Mkaguzi wa Ndani kuna upungufu mkubwa wa wakaguzi wa ndani katika Halmashauri yetu ukilinganisha na fedha nyingi sana zinazopelekwa katika miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mimi nishauri kuanzia sasa ipo haja Wakaguzi wa Ndani wakaanza kutekeleza majukumu yao kuanzia fedha zinavyopelekwa, wasisubiri miradi ipelekwe ndio waone changamoto ziweze kuibuliwa. Changamoto nyingi zinajitokeza katika utekelezaji wa miradi ambazo zingeweza kuzuiliwa na Mkaguzi wa Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao uhaba mkubwa wa watumishi tunaomba waongezwe, kuna changamoto ya vitendea kazi ikiwemo mafuta hata magari. Magari yao yamepelekwa miaka mingi sana na yalikuwa yakitumiwa na utawala. Mimi niombe Serikali iangalie, ipeleke magari kutokana na utekelezaji ulivyo wa kasi wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya fedha, fedha nyingi wanategemea wapewe na Mkurugenzi ambaye wanakwenda kumkagua. Hapo zamani walikuwa zilizokuwa zinapelekwa katika Fungu la *General Purpose,* lakini ile *General Purpose* Halmashauri zingine kwa sasa hivi hazipelekewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mkaguzi wa Ndani kuendelea kuwaomba Wakuu wa Idara/Mkurugenzi ambaye anakwenda kumkagua kwa hiyo anaweza apate sio kwa wakati ambao unatakiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi niombe Wakaguzi wapelekewe miongozo ya matumizi ya fedha inayopelekwa ili waweze kunusuru miradi ambayo inakwenda kutekelezwa kinyume na ilivyopangiwa. Nitolee mfano, Jimbo la Meatu lilipelekewa fedha za kutekeleza/kukamilisha maboma, lakini *user department* ambaye ni Mkuu wa Idara ya Afya alibadili matumizi. Tunayo maboma kumi ya zahanati, lakini alikwenda kuanzisha boma jipya, akaacha kukamilisha yale yaliyokuwepo ambayo ndio ilikuwa *base* ya kuombea zile fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 35 zilikwenda kuanzisha na mpaka nilipokuwa mimi natembelea lilikuwa

usawa wa kifua changu. Lakini mwaka huu wamepelekewa fedha nyingine za kukamilisha maboma mwezi Machi, Mkurugenzi alikuwa kwenye bajeti, yeye kwa kushirikiana na Afisa Mipango wamebadilisha fedha zile, badala ya kwenda kukamilisha maboma yale kumi wamekwenda kufanya miradi mingine wanayojua wenyewe. Lakini tukimuwezesha *Internal Auditor* ataweza kulizuia hili ndani ya *CMT* kabla halijapelekwa katika Kamati ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niunge mkono hoja ya Kamati kwamba kuna haja ya kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ili kuleta tija kwenye Kkitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Tunaona Kamati za Ukaguzi zinashindwa kufanya vikao vyao kutokana na ukosefu wa fedha, lakini muundo wake kama ulivyoelezwa bado hauleti tija katika kusimamia fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wanaweza wakaa akidi ikawaruhusu kufanya wakiwa watumishi wa Halmashauri, lakini mimi niliwahi kuhudumu Halmashauri moja Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi alikuwa Afisa Maendeleo ya Jamii. Hili liangaliwe, Wenyeviti wawe na weledi, wawe na uelewa wa uhasibu ili kuweza kuleta tija katika usimamizi wa majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano taarifa hii inawasilishwa kwa Afisa Masuuli wa Wilaya au wa Serikali ambaye ndiye mhusika aliyekaguliwa, kwa hiyo, yeye ni hiari yake aifanyie kazi ile taarifa au asiifanyie. Na hoja nyingi zimekuwa zikibaki mpaka zinakutwa na mkaguzi wa nje. Mimi niiombe Serikali ichukue maoni ya Kamati ya Bajeti ili sasa Mkaguzi wa Ndani awajibike moja kwa moja kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini niombe taarifa ya *internal auditor* iwe ajenda ya kudumu katika Kamati ya Ushauri ya Mkoa ili hoja ziwe zinafanyiwa kazi. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mheshimiwa Jerry William Silaa ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Wizara yetu hii muhimu kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nitumie nafasi hii kuwapongeza sana kwa usimamizi mzuri wa kamisaa wetu Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Hassan Chande, lakini niwapongeze sana watendaji wakiongozwa na wakuu wetu watatu hawa; Emmanuel Tutuba - Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na Naibu Makatibu Wakuu wawili; kaka yangu Lawrence Mafuru na dada Jenifa Omolo, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziada nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli kazi anayoendelea kufanya ni lazima tuseme, anafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri juu ya eneo la usimamizi wa sera za kiuchumi, uchumi jumla na akatuambia ni ukweli mambo makubwa ambayo yametusaidia sana ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kuendelea kubaki kwenye asilimia 4.9 ukilinganisha na asilimia 4.8 kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, kubwa sana ni kuwezesha shughuli mbalimbali baada ya UVIKO-19 kurejesha ile hali nzuri ambayo tulidhurika katika muda ule ambao watu mnakumbuka tulivyoingia kwenye UVIKO-19. Lakini ziada ya hapo pia kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya riba nafuu.

Haya ni mambo makubwa na ni ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Ndio amesababisha tukaendelea kuwa *stable* kama nchi katika hali ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitajielekeza katika maeneo kama mawili hivi, na muda ukiniruhusu eneo la tatu.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni madeni; nitumie nafasi hii kumpongeza tena kama wenzangu waliotanguliwa kusema, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutoa shilingi bilioni 772.87 kuweza kulipa madeni mbalimbali. Madeni ya wakandarasi zaidi ya shilingi bilioni nne, wazabuni zaidi ya shilingi bilioni 81.6, watumishi nje ya mishahara shilingi bilioni 25.7, watoa huduma shilingi bilioni 52.7 na madeni mengineyo zaidi ya shilingi bilioni 608.51, jumla yake ni takribani shilingi bilioni 772; siyo jambo la kawaida, ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, taarifa inatuambia yapo madeni mengine ambayo yako chini ya Msajili wa Hazina, yapo madeni ya mashirika na taasisi za umma ambayo yanatakiwa kulipwa na Msajili wa Hazina; hapa shida ipo.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wenzetu hasa wa sekta binafsi, wanajitahidi sana kujiinua kiuchumi kwa kukopa na kadhalika ili waweze kusaidia kutoa huduma Serikalini. Lakini Watanzania wengi wanakufa, wafanyabiashara wenzetu hawa wanaumia. Leo nataka nikwambie mfano mdogo sana, mwaka 2005 kampuni moja na hii niliwahi kuwasilisha hata kwenye Kamati Kampuni moja, *NICOS* ilifanya kazi na *TRL* wakati ule wa kampuni tanzui ile *HSC* sijui. Toka wakati huo, mwaka 2005, ikalipwa mara moja, mbili, baadaye mgogoro, mwaka 2009 mahakamani, mwaka 2014 hukumu ikatoka mumlipe pamoja na riba na gharama zake zote za mahakama. Mpaka leo mwaka 2022 miaka saba, kimya, hakuna cha kulipa wala kujibu barua.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho wa siku leo, baada ya kubanana sana watu ndio wanataka kwenda tena

mahakamani kusema hatujaridhika na hukumu ya mahakama ya miaka nane, siyo sawa. Huyu ni Mtanzania. Sasa huyu ni mmoja, je, Watanzania wangapi ambao wamekopa na leo wamefilisika kwa sababu ya kushindwa kulipwa madeni yao?

Kwa hiyo, niliona ni vizuri jambo hili wenzetu mliangalie kwenye sura ambayo itawasaidia Watanzania waweze kujiinua kiuchumi badala ya kuweza kuanguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme jambo la pili; wengine wamesema pia kuhusu Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani *(Internal Auditor).* Taarifa yetu inajieleza sana juu ya taarifa ya Mkaguzi wa Ndani kuelekezwa kwenye Kamati ya Ukaguzi *(Audit Committee),* na tukazungumza pale idadi ya watu watano, lakini tungetamani sana ili kuondoa *inpairness***,** wawili watoke ndani watatu watoke nje. Ushauri mzuri nami naunga mkono kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha, ukiangalia Taarifa ya *CAG* sehemu kubwa hasa kwenye *LGAs,* kwenye taarifa kule kwenye Halmashauri zetu, shida ikitokea kule kwenye Taarifa ya *CAG* anakwenda kubebwa *Internal Auditor,* Mhasibu na Mweka Hazina, hakuna wengine wanaobwebwa. Lakini furaha ikija kwenye taasisi ya kupata hati safi anapigiwa makofi Mkurugenzi na wasimamizi wao ambao ni Sekretarieti za Mikoa; hii ni shida. Jicho letu liende vizuri, niliwahi kushauri humu mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natoa *experience,* nimetumika kwenye Sekretarieti za Mikoa. Kuna mtu anaitwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani *(Regional Chief Internal Auditor),* hana kazi, hana kazi. Na kwa nini hana kazi, anahitajika akitumika huyu naamini *CAG* atakwenda kufurahi kufanya kazi zake vizuri na ata-*rely on the work of internal auditors.* Vinginevyo, kama alivyosema Mheshimiwa Subira, siyo lazima, sheria haimlazimishi *external auditor* aka-*rely* kwenye kazi ya *internal auditor,* akikuta *internal control* iko vibaya anaachana nayo, anakuja na ya kwake.

Mheshimiwa Spika, sasa liko jambo hapa, ni la kimuundo tu na nitoe mfano, Sekretarieti hizi chini kule, kutoka kwenye Sekretarieti za Mikoa kuna mtu anaitwa Katibu Tawala Msaidizi - *Local Government.* Huyu mtu ana vi-*organ* pale, yuko *autonomous* kabisa, katengeneza mtu wa fedha na katengeneza *internal auditor,* lakini hawa watu ni ma-*junior* sana, ma-*junior in such a way* kwamba hawawezi kwenda kusimamia kazi ya wakubwa wao chini.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kuna ma-*internal auditors* ambao ni Wakuu wa Idara wanakwenda kusimamiwa na *senior auditor* ambaye anatoka kwenye kitengo cha Katibu Tawala Msaidizi - *Local Government.* Kwa nini wakati kuna *Chief Internal Auditor* hana kazi, hawezi kushuka chini anaishia kufanya kazi kwenye ofisi za ma-*DAS* tu, ndiyo anakagua. Sasa huo u-*chief* wa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nashauri ni vizuri mkatengeneze muundo ili uboreshwe mumpe majukumu Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Mkoa aweze ku-*oversee* kazi za ma-*internal auditors* ambao kimsingi hata kwenye ikama zenu yule ni bosi wa ma-*internal auditors* wa *Local Government.* Kwa hiyo utaona ile *seniority* inaweza ikaenda vizuri. Na mwisho wakitoka na taarifa kimkoa basi ni vizuri sana ninavyoona *internal auditors* wanaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa dakika moja ni *contingency fund (CFE).*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30, kengele ilishagonga.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, basi hili niliache, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga atafuatiwa na

Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka ajiandae.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia Wizara hii ya Fedha.

Mheshsimiwa Spika, jambo la kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii adimu kuweza kuchangia Wizara ya Fedha ambayo inadai shilingi trilioni 14.94. Nimejaribu kuangalia mchanganuo pamoja na Mheshimiwa Waziri kweli mimi sina mashaka kulingana na mchanganuo jinsi nilivyouona hapa kwenye hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda muda wangu huu kuishauri Serikali kama zilivyo kanuni, taratibu na sheria zetu kwamba Mbunge ni mtunga sheria, halafu ni mshauri wa Serikali. Walipakodi nchi hii wanaolipa ni wachache sana, nakuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwanza kwenye Wilaya yangu mnisaidie nipate Ofisi ya Mamlaka ya *TRA* ili wafanyabishara waweze kupata huduma karibu. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Spika, ukiangalia Mkoa wa Geita sehemu nyingi hazina Ofisi za *TRA*, pale Mbogwe Ofisi ilishakamilika lakini bado haijafunguliwa. Kwa hiyo nikuombe Waziri ulichukue hili na uweze kunijibu kule mwishoni utakapotoa ufafanuzi wako kwamba sasa Mbogwe inaenda kufunguliwa Ofisi ya *TRA* ili kusudi wanaeonda zaidi ya kilometa 40 kwenda Bukombe kwenda kulipa kodi waweze kulipia karibu.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, mwaka jana nilisimama hapa, Naibu Waziri wa Fedha alikuwa Mheshimiwa Masauni nilikuwa nawalilia sana wafanyabiashara jinsi walivyokuwa wanapambana na *TRA*, lakini kwa sasa hivi bila unafiki kwa kweli kumekuwa na mazungumzo na makubaliano mazuri kwenye upande wa *TRA*.

Kwa hiyo nimpongeze Mkurugenzi wa *TRA* pamoja na Makatibu Wakuu wa *TRA*, najua mmeajiri vijana wengi katika sekta hii, niiombe Wizara hii sasa ijitahidi kuwapa mafunzo ili kusudi watakapoenda kwa wateja wetu, wananchi wetu, wafanyabiashara wetu wawe na kauli nzuri ili kuweza kuwafanya watu walipe kwa hiyari kama Rais anavyotaka maana nia ya Rais ni kumuona kila Mtanzania anafurahi, analipa kodi bila kusumbuliwa, watu wasivamiwe kama zamani walivyokuwa wakinyang'anywa na kufungiwa akaunti zao na kwa kweli mimi nikiri wazi tu nimetembea Taifa jirani hapa, kodi wakati ikifika mtu anaenda kabisa kulipa mwenyewe bila hata kufuatwa. Na neno la kodi hili ukiangalia hata kwenye maandiko matakatifu ni itu ambacho kipo halali. Kwa maana hiyo hapo hakuna maswali sana.

Kwa hiyo, tuombe tu hawa mliowaajiri muwape mafunzo ili wasije na munkari na morali za kutoka huko chuoni wakaanza tena kusumbua wananchi wetu na kutochonganisha tena nikawa mchango wangu huu leo nimeomba Ofisi ya *TRA* halafu wananchi wakaanza kukamatwa na kusumbuliwa, hapo nitakurudia Mheshimiwa Waziri kwa vile wapo chini yako. *(Makofi)*

Lakini ajenda ya pili nilete malalamiko ya wafanyabiashara hapa nchini, haya mabenki ya ndani yanawakanyaga sana wafanyabiashara wa ndani hapa. Tukiangalia tumetoka kwenye hili suala la *corona,* mfano kuna watu waliagiza mizigo yao China, kuna watu waliagiza mizigo yao mataifa mbalimbali, lakini wafanyabiashara hao wamekopa katika haya mabenki. Mabenki yameshinda kuwasikiliza, kuwapunguzia riba na kipindi naingia hapa Bungeni hotuba ya Rais wa Awamu ya Tano alitoa maelekezo kabisa kwamba riba zipungue kwenye mabenki. Lakini pia hata Mama Samia Suluhu Hassan wakati analihutubia Bunge hapa suala la riba aliliongelea hapa Bungeni kwamba riba zipungue. Waziri hizi taasisi zipo chini yako, unafeli wapi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Waziri ana mamlaka ya kuweza hata kufuta leseni ya hizi benki, maana kweli wanasiasa wengi

sasa hivi wanasimama wanasema nchi imefunguliwa, lakini kufunguliwa kwa nchi inaweza ikawa maumivu kwetu sasa. Kama sisi tunapigwa riba za juu wa ndani, halafu mgeni akija anapoozewa riba, inafunguliwaje hapo nchi? Si sisi sasa tumefungwa, wamefunguliwa wa nje! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuombe Waziri hili lichukulie *serious* sana, wafanyabiashara wa ndani wanaumia sana, halafu mbaya zaidi hizi taasisi za kifedha hazina kauli kwa wafanyabiashara wa ndani vizuri. Haziwavumilii kwa mfano mtu amerejesha marejesho tisa, bado marejesho matatu tu unaenda kukamata nyumba yake, unaenda kumfilisi, ina maana ulimpa mkopo huo umsaidie au kumfilisi hiyo nyumba aliyonayo?

Mheshimiwa Waziri kwa vile leo nimepata nafasi hii, nakushauri sana Rafiki yangu na nanakupenda sana na mtu anayekupenda ni lazima akueleze ukweli bila kukupongeza pongeza maana yake mtu anaweza akawa anakupa pongezi kumbe anategemea umpe chochote. Mimi ninakushauri kwa vile ni jamaa yangu najua ndoto zako bado Taifa tunakutegea sana. Kwa hiyo, livalie njuga hili na haya ya mabenki ya ndani yaweze kupunguza riba. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Kilimo alielekeza mabenki yatoe asilimia tisa tu kwenye kilimo, naona kama kwenyewe kunawezekana. Sasa huku kwingine kunashindikana vipi? Rais wa Kwanza alishasema na wa Awamu ya Sita alishasema riba zipungue, hazipungui. Futa leseni, zitasajiliwa benki nyingine tutakuja kufanya nazo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka nizungumzie hapa hali halisi ya maisha ya Watanzania wale wa kawaida. Kweli tunasema kwamba hali sasa hivi ina unafuu lakini bado hali ni ngumu. Sasa wewe kwa vile ni Waziri wa Fedha, angalia kama kuna sehemu yoyote fungulia fedha ili kusudi zifunguke hata kwa wanyonge zijae mifukoni, maana kwenye kampeni huwa tunasema tunawapigania wanyonge, sasa wanyonge

hawajapata fedha bado, ninaangalia tunaenda mwishoni mwishoni bado kuna Bajeti Kuu, na kwenyewe niombe viongozi mnipe nafasi niweze kuruka vizuri na kuweka mchango wangu vizuri maana ninayo mambo mengi, maana sikupata nafasi ya kuchangia Wizara nyingi sana, lakini zipo Wizara ninahitaji nipate nafasi ya kuweza kuwasemea wananchi wangu wa Jimbo la Mbogwe.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo sasa nikuombe Waziri wa Fedha kwa kuwa leo tupo Wizara hii ya Fedha kama kuna uwezekano wowote ule kufungulia mahali popote pale, fedha zifunguke ili kusudi hata na wananchi wangionge nao waende wakanufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa jitihada mnazozifanya, tumeona kwa watumishi mmeongeza mishahara, watumishi kwa kweli wanafurahi, walimu sasa hivi kila mwalimu anachekelea, watumishi mbalimbali wanafurahia kwa ongezeko hilo la asilimia 23.3 lakini wapo wengine ambao hawana nafasi ya kuweza kuingia kwenye manufaa haya. Kwa hiyo, ni vyema Waziri kwa vile ni msomi mzuri ujaribu kufikiria jinsi gani unaenda kulisaidia Taifa ili kila mtu apate haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, *yes* naomba kumalizia, mimi nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, maana nafasi ni ngumu sana kuzipata humu ndani, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Jerry William Silaa atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Fedha. Kwanza nami niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kazi kubwa anayoifanya na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia hotuba ya Waziri na yapo maeneo matano, kama muda utaniruhusu nitaomba kuchangia.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwenye bajeti hii tumeona Ofisi ya Msajili wa Hazina ikichangia shilingi bilioni 629 kutokana na magawio ya mashirika ya umma ambayo Ofisi ya Msajili wa Hazina inayasimamia, na nitumie fursa hii kumpongeza binafsi Msajili wa Hazina, Bwana Mgonja, na timu yake yote.

Mheshimiwa Spika, lakini niombe sana Serikali, tulisema hapa kwenye taarifa ya Kamati na ninaomba niseme hapa, mpaka ninapozungumza hapa yako mashirika 30 yasiyokuwa na Bodi za Wakurugenzi. Sasa kwenye mashirika haya, kwenye *cooperates,* Bodi ya wakurugenzi ndiyo kama Bunge lako hili.

Mheshimiwa Spika, unapokuwa na shirika ambalo lina *management,* halina bodi, hata zile hoja walizokuwa wanazungumza akina Mheshimiwa Subira Mgalu za kiukaguzi, hata zikifikishwa kwa afisa masuuli na bodi hakuna tija inakuwa iko chini sana. Niiombe sana Serikali iongeze kasi na itengeneze mfumo mahususi wa kuhakikisha mashirika haya bodi zinapomaliza muda wake basi kuwe na bodi mpya ili *succession plan* iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni eneo ambalo ningeomba niongee kwa msisitizo mkubwa. Ni eneo la kilimo. Kilimo cha nchi yetu kina--*employ* zaidi asilimia 65 ya watu. Ndio sekta inayoajiri watu wengi zaidi, lakini kilimo kina mchango mkubwa kwenye *GDP* ya nchi yetu takribani 29.1%.

Tulipata taarifa hapa kwamba Benki Kuu imetenga shilingi trilioni moja kama *stimulus fund* ya kusaidia kupata mikopo ya riba nafuu kwenye mabenki.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizonazo mimi mpaka hivi tunavyozungumza hata shilingi moja bado haijatoka Benki Kuu kwenda kwenye benki yoyote ya kibiashara ikiwemo Benki ya Kilimo. Nimuombe Mheshimiwa Waziri akija ku-*wind up* hapa atueleze hii trilioni moja iliyokuwa imetengwa na Benki Kuu kwa ajili ya kusaidia mikopo ya kilimo, maana wote mnafahamu mkulima, hapa ameongea Mheshimiwa Maganga, hizi rfiba anazoziongelea kwenye benki za biashara wanakopeshwa wafanyabiashara, wanakopesha watu wenye *security,* hakuna sehemu mkulima anaweza kupokelewa akakopeshwa na kama atakopeshwa kwa riba hizi anazoongea Mheshimiwa Maganga hakuna mkulima anaweza kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ndio maana tuliipongeza sana Serikali ilivyotenga hii trilioni moja tuliamini sasa muarobaini wa mikopo ya kilimo unaenda kupatikana, lakini mpaka sasa pamoja na kwamba masharti yaliyotengenezewa ile shilingi trilioni moja moja kwa moja yali-*exclude* Benki ya Kilimo kwa sababu inakosa zile sifa zilioainishwa kwenye masharti yale ya Benki Kuu tungetegemea kuona mikopo hii ya kilimo kwenye benki nyingine yanatoka.

Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa waziei akija ku-*wind* na sio vyema, kaka yangu, Yanga mwenzangu, kushika shilingi, lakini nitakuwa sina jinsi. Atueleze hii shilingi trilioni moja ni wakulima wangapi wa benki ipi wameshapata mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana sisi watu wa Dar es Salaam hatuna wakulima, lakini tunazungumzia nchi mzina, tunazungumzia Waheshimiwa Wabunge ni wakulima humu ndani, na sisi chakula cha Dar es Salaam kinatokana na kilimo cha nchi nzima. Kwa hiyo, tungependa kuona jambo hili linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, eneo la sensa. Niipongeze Serikali maandalizi yanaenda vizuri, lakini bado kuna kitendawili cha wale watakaotumika kufanya sensa ile ya watu na makazi. Tumeona kwenye *postcode, postcode* kule kwetu kuna asilimia imetekelezeka kwa utendaji mzuri na kuna asilimia imefeli kutokana na kupata watu, kweli tuna matatizo ya ajira, kweli vijana wetu hawana ajira, lakini unapata mtu ambaye hana weledi wa kiutumishi, anapewa kazi kwa kuwa ina posho ataomba, lakini unakuta mtu anatoka Msasani anakuja kuhesabu watu Gongo la Mboto, tija inakuwa iko chini.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri tu kwa Serikali, sensa za miaka ya nyuma zilikuwa zinatumia sana walimu. Walimu si tu kwamba wana weledi, lakini ni watumishi, wanaaminika, wanaishi maeneo yale, wanaheshimika na jamii. Kwani walimu wa nchi hii wamekosa nini? Wamekosa sifa gani kutumika kwenye maeneo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi niseme inawezekana tukachukua jambo hili kama tumetengeneza *solution* ya ajira ya vijana ambao hawana ajira, kweli tunataka kuwatetea, lakini tuangalie tija ya sensa.

Mheshimiwa Spika, na nitumie fursa hiyohiyo kutoa wito kwa wananachi kujitokeza kwa wingi sana kuweza kushiriki zoezi la sensa kwa sababu sensa hii ndio inaenda kujenga msingi wa maendeleo na utengaji wa fedha za miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, sio kwa umuhimu wake, kumekuwa na kilio kirefu cha wafanyabiashara wanapoenda kutafuta *TIN Number.* Mamlaka ya Mapato Tanzania inataka kuwe na *assessment,* kuwe na makadirio ya mapato na akipewa *TIN Number* ile robo ya kwanza alete marejesho. Anazitoa wapi na hajaanza biashara? Akina Mheshimiwa Katimba wamewahi kuchangia Mabunge ya nyuma, Wabunge wengi wamechangia, hivi kuanza na *assessment* ya *zero* tunapata tatizo gani?

Mheshimiwa Spika, ili mtu yule akianza biashara aje a-*declare* mapato aanze kulipa. Sasa unavyompa mtu *TIN Number* leo, ndio maskini wa Mungu labda kastaafu ama hana ajhira ama anajiajiri, kapata kiusajili chake, anataka *TIN Number* unamwambia wewe utaleta shilingi 400,000 kwa mwaka na robo ya kwanza ulete shilingi 100,000 anaitoa wapi? Ni kilio kikubwa, ni kilio kikubwa kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wa nchi hii ambao tunaomba sana Serikali iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ni mbia katika biashara hizi, mbia ambaye hatoi mtaji wala haji kufanya biashara kwenye maeneo haya, kwa hiyo, inatakiwa afahamu kwamba, mtu anapojitolea kufanya biashara ndio amejitolea kuwa mbia mpya wampokee vizuri watengeneze mazingira ya kumsaidia kufanya biashara, ili akipata yeye na kodi imepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa mmoja amechangia hapa kuhusiana na *EFD machine.* Kule kwangu kuna mfanyabiashara mmoja amenitumia *message* amefungiwa biashara kule *Kigogo Fresh Pugu*. Unamfungia mfanyabisahara duka kwa kuwa hana *EFD machine,* haya, sasa ameshafunga, unapata wapi kodi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo elimu itoke, lakini tuangalie mfumo mzuri wa kuwasaidia wafanyabiashara hawa waweze kufanya biashara vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JERRY W. SILAA:** Kengele ya pili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sekunde 30. Malizia sentensi.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nikushukuru wewe, sio kwa sura ile ya Mheshimiwa Maganga kwa kunipa nafasi ya kusema, maana nafasi zipo na

zinapatikana, lakini niendelee kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande - Naibu wa Fedha na Mipango ajiandae.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika Wizara hii ya Fedha. Kwa vile muda wangu ni mfupi nitasema kwa *points* zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Bajeti kwa jinsi ambavyo wameweza kuchanganua hii bajeti na pia kwa maagizo waliyotoa au ushauri walioutoa ambao ninaamini utasaidia sana katika kusimamia fedha za umma. Lakini pili nichukue nafasi hii kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)* kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuweza kuonesha yale maeneo mbalimbali ambayo yana ubadhirifu wa fedha ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi nizungumzie kuhusu Deni la Taifa. Fungu hili 22 limekuwa likipata hati isiyoridhisha kwa muda mrefu. Hii inatokana na mfumo ambao sio thabiti wa usimamizi wa kumbukumbu za madeni. Kwa hiyo, ningeishauri Serikali kwamba, iimarishe kitengo chake cha *Debt Management Office* ili kiweze kuweka kumbukumbu hizi vizuri, vinginevyo tutapata taarifa ambazo si sahihi. Na Kamati ya Bajeti nafikiri nimesikia wakishauri lianzishwe Fungu jipya na mimi naunga mkono, ili waweze kusimamia vizuri Deni la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nizungumzie kuhusu *Consolidated National Accounts* yaani Hesabu Jumuifu ya Taifa. Na fungu hili pia limepata hati ya mashaka kwa muda mrefu. Kwa miaka kadhaa hesabu za hili fungu jumuishi

zimekuwa zikipata hati yenye mashaka kutokana na kutokamilika kwa taarifa zake. Hivyo Wizara iimarishe ofisi hii ili iweze kufanya kazi yake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo pia niungane na wenzangu walionitangulia kwamba *tax base* ya nchi hii iongezwe kutokana na kwamba mpaka sasa hivi walipa kodi ni wachache sana. *So far* inaonesha ni kama watu milioni *2.7* ambao wanalipa kodi, ukiangalia nchi hii ilivyo kubwa na *population* ilivyo kubwa naamini wenzangu waliopita walivyoweza kushauri basi kuwe na wasimamizi wa kodi wanaoenda mpaka kwenye kata kule wanaweza kupata walipakodi wazuri. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba *TRA* izidishe kuongeza waajiri wenye utaalamu ambao wanaweza kwenda mpaka sehemu za kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna malalamiko kwamba *EFD machines* kwanza ni chache, pili hazifanyi kazi vizuri. Kila ukienda kununua kitu unaambiwa mashine hazifanyi kazi, kwa hiyo, ni vyema Wizara ikaangalia jinsi ya kuimarisha hizi *EFD machines. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nije na wazo ambalo nilifikiri kwamba linaweza likatusaidia sana, hapo nyuma tulikuwa na Tume ya Mipango ambayo ilikuwa haiko pamoja na Wizara hii ya Fedha. naamini kwamba, Tume ya Mipango ingeanzishwa au ingekuwa *re-established* naamini kwamba ingesaidia sana katika kuangalia mipango yetu na kuona *priority areas* zetu ambazo zinatakiwa ziangaliwe na zitengewe fedha zaidi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, kengele hiyo sijui ni ya kwanza? Au ya pili?

Mheshimiwa Spika, *anyway,* naamini kwamba Tume hii ya Mipango ni muhimu sana katika nchi yetu. Maana sasa

hivi Wizara ya Fedha ndio yenyewe ikae ipange, yenyewe ikae itoe fedha, hii sio sahihi kabisa. Tunatakiwa tuwe na tume ambayo ni *independent... (Makofi)*

**SPIKA:** Haya, sekunde 30 malizia sentensi.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, mimi niendelee kusema tu kwamba, niombe Ofisi ya *CAG* wapewe hela nyingi ili waweze kuibua sehemu mbalimbali ambazo zinatumia vibaya fedha za umma ili waweze kuongeza ile *sampling* yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mheshimiwa Mtoa Hoja ajiandae kuhitimisha hoja yake.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu, na mimi nitakuwa na hoja moja tu kuhusiana na maduka ya kubadilishia fedha za kigeni hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka mwaka 2018 Serikali iliunda *task force* na ikafanya uvamizi katika maduka haya ya kubadilishia fedha na hususan katika Kanda ya Kaskazini, mikoa ya Arusha na Kilimanjaro ndio ambao wameathirika kwa kiwango kikubwa. *Task force* hizi zilivamia maduka haya zikachukua fedha, zikachukua vifaa mbalimbali ikiwemo *computers, EFD machines,* baadhi ya wafanyabiashara wakachukuliwa hati za ardhi, na kadhalika. Na leo nazungumza hii ni kama mara ya tatu au sio ya nne ndani ya Bunge hili kutaka kujua kauli ya Serikali kuhusiana na wafanyabiashara hawa ambao wameporwa fedha zao toka mwaka 2018 mpaka leo hakuna muafaka wowote uliofikiwa kuhusiana na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mmechukua mpaka hati za ardhi za watu, mmechukua fedha *cash,* mmechukua vifaa mbalimbali, wafanyabiashara hawa hawajui hatima yao. Ni

lini Serikali mtafikia muafaka kuhusiana na mashauri haya ya wafanyabiashara hawa ambao mlikwapua fedha zao katika maduka ya kubadilishia fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi mmeunda tena *task force* mpya, mmeenda kwa wafanyabiashara hawa kuwaambia tena wanadaiwa. Sasa mmewachukulia kila kitu, mmewanyang'anya, bado mmeunda *task force* tena kuwaambia wafanyabiashara hao wanadaiwa, kwa nini? Na kwa nini mnafanya kazi kwa *task force* tu ya kutishia watu na si kuleta amani na muafaka ili watu wafanye biashara kwa uaminifu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, naomba tupate majibu ya kina na ya ukweli. Na wafanyabiashara hawa wanataka kujua hatima ya fedha zao mlizozichukua bila utaratibu.

Mheshimiwa Spika, na niliwahi kusema hapa, hawa watu wanavyofanya biashara wana leseni za biashara, wamefuata taratibu zote, hakuna mtu ambaye alikuja tu akawa anafanya biashara hajafuata taratibu. Mliwatambua, walifanya biashara kwa utaratibu, kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni. Bado mkaja mkawanyanyasa na kuwavamia na kuwachukulia fedha na kila kitu. Naomba kupata majibu Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni mara nyingi nimeshaongelea suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama haitoshi mmeweka masharti mapya magumu ya watu wanaotaka kufanya biashara ya kubadilisha fedha kwa kuanzisha maduka. Mmeweka masharti magumu sana ambayo kwa kweli, hayawezi kutekelezeka. Mnataka mtu ili apewe leseni hii awe na fedha shilingi bilioni moja ndio aweze kufungua, na tena katika hiyo bilioni moja ili aweze kupata sasa leseni na kibali, maana yake awe na fedha asilimia 70 ya hizo fedha, maana yake ni shilingi milioni 700. Hivi kwa nini kuna ugumu kwenye jambo hili katika kufanya biashara hii?

Mheshimiwa Spika, huko nyuma watu walifanya biashara, Arusha ndio biashara ambayo ipo na Kilimanjaro

kwa sababu ni miji ya kitalii. Sasa kwa nini mnaweka masharti haya magumu kiasi hicho? Kuna nini kimejificha hapa Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi wako baadhi ya wafanyabisahara pamoja namasharti hayo magumu, wako baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekidhi hivyo vigezo. Wameleta maombi, lakini mpaka leo wana karibu miaka miwili, mitatu, hamjatoa leseni, kuna nini hapa? Kuna nini ambacho kimejificha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, ningetamani nipate majibu ya masuala haya niliyoyaeleza, lakini kama haitoshi tunataka kujua hii biashara ya kufungua maduka ya kubadilishia fedha ndani ya nchi hii, kama mtangaze ni janga mseme ni janga, kama mnaona ni biashara ambayo ni hatari muwaambie. Hawa wafanyabiashara wamekaa hawajui hatima yao, hata hao wapya ambao wamekidhi vigezo wameleta kwenu bado mmekaa kimya, kuna nini hapa ambacho kinaitishia Serikali na mnapata kigugumizi kuhusiana na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Langu ni hilo na kama sitaridhika nafikiri tutakutana kwenye shilingi baadae Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba kwa kazi kubwa anayofanya hasa katika kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaendelea kuwa imara. Nampongeza pia Mheshimiwa Hamad Hassan Chande - Naibu Waziri, Ndugu Emmanuel Tutuba – Katibu Mkuu Fedha na Mipango, pamoja na Naibu Katibu Mkuu pamoja na timu yote ya Wizara. Kwa namna ya pekee nimpongeze mwenye fedha mkuu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nina maombi yafuatayo; naomba mtupitishie maombi yetu ya fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Halmashauri ya Nyasa, taarifa za ngazi zote zipo tayari na imebakia ruksa yenu. Hata hivyo natoa shukrani nyingi kwa hatua iliyofikiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma za kikodi tunashauri Wilaya ya Nyasa nayo ijitegemee ki-*TRA* badala ya kuwa mtoto wa Mbinga.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake Mheshimiwa Hamad Hassan Chande na wataalamu wa Wizara pamoja na wadau kwa kazi nzuri wanayofanya katika sekta ya fedha na uchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalo jukumu kubwa la kuwapatia wananchi huduma bora za umma. Ili Serikali iweze kutimiza wajibu wake kwa umma, inahitaji kuwa na rasilimali fedha ya kutosha inayotokana kwa kiasi kikubwa na makusanyo ya kodi kutoka vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jukumu hili limeainishwa vizuri sana katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025. Kama Serikali itashindwa kukusanya mapato ya kutosha kupitia mamlaka husika, uwezo wake wa kutoa huduma bora kwa Watanzania utakuwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na tatizo la kupoteza sehemu ya mapato yanayotokana na kodi kutokana na sababu mbalimbali. Upotevu wa mapato ya Serikali husababishwa na yafuatayo:-

Moja, asilimia kubwa ya wafanyabiashara wadogo *(SME's* na Wamachinga) hawajadhibitiwa na kuwekwa rasmi

kwenye mifumo wa kulipa kodi. Idadi yao ni kubwa lakini mchango wao kwenye kulipa kodi ni mdogo sana.

Pili, ukwepaji wa kodi; katika hili imejidhihirisha kwamba watu wachache sana, hasa hasa walio kwenye ajira na sekta rasmi ndio wanaolipa kodi, hivyo kubeba mzigo wa wale wasiolipa kodi, ambao bado wanafaidi bidhaa na huduma za umma sawasawa na wale wanaolipa kodi. Walipakodi waliosajiliwa kukusanya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ni walipakodi wachache na hawa ndio wanaotumia mashine za *EFD.*

Tatu, kwa kiasi kikubwa, wafanyakazi wa Halmashauri nyingi nchini wenye majukumu ya kukusanya kodi pamoja na sehemu kubwa ya wafanyabiashara walio rasmi na wasio rasmi hawana mashine za kukusanyia kodi. Hii imesababisha Serikali kupoteza kiasi kikubwa cha mapato.

Nne, upotevu kwenye misamaha ya kodi; baadhi ya misamaha ya kodi iliyotolewa na Serikali kwa nia nzuri imekuwa ikitumika visivyo kuwanufaisha watu au makampuni yasiyostahili. Hali hii imekuwa ikisababisha upotevu wa fedha za Serikali.

Tano, utoroshwaji wa mali na fedha nje ya nchi; viwango vipya vya upotevu wa mapato yatokanayo na utoroshwaji wa fedha nchini kwenda nje ya nchi ni dola za Kimarekani milioni 464 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu, natoa mapendekezo yafuatayo kwa Serikali; kwanza naishauri Serikali iwe na mkakati wa kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo na wale wasio rasmi, iwasajili kwenye maeneo yao na kuweka mifumo rasmi ya kuwalipisha kodi kutokana na shughuli wanazofanya. Kufanikisha hili, Serikali inashauriwa kuajiri watumishi wa kutosha ili wasaidie kufanikisha azma hii.

Pili, naishauri Serikali ipunguze misamaha ya kodi na hii itolewe kwa wanaostahili baada ya kufanya tathmini ya kutosha kubainisha wahitaji sahihi; tatu, naishauri Serikali

iboreshe uwazi katika utoaji wa misamaha ya kodi; nne, naishauri Serikali iendelee kuelimisha wananchi na kuwajibisha wale wote wanaohusika na ubadhirifu au wanaokiuka sheria zinazosimamia fedha za umma.

Tano, naishauri Serikali isambaze kwa wafanyabiashara wote mashine za kukusanya kodi *(EFD),* na izidi kuwekeza katika mifumo ya kielektronki ya ukusanyaji kodi, hata katika ngazi ya Halmashauri na wafanyabiashara wadogo wadogo; sita, naishauri Serikali itekeleze kwa makini suala la mapitio ya sheria mbalimbali ili makampuni yote yalipe kodi stahiki; na saba, naishauri Serikali itoe elimu kwa wananchi wote ili watambue kuwa ni wajibu wao kulipa kodi kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya haya, mapato mengi yataweza kukusanywa na hivyo kuwa katika nafasi nzuri ya kupata huduma muhimu na kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** *Mheshimiwa Spika*, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

*Mheshimiwa Spika*, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

*Mheshimiwa Spika*, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha ubunifu wa ukusanyaji mapato na usimamizi mzuri wa matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na

uendelezaji wa miradi ya kimkakati na pia utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness).* Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni *kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi kumi ya bajeti ya mwaka huu, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imesimamia kwa ufanisi ukusanyaji mapato na utekelezaji wa miradi mingi ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na kadhalika. Napongeza Serikali kwa mwendelezo mzuri wa utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa umeme Mto Rufiji. Mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uboreshaji wa bandari utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. Umeme, reli na bandari ni nguzo imara ya kiushindani katika uchumi wa Tanzania na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

*Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki wakati dunia inapambana na janga la *corona virus (covid-19),* tumejifunza umuhimu wa kuwepo kwa mikakati mbadala kutokana na nchi nyingi tunazoshirikiana kibiashara na kiuchumi kukumbwa na mtikisiko wa kiuchumi. Biashara ya usafirishaji hasa wa anga imeathirika sana na napongeza mkakati wa shirika la ndege kuanza kutumia ndege zake kusafirisha mizigo. Mkakati huu ambao umetumiwa na hata mashirika makubwa ya ndege utawezesha usafirishaji wa mazao yetu ya kilimo kufikia masoko kirahisi na hapo hapo uhakika wa mapato kwa shirika la ndege hasa kipindi hiki kukiwa na upungufu wa abiria. Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Msajili wa Hazina anapaswa kuendelea kuimarisha mitaji kwa mashirika ambayo yatachochea ukuaji wa uchumi ikiwemo Benki za *TADB, TIB* na *ATCL* ili iweze kusimama kibiashara ikiwa ni nguzo muhimu hata kwa sekta zingine.

*Mheshimiwa Spika*, napendekeza kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea hata kwa kutafuta vyanzo mbadala vya fedha kugharamia ujenzi huo, kwa vile kutakuwa na fursa

kubwa za usafirishaji. Pamoja na ujenzi wa *SGR,* napendekeza kuendelea na kuboresha reli ya *TAZARA* na uboreshaji wa bandari zetu ikiwemo ujenzi wa bandari kavu ikiwemo ya Inyala, Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki ili kupunguza gharama za kusafirisha pembejeo na mazao. Serikali ichukue hatua za haraka kuinusuru reli ya *TAZARA* hata ikibidi kurekebisha mikataba ya umiliki na uongozi ili mradi iendeshwe kwa tija.

Mheshimiwa Spika, kuna kuchukua hatua za makusudi kwa kutumia zaidi *TAZARA* kusafirisha mizigo ambayo imeelemea hata uwezo wa barabara zetu. Usafirishaji wa mizigo kwa kutumia *TAZARA* ilenge kupunguza gharama za pembejeo kwa wakulima na wakati huo kupunguza gharama za kusafirisha mazao ya wakulima.

Napendekeza Serikali iwekeze angalau shilingi bilioni 100 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya kuboresha mindombinu ya reli na karakana. Uwekezaji huu utawezesha *TAZARA* kujiendesha kwa faida na kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipa zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa mwaka ikiwa ni mishahara ya wafanyakazi wa *TAZARA*. Uwekezaji huu unahitaji haraka wakati Serikali za Tanzania na Zambia zinaendelea na jitihada za kurekebisha mikataba ikiwemo wa uendeshaji wa *TAZARA*. Pamoja na kuboresha *TAZARA*, napendekeza kukamilisha taratibu za ujenzi wa bandari kavu ya Inyala, Mbeya ambapo Mamlaka ya Bandari kwa kipindi kirefu wamewahakikishia wananchi kulipa fidia ya eneo lao wanalolichukua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za mapato kutokana na janga la *Covid-19,* kuna fursa nyingi za muda mfupi za kuongeza mapato kupitia hatua za kiutawala kiwemo ya kuondokana na matumizi na malipo ambayo hayana tija kwa Serikali na hata walipakodi. Kutokana na mahitaji makubwa ya uwekezaji kwenye miradi ya kimkakati, uchumi wetu utaendelea kuwa na mahitaji makubwa ya mikopo ya pesa za kigeni na wakati huo huo kulipa mikopo iliyoiva.

Pia Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha mapato ya fedha za kigeni yanaongezeka kupitia mazao ya kilimo, madini na utalii. Kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yatasaidia kuimarisha Deni la Taifa kuwa himilivu na pia kuendeleza utulivu wa shilingi yetu dhidi ya sarafu kuu za kigeni na hata kuhakikisha utulivu wa mfumuko wa bei. Serikali ihakikishe kipaumbele cha kuwekeza kwenye kilimo ikiwemo pembejeo na umwagiliaji kwa lengo la kuongeza tija na pia kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kulinda mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upotevu mkubwa wa fedha za Serikali ikiwemo miradi ya Serikali Kuu na Halmashauri, napendekeza Serikali kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kuongeza ufanisi na uhuru wa Wakaguzi wa Ndani. Serikali ihakikishe Mkaguzi wa Ndani wakati wote anakuwa huru kutoka kwa Afisa Masuuli. Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri wasimamiwe na Mkaguzi Mkuu wa Mkoa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Serikali iimarishe uhuru wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani *(Internal Auditor General)* na hata kupandisha hadhi ya Ofisi kuwa na Fungu la Bajeti linalojitegemea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, halafu Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, Rahim, kwa kutuwezesha kujadili hapa katika hali ya uzima na afya, lakini pili nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tatu, naomba nikushukuru wewe Spika na nikupongeze sana kwa kazi nzuri ambayo unaifanya, na hili, wote ni mashahidi na tunaamini kwamba, kwa mujibu wa tafiti wanawake wanapopewa nafasi ama wanapokuwa na nafasi hawajawahi kushindwa, kwa hiyo, nawapongeza sana, lakini pili wanakuwa ni waaminifu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nimpongeze na nimshukuru pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Makamu wake na Wajumbe wenzangu wote kwa namna walivyotupa ushirikiano mkubwa katika suala letu hili, lakini niwashukuru pia Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wao wote na michango yenu yote ambayo mmeitoa. Ni michango yenye afya, yenye dhamira ya kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Waziri wangu, Waziri wa Fedha na Mipango, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, yeye kwangu huyu ni *mentor* yaani ni kocha mzuri ambaye anatupa maelekezo na tunaenda vizuri na kufanya kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia watendaji wenzangu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kiasi kikubwa sana ambapo wanatupa ushirikiano katika kazi zetu za siku hadi siku wakiongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Makamishna na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze tu moja kwa moja katika mjadala ama hoja ambazo zimejadiliwa hapa leo na nianze na maoni ya Kamati; Kamati iliona kwamba tuna uhaba mkubwa wa wafanyakazi ama watumishi wa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, hili nikiri ni kweli kwamba *TRA* watumishi wetu bado ni haba, lakini Serikali imechukua juhudi mbalimbali za kuongeza watumishi hao. Ndani ya mwaka huu Serikali imedhamiria kuajiri vijana 2,100 na tayari vijana 1,443 wamesharipoti kazi na wameshapatiwa mafunzo ya kiutendaji na 657 wamo katika mchakato wa kupatiwa ajira ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja imezungumzwa kuhusu mali chakavu au vyuma chakavu. Baadhi ya watu wanaziita mali kachara. Ni kweli zipo na mchakato ule unaonekana ipo haja ya kufanyiwa mapitio. Hili tumelichukua na tutalifanyia mapitio ili kusudi mauzo ya mali kachara ama vyuma chakavu vile yaende kwa haraka sana katika mchakato wake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nizungumzie suala la forodha ambalo amezungumza ama ametoa maoni Mheshimiwa Mbunda, jirani yangu pale kwamba ipo haja ya kufungua ama kuweka Ofisi za Forodha katika mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, hili tumelichukua na tayari limeanza kufanyiwa kazi na Serikali. Sasa hivi Serikali, iko timu maalum ambayo imeundwa inafanya tathmini ya sehemu kwa mfano kama vile Momba na sehemu nyingine kuona kwamba kama ipo haja ya kufungua Ofosi za Forodha latika mpaka fulani, basi Serikali haitasita na ipo tayari kutufua Ofisi za *TRA* katika mipaka yetu hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nizungumzie suala la ukusanyaji wa mapato ambayo Mheshimiwa Tarimba kwa kiasi fulani amegusa kidogo kwamba ipo haja ya kutanua wigo nalo hilo pia limechukuliwa na Serikali na Serikali imefanya juhudi hizo hata kama alivyosema yeye mwenyewe vijana 360 wamechukuliwa kuwekwa kwa muda, siyo waajiriwa lakini wanasaidia ukusanyaji wa fedha na kutoa taaluma kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimuite Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote niwashukuru

sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na niwaambie kwamba michango yao tumeipokea baadhi nitaisemea hapa, lakini nitawaomba waridhie mingine tutaitoa kwa maandishi na kwa hotuba tutakapokuwa tunawasilisha Bajeti Kuu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Chande kwa ufafanuzi wa hoja ambazo amezitoa na kwa ushirikiano ambao amekuwa akinipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, la tatu, niwapongeze Kamati ya Bunge wakiongozwa na Mwenyekiti pamoja na Makamu wake, Kamati nzima pamoja na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake kwa kweli kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaelezea hoja zilizotolewa na Wabunge naomba mambo haya nitakayosema yaingie kwenye kumbukumbu. Jambo la kwanza naomba Bunge lako tukufu litambue ukubwa wa kazi aliyonayo Mheshimiwa Rais ya kuwezesha miradi ya maendeleo iweze kufanyika katika nchi yetu. Hili jambo baadhi ya watu ambao hawajaangalia takwimu za nchi yetu zinasemaje wanaweza wasijue kazi aliyonayo Mheshimiwa Rais japo wanaona mambo yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu karibu kila kitu ni cha lazima, karibu kila kipengele cha matumizi ni kipengele usichoweza kukiahirisha, kipengele hicho ndicho kinachofanyakazi iwe ngumu sana kwa sababu karibu kila *expenditure item,* kila kipengele cha matumizi unachokigusa ni kipengele usichoweza kukiahirisha. Kwa mfano tumetoa kwenye taarifa yetu kwamba makusanyo yetu ya ndani yalikuwa shilingi trilioni 19.99 ukienda kwenye mchanganuo wa haraka Deni la Taifa kwa mwaka linachukua karibu shilingi trilioni 6.9 ni kama shilingi trilioni saba hivi, mishahara ukiweka na tunakoelekea itachukua zaidi ya shilingi trilioni sita na sehemu ukiweka na mahitaji mengine ambayo ni ya lazima.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye miradi mikubwa reli peke yake tuna zaidi ya shilingi trilioni 1.45 kwa miradi ambayo kwa *lot* ambazo zilikuwa zinaendelea. Ukienda kwenye barabara tuna zaidi ya shilingi bilioni 579 ambazo hizi zinapitia kwenye *TANROADS,* ukienda kwenye *TARURA* barabara za vijijini ambazo fedha hizo ziko kwenye mifuko hugusi gusi tu ni zaidi ya shilingi bilioni 414 kwa mwaka, ukienda kwenye elimu ya juu peke yake ni zaidi ya shilingi bilioni 423.5, ukienda kwenye *REA* ni zaidi ya shilingi bilioni 367, ukienda kwenye maji ni zaidi ya shilingi bilioni 346, ukienda kwenye elimu bila malipo ni zaidi ya shilingi bilioni 202. Hapa unaongelea kwenye mahitaji yale usiyoweza kuyaahirisha ni shilingi trilioni 16.5 kati ya shilingi trilioni 19 hayo ni yale mahitaji usiyoweza kuyaahirisha, yale ambayo fedha zake zimehifadhiwa mahsusi kwa matumizi yale.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake afya peke yake inachukua zaidi ya shilingi trilioni 2.5, elimu inachukua zaidi ya shilingi trilioni 5.6, maji yanachukua zaidi ya shilingi bilioni mia nane na nusu na *social production* inachukua zaidi ya shilingi trilioni 1.8. Unaweza ukaona ni *space* kiasi gani inayosalia kwenye matumizi ya shughuli zingine, ni kiasi gani kinachosalia kwenye shughuli zingine haya ni matumizi mengine ambayo hauwezi ukarudi nyuma pawe na UVIKO, pawe na vita Ukraine, pawe na ukame, haya ni matumizi ambayo huwezi ukayaahirisha.

Mheshimiwa Spika, kazi hii yote ndiyo inayomfanya Mheshimiwa Rais asilale, ndiyo maana utaona leo yuko huku, leo yuko huku na wengine wanadhani haya mambo yanaweza yakaenda hata pasipokuwa na mwanga, hata pasipokuwa na jua limewaka. Mimi nawaulizeni swali dogo tu ni Waziri gani wa Fedha wa nchi za kiafrika anaweza akafanya *appointment* ndani ya wiki moja akaonana na Rais wa Benki ya Dunia? Ni Waziri gani wa nchi za Kiafrika anaweza akafanya *appointment* ndani ya siku tatu akaonana na Rais wa *IMF? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo yanafanyika kwa uzito wake na Mheshimiwa Rais anaona

ayaongezee nguvu na ndiyo maana unaona alipoenda kwenye nchi za Ulaya alionana na taasisi zote zile za muhimu kwa shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alipoenda Marekani alionana na taasisi zote hizi za muhimu kwa wiki moja ameonana na Rais wa Benki ya Dunia, Rais wa *IMF* na ameonana na Makamu wa Rais wa nchi kubwa kama ya Marekani na mimi namshukuru sana alinifanya niwe Mnyiramba wa kwanza kuingia Ikulu ya Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni sehemu tu ya kazi kubwa ambazo zinalazimika Rais aingie mstari wa mbele ili kazi hizi ziweze kwenda. Hivyo hivyo na alivyokuwa Falme za Kiarabu kule alionana na viongozi wakuu wote wale na maeneo mengine yapo ambayo yanakuja ambako yatatusaidia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, nimshukuru sana na nimpongeze na niwaombe watanzania waielewe kazi hiyo ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alisemea Mheshimiwa Mbunda pamoja na Wabunge wengine waliochangia kuhusu jambo la ukaguzi wa ndani, tumepokea hoja hiyo tutaitolea ufafanuzi tutakapokuja kwenye Bajeti Kuu.

Kuhusu Ofisi za Mamlaka ya Mapato tumepokea hilo nilishapokea na baadhi ya Wabunge wengine ambao wameongelea katika Bunge hili wakiwa wanaongea wengine kupitia maswali pamoja na hawa ambao ameongelea tumelipokea na hilo tutabainisha na mipaka mingine tutatembelea na tutachukua uamuzi baada ya tathmini ili tuweze kuwarahisishia wananchi utaratibu wa kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumepokea suala la chuma chakavu na Naibu Waziri ameliongelea vizuri. Tumepokea hoja pia aliyoisemea ndugu yangu Tarimba mwananchi bingwa mtarajiwa ambaye amelielezea sana katika eneo hili la kutumia mifumo ni njia ambayo itatupa ufanisi na

Mheshimiwa Rais amelisisitiza sana hili na sisi ndani ya Wizara tunaendelea kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameongelea Mwenyekiti wangu wa Kamati Mheshimiwa Sillo mazingira ya kufanyia biashara hii ni kazi kubwa tunaendelea nayo namna ya kutekeleza *blue print* yetu ambayo imebainisha maeneo mengi sana ambayo yatatupa mazingira mazuri ya kufanyia biashara zikiwemo biashara kubwa pamoja na biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine ambayo ameongelea yanayohusiana na mikataba ya *double taxation*. Mafunzo tumepokea na hilo ni jambo ambalo tunatoa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mama yangu Leah pamoja na Wabunge wengine wameongelea fedha za miradi na kwa kweli kazi kubwa sana imefanyika kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea karibu mikoa yote ya nchi yetu imepata zaidi ya asilimia 100 ya fedha za maendeleo walizokuwa wanatarajia kuzipata katika mwaka huu wa fedha na ndiyo maana mnaona miradi ya maendeleo inaenda kwa kasi ambayo inastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemsikia ndugu yangu Mtemvu, nimemsikia rafiki yangu Maganga Ofisi ya *TRA* nitatembelea, tutaenda kuifungua na Maganga wewe ni kichwa ulitoa wazo la kununua mitambo ya kutengenezea barabara wazo lako tulilitekeleza katika Wizara ya Maji na tutaangalia na katika maeneo mengine na kuhusu masuala ya riba tunaendelea kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachotumia kwenye riba ni utaratibu kwamba soko letu tunatumia nguvu ya soko katika kuamua masuala haya ya kiuchumi. Majirani zetu waliwahi kujaribu kutumia nguvu ya dola kuweka ukomo kwamba asubuhi tu tunaamka tunasema leo riba itakuwa asilimia tano, ilileta madhara kiuchumi kwa sababu hivi viashiria vya

kiuchumi mpana huwa vinategemeana, unaweza ukakiathiri kimoja ikaleta tatizo kwenye viashiria vingine. Kwa hiyo, tutaendelea kutumia nguvu ya soko lakini pia na ya kisera kuweza kuhakikisha kwamba tunafika katika hatua hiyo hili linakwenda likitekelezeka na tunaamini itaenda kufanyika na kukamilika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jerry nimesikia haya masuala ya Bodi tutayajibu katika hotuba kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu nani atatumika kwenye sensa, sasa hivi vijana hata ukiondoa walimu tuna vijana ambao ni wasomi ambao na wenyewe ni walimu kimsingi wengine ni walimu, wengine ni walimu wa akiba.

Kwa hiyo, tuliona kwa sababu zoezi hili linahitaji watu wengi sana, walimu watatumika kufundisha, watatumika kusimamia, lakini na hawa vijana ambao wengi wao wameshasoma, ni wasomi wazuri na wenyewe watafanya hiyo kazi huku wakishirikiana na walimu ili tuweze kuleta ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa tulilolifanya tumefanya hawa vijana watoke katika maeneo yale yale ambayo watayasimamia ili kupunguza gharama kwa sababu kwa sasa hivi hakuna kata isiyo na wasomi. Kwa hiyo, tuliona watumike kule kule waliko ili waweze kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Cecilia pamoja na mama mkwe wangu pale Mama Kaboyoka nimepokea jambo hilo tutalisemea kwenye hotuba kubwa, lakini hili la maduka ni jambo ambalo tunaendelea kulifanyia kazi, hatujamaliza idadi yote, lakini tunaendelea kulifanyia kazi na Mheshimiwa Cecilia mtani wangu, ukihitaji takwimu pia nitakupatia, lakini hatujafika mwisho kwa sababu tunafanya kwa umakini, lakini nikuhakikishie ni zoezi ambalo linaendelea kufanyiwa kazi na wewe ukitafiti zaidi utapata taarifa kama hizi

ninazokwambia na baadhi ya watu wameshapata utekelezaji wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu wale walioomba leseni mpya pamoja na yale masharti hilo ni jambo kubwa la kisera nitaomba uridhie ili tulitolee tamko baada ya kuwa tumeshakamilisha hotuba yetu kubwa tunayoiandaa ili tuweze kutoa tamko ambalo litahusika na watu wengine wote waweze kufuata muongozo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hiyo kama nilivyosema mambo mengine tutayajibu kwenye hotuba kubwa ya bajeti, nakushukuru na nakupongeza kwa kuendesha kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema maneno hayo naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu Namba Mbili ambacho ni Matumizi ya Kawaida ukurasa wa 334. Tunaanza na Fungu Namba 50 – Wizara ya Fedha na Mipango.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 050 – Wizara ya Fedha na Mipango**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*........................ Sh.10,505,104,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na wapo Wabunge ambao wanataka ufafanuzi hapa; Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikiri tu sina nia ya kushika shilingi, lakini ninahitaji maelezo ya Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba yatakuja kama alivyosema kwenye hotuba kubwa.

Suala la *Bureau De Change* bado ni tatizo haswa kwenye hii mikoa yetu kama Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa hiyo, kwenye hilo suala la mtaji wa bilioni moja kwa sababu ile ni *spot transaction* haihitaji mtaji mkubwa hivyo na kuutunza pia mtaji wa bilioni moja kwa maana kwamba *seventy percent* kuilinda kwa mfanyabiashara wa kawaida bado ni *risk* sana, itahitaji labda polisi nao wawe wanakuwa wanapita kwenye maduka yote fedha.

Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri atuhakikishie kwa sababu kidogo kuna tafrani kule na imesababisha kumekuwa sasa na *black market* tayari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unataka Waziri akuhakikishie nini?

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba Sera hii sasa inaenda kurekebishwa huo mtaji uliowekwa na sera wa bilioni moja kwa biashara ile na iwe asilimia 70 *cash* hauko *realistic* kwa biashara hiyo tunavyoifahamu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, *actually* alishakuja mpaka ofisini kwa ajili ya wananchi wake pamoja ukanda mzima wa *corridor* ya utalii kusemea jambo hilo ofisini na nikiri kwamba tulikaa kikao ofisini kujadili jambo hilo. Nimuombe aridhie kwamba tumepokea hiyo hoja na tumepokea hizo *concern* na zina uzito na kwasababu ni jambo la kisera na ni jambo liko kwenye *powers* za *central bank* tunaendelea kufanyia kazi ndani ya ofisi na tutatoa majibu ambayo yatakuwa na manufaa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi tunayahitaji hayo maduka na hata wale waliokuwa wanafanya ndiyo watu ambao walishapata uzoefu kwenye sekta hiyo. Tunayahitaji na kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais amefanyakazi kubwa ya diplomasia ya kiuchumi masuala ya utalii yamefunguka sana. Hivi tunavyoongea hoteli nyingi zimeshajaa mpaka Desemba kwenye kanda ambazo ni za utalii. Kwa hiyo, wale watu wote watahitaji kubadilisha fedha tutaangalia kwa uzito hilo jambo alilolitoa ili kuweza kuweka mbele maslahi mapana ya Taifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo inasimamia mashirika ya umma ipo chini ya Wizara ya Fedha. Kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* ya sasa inaonesha kwamba mashirika ya umma yanadaiwa na wazabuni, wafanyakazi na wengine takribani shilingi trilioni 7.91 ambayo ni madeni muda mrefu. Ukiangalia kwenye ripoti ya *CAG* ya mwaka jana ilionesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2019/2020 mashirika ya umma yalikuwa yanadaiwa shilingi trilioni 6.8 sasa hivi yameongezeka mpaka shilingi trilioni 7.91. Sasa mimi nataka *clarification* tu sitaki *commitment* yoyote sitaki kuchukua mshahara wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka *clarification* ni kwa jinsi gani na mkakati upi ambao Serikali mnao wa kuhakikisha

kwamba haya madeni mnaya-*clear out* ili hawa wazabuni waweze kulipwa maana yake mwaka ilikuwa ni shilingi trilioni 6.8 sasa hivi shilingi trilioni 7.9 na hapo umeonesha kwenye hotuba yako zimetoka shilingi bilioni tu kulipa wazabuni. Nataka mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inamaliza haya madeni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kujibu na nimpongeze Mheshimiwa Matiko, bibi yangu kwa kuacha mshahara ule ili nyanya wake wakautumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ni kweli tumekuwa na madeni ya aina hiyo na Mheshimiwa Mbunge apongeze tu jitihada za Mheshimiwa Rais, unaweza ukaona kwamba tumeweza katika mwaka huu wa fedha kutumia mpaka *non cash bond* kwa ajili ya kulipa madeni ambayo yamekuwa makubwa ambayo yalikuwa yanaendelea. Tumetumia hiyo tukaweka *non cash bond* ya karibu shilingi trilioni 2.17 ambazo zilikuwa ni sehemu ya haya madeni makubwa makubwa.

Sasa kwa sasa hivi kwenye upande huu wa mashirika ya alikosema mashirika ya umma madeni haya ambayo yanadaiwa unaweza ukaona takribani kila mwaka tunatenga si chini ya shilingi bilioni 400 kwa ajili ya madeni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifanya ni kwa ajili ya ku-*balance* tu kwamba tulipe madeni, lakini pia huduma ambazo ni za muhimu kama nilivyotoa namba hizo na zenyewe ziweze kuendelea. Kwa hiyo tutaendelea ku-*balance* hivyo na baadhi ya madeni tumeshakubaliana ambayo yapo kwenye *cooperate* kuona namna ambavyo tunaweza tukafanya *offsetting,* lakini na zenyewe tunafanya kidogo kidogo ili mradi shughuli zingine za maendeleo kwa sababu kuna mahitaji ya muhimu ambayo hayawezi yakaahirishwa na yenyewe yaweze kuendelea.

Kwa hiyo hoja yake tumeipokea na tukikaa pembeni atanipa *details* mahususi ili tuweze kuhakikisha kwamba tunaongeza kasi hiyo ili tusiathiri shughuli za kiuchumi kwa sababu tunapolipa madeni mengine ni mitaji ambayo inakuwa *re-invested* na inaweza kutengeneza fursa kubwa zaidi za kiuchumi, nakushukuru.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye utaratibu wa kusoma mafungu yote kwa muda wetu uliobaki. Katibu!

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Fungu 50 jumla ya fedha inayoombwa ni shilingi 88,924,929,000.

**Fungu 050 – Wizara ya Fedha na Mipango**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*........................Sh. 10,505,104,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 1,514,118,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*...................Sh. 49,625,149,850
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*......................Sh. 1,584,344,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*...........................................Sh. 1,080,290,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*......................Sh. 1,158,007,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*.............................................Sh. 1,296,721,000
Kifungu 1010 – *Information and Communication Technology Unit*........................................Sh. 0
Kifungu 3001 – *Internal Auditor General*.........Sh. 7,129,184,400
Kifungu 5001 – *Government Asset Management Division*....................................Sh. 7,373,954,000
Kifungu 6001 – *Financial Management Information Systems Division*.......................Sh. 7,658,056,750

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 001 – Deni la Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................Sh. 9,093,984,694,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 007 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*........................Sh. 3,976,028,640
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 689,946,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*..........................Sh. 545,190,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*......................Sh. 722,342,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*................................................Sh. 310,600,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Unit*..........................Sh. 941,496,000
Kifungu 1007 – *Information, Education and Communication Unit* ..................Sh. 331,720,020
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*.......................Sh. 505,827,020
Kifungu 2001 – *Public Investment Management Division*.................................Sh. 30,214,279,736
Kifungu 3001 – *Privatization and Monitoring*.....Sh. 2,406,457,584
Kifungu 4001 – *Management Service Division*...................................Sh. 1,728,125,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 010 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Administration General*...........Sh. 2,082,592,000
Kifungu 1002 – *Internal Audit Unit*......................Sh. 155,690,000
Kifungu 1003 – *Finance and Accounts Unit*......Sh. 222,990,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*........................Sh. 21,430,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*...Sh. 95,400,000

Kifungu 2001 – *Technical Department*..............Sh. 260,130,000
Kifungu 2002 – Zanzibar Office ...........................Sh. 144,073,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 013 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*........................Sh. 1,748,721,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*......Sh. 136,590,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*..........................Sh. 14,520,000
Kifungu 1004 – *Monitoring Unit*............................Sh. 177,080,000
Kifungu 1005 – *Inspection Unit*...............................Sh. 148,550,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*...Sh. 49,735,000
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*.........................Sh. 403,510,000
Kifungu 1008 – *Management Info. System Unit*....Sh. 236,880,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda ukurasa wa 81 Fungu Namba 21 - Hazina Fungu hili lina mabadiliko ya Serikali na jumla inayoombwa sasa ni shilingi 2,126,873,518,000.

**Fungu 021 – Hazina**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 1,385,730,000
Kifungu 1009 – *Public Procurement Policy Unit (PPU)*..................................Sh. 1,815,500,000
Kifungu 2001 – *Government Budget Division* .............................Sh. 1,632,104,944,000
Kifungu 2002 – *Policy analysis Division*.........Sh. 420,697,370,000
Kifungu 4001 – *External Finance Division*.........Sh. 54,074,636,000
Kifungu 4002 – *Public Private Partnership Unit*..Sh. 1,755,682,000
Kifungu 5001 – *Financial Sector Development Division*......................................Sh. 4,272,483,647
Kifungu 6001 – *Debt Management Division*....Sh. 4,194,716,000

Kifungu 7001 – *Poverty Eradication Department* .............Sh. 0
Kifungu 8001 – *National Planning Division*......Sh. 6,572,456,353

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

**Fungu 022 – Huduma za Mfuko Mkuu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................Sh. 2,223,831,932,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu, kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3001 – *Public Debt Management*..........Sh. 785,726,600
Kifungu 3002 – *Expenditure Management*.....Sh. 4,381,140,000
Kifungu 3003 – *Financial Management*...........Sh. 27,543,273,400
Kifungu 3004 – *Financial Operations and Standards*...................................Sh. 6,109,930,000
Kifungu 3005 – *Sub Treasury Arusha*....................Sh. 363,920,000
Kifungu 3006 – *Sub Treasury Coast*........................Sh. 185,350,000
Kifungu 3008 – *Sub Treasury Iringa*..........................Sh. 193,445,000
Kifungu 3009 – *Sub Treasury Kagera*.......................Sh. 211,365,000
Kifungu 3010 – *Sub Treasury Kigoma*.....................Sh. 234,180,000
Kifungu 3011 – *Sub Treasury Kilimanjaro*.............Sh. 194,020,000
Kifungu 3012 – *Sub Treasury Lindi*...........................Sh. 224,690,000
Kifungu 3013 – *Sub Treasury Mara*.......................Sh. 194,530,0000
Kifungu 3014 – *Sub Treasury Mbeya*......................Sh. 184,940,000
Kifungu 3015 – *Sub Treasury Morogoro*...............Sh. 246,880,000
Kifungu 3016 – *Sub Treasury Mtwara*.....................Sh. 185,412,500
Kifungu 3017 – *Sub Treasury Mwanza*.................Sh. 184,770,000
Kifungu 3018 – *Sub Treasury Rukwa*.....................Sh. 184,880,000
Kifungu 3019 – *Sub Treasury Ruvuma*.....................Sh. 263,000,000
Kifungu 3020 – *Sub Treasury Shinyanga*.............Sh. 184,070,000
Kifungu 3021 – *Sub Treasury Singida*......................Sh. 185,210,000
Kifungu 3022 – *Sub Treasury Tabora*......................Sh. 180,570,000
Kifungu 3023 – *Sub Treasury Tanga*......................Sh. 207,415,000
Kifungu 3024 – *Sub Treasury Manyara*................Sh. 234,560,000

Kifungu 3025– *Sub Treasury Njombe*..................Sh. 238,230,000
Kifungu 3026 – *Sub Treasury Geita*.......................Sh. 184,910,000
Kifungu 3027 – *Sub Treasury Katavi*.....................Sh. 185,050,000
Kifungu 3028 – *Sub Treasury Simiyu*.....................Sh. 212,510,000
Kifungu 3029 – *Sub Treasury Songwe*..................Sh. 182,520,000
Kifungu 3030 – *Sub Treasury Dar es Salaam*.........Sh. 349,120,000
Kifungu 4001 – *Local Government Finances*.......Sh. 535,620,000
Kifungu 7001 – *Pension and Gratuity*.................Sh. 1,161,597,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Mkaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*...........Sh. 14,518,776,700
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 1,316,857,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*........................Sh. 359,607,000
Kifungu 1004 – *Ministerial Audit Division*..........Sh. 9,782,734,300
Kifungu 1005 – *Local Government Authorities Division*...................................Sh. 15,364,284,000
Kifungu 1006 – *Performance Audits Division*.....Sh. 3,874,646,450
Kifungu 1007 – *National Account Division*......Sh. 5,509,984,650
Kifungu 1008 – *Technical Support Service Unit*..........................................Sh. 7,247,251,100
Kifungu 1009 – *Public Authorities Audit Division*..................................Sh. 6,044,568,000
Kifungu 1010 – *Planning Monitoring, and Evaluation Division*.....................................Sh. 1,308,083,000
Kifungu 1011 – *Procurement Management Unit*.............................................Sh. 640,507,000
Kifungu 1012 – *Information and Communication Technology Unit*.....................Sh. 2,386,598,000
Kifungu 1013 – *Forensic Audit Unit*...................Sh. 3,367,209,000
Kifungu 1014 – *Quality Assurance Unit*...............Sh. 1,166,421,000
Kifungu 1015 – *Government Communication Unit*.............................................Sh. 386,798,000
Kifungu 1016 – *Risk Management and Compliance Unit*...............................................Sh. 137,075,500

Kifungu 1017 – *Legal Services Unit*......................Sh. 306,077,300
Kifungu 1018 – *Parliamentary Coordination Unit*...............................................Sh. 878,740,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 118,800,000
Kifungu 1003 – *Planning Unit*................................Sh. 414,090,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*.......................Sh. 151,750,000
Kifungu 1006 – *Information and Comm. Tech. Unit*...........Sh. 0
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*...........................Sh. 97,440,000
Kifungu 2001 – *Public Investment Management Division*......................................Sh. 256,500,000
Kifungu 3001 – *Privatization and Monitoring* ....Sh. 238,050,000
Kifungu 4001 – *Management Service Division* ....Sh. 313,370,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 013 – Kitengo cha Udhibiti Fedha Haramu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Unit*......................Sh. 470,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu, kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda ukurasa wa 25, Fungu Namba 21 Hazina, Fungu hili lina mabadiliko ya Serikali na hivyp basi fedha inayoombwa sasa ni shilingi 1,287,755,199,000.

**Fungu 021 – Hazina**

Kifungu 1009 – *Public Procurement Policy Unit (PPU)*....................................Sh. 485,375,000
Kifungu 2001 – *Government Budget Division*................................Sh. 822,096,854,000
Kifungu 2002 – *Policy and Analysis Division*...Sh. 459,137,511,000
Kifungu 4001 – *External Finance Division*...........Sh. 1,665,609,000
Kifungu 4002 – *Public Private Partnership Unit*..Sh. 2,820,000,000
Kifungu 5001 – *Financial Sector Development Division*........................................Sh. 749,850,000
Kifungu 6001 – *Debt Management Division* ......Sh. 500,000,000
Kifungu 8001 – *National Planning Division* .........Sh. 300,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko ya Serikali)*

**Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3003 – *Financial Management*..........Sh. 1,784,127,000
Kifungu 3004 – *Financial Operations and Standard*....................................Sh. 737,705,000
Kifungu 4001 – *Local Government Finances*.....Sh. 162,130,000
Kifungu 7001 – *Pension and Gratuity*.................Sh. 160,830,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 – *Adminstration and Human Resources Management Division.*..........Sh. 7,328,000,000
Kifungu 1010 – *Planning Monitoring, and Evaluation Division*....................................Sh. 3,598,935,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 050 – Wizara ya Fedha na Mipango**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*...........Sh. 1,700,000,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*.......................Sh. 19,191,059,000
Kifungu 1010 – *Information and Communication Technology Unit*..........................................Sh. 0
Kifungu 3001 – *Internal Auditor General*..............Sh. 760,000,000
Kifungu 5001 – *Government Asset Management Division*....................................Sh. 1,383,601,000
Kifungu 1006 – *Financial Mgt. Inform. Systems Division* ....................................Sh. 3,724,550,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake, naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge zima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, na sasa nitawahoji hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri lakini pia na Naibu Waziri na watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya na kwa kuisikiliza Kamati yetu ya Bunge, Kamati yetu ya Bajeti, kwa hiyo, na wao niwapongeze sana kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuishauri Serikali hasa kipindi hiki cha bajeti. Tunawapongeza Kamati yetu lakini pia tunawapongeza sana Wizara, kwamba yale ambayo mmekusudia kuyafanya Bunge limeyakubali na limeyapitisha.

Waheshimiwa Wabunge nichukue fursa hii kutangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Sasa tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa yale ambayo mmesema mnaenda kuyatekeleza ikiwa ni pamoja na yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyachangia hapa ndani na hamjapata fursa ya kujibu japokuwa tunafahamu kwamba mtaleta majibu mahsusi kwa maandishi, lakini tunaamini kwa namna ambavyo mnaisikiliza Kamati inavyofanya kazi kwa karibu nanyi mtafanya vivyo hivyo kwa yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema kwenu siku ya leo waliopata nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kuna mambo machache hapa; la kwanza kipindi cha maswali ya asubuhi nilikuwa nimemwambia Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu hapa kama alikuwa na majibu ya hilo swali lililoulizwa angeweza kujibu au ningempa fursa baadaye.

Sasa swali lililokuwa limeulizwa lilikuwa ni swali namba 343 la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Grace Tendega aliuliza swali la nyongeza; swali la msingi lilikuwa linahusu Vitambulisho vya Taifa halafu Mheshimiwa Tendega akauliza kuhusu Watanzania ambao wameenda huko walikoenda kwamba Serikali mbona haisemi jambo, maana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anafanya kazi nzuri, anawaweka watu pamoja, ameonana na viongozi mbalimbali wa upinzani pamoja na wengine sio viongozi lakini ameonana nao kwa nia njema. *(Makofi)*

Kwa hiyo, alikuwa anauliza Mheshimiwa Grace Tendega kwamba kwanini na hao wengine basi wasione sababu ya kurejea na pengine Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iseme jambo.

Kwa hiyo, nikasema kwasababu huwa linasemwa semwa na linarudi rudi hapa pamoja basi pamoja na kwamba lilikuwa nje ya lile swali la msingi basi Wizara itafute inachotaka kujibu kuhusu swali la Mheshimiwa Grace Tendega.

Kwa hiyo, nimeletewa taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri yupo tayari kujibu swali hilo na sasa nimpe fursa ya dakika chache aweze kulijibu hilo, swali halafu tumalize. Mheshimiwa Hamad Masauni. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ufafanuzi wa swali ambalo Mheshimiwa Tendega aliuliza leo asubuhi kuhusiana na kauli ya Serikali ya kuwataka Watanzania ambao wapo nje kurudi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kulieleza Bunge lako tukufu kuwa nchi yetu ipo salama na haina tishio lolote la usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wimbi la ongezeko kubwa sana la wawekezaji, Watanzania na wageni ni uthibitisho wa mazingira mazuri ya kiuchumi, kiusalama na kisiasa yaliyopo nchini. Hivyo nataka niwahakikishie Watanzania wote kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan tutaendelea kuhakikisha kwamba hali ya kisiasa, kiusalama na kiuchumi iliyopo nchini inaendelea kudumu kwa maslahi mapana ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika mara kadhaa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa dhamira ya kuimarisha mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kiusalama katika nchi yetu. Kwa upande wa hatua ambazo amewahi kuzichukua kwa uchache kiusalama ninyi ni mashahidi tumeona ongezeko la bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kiwango kikubwa kutoka shilingi bilioni 939 kufika zaidi ya shilingi trilioni 1.2 kwa mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya jitihada hizo za Mheshimiwa Rais ndio yamepelekea kuimarika kwa usalama katika nchi yetu pamoja na misingi ya sheria, haki za binadamu pamoja na utawala bora. Naomba pia nichukue fursa hii kuwahakikishia wananchi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuvisimamia vyombo vyake vya usalama ili viweze kutekeleza majukumu yake kwa misingi ya kisheria ili tu haki isitendeke, lakini ionekane kwamba imetendeka. Lakini kwa upande wa hatua za kiuchumi nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameeleza vizuri kwa kina sana juu ya hatua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika jitihada ambazo ningeomba nichukue fursa hii za kusisitiza kwa uchache, tumeona jitihada ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya ya kuimarisha diplomasia ya uchumi nchini, leo hii tunashuhudia

jinsi ambavyo Taifa letu limeweza kupungukiwa na mzigo mkubwa wa madeni kutokana na kazi kubwa ambayo ameifanya ya kuhakikisha kwamba anaimarisha mahusiano ya taasisi zenye kuweza kutoa mikopo yenye masharti nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Rais amefanya mabadiliko makubwa sana ya mfumo wa ukusanyaji wa kodi katika nchi hii jambo ambalo sio tu limeongezea imani, wigo, vyanzo na viwango vya kodi ambayo inakusanywa nchini. Mheshimiwa Rais amefanya jitihada kubwa vilevile katika kuhakikisha anaimarisha mazingira ya uwekezaji nchini kiasi cha kupelekea uwekezaji wa kiwango kikubwa katika nchi yetu. Lakini kwa upande wa kisiasa Mheshimiwa Rais amefanya jitihada nyingi sana kuimarisha mazingira ya kisiasa nchini.

Mheshimiwa Spika, mfano ameshakutana na viongozi wa upinzani kama ulivyosema mara kadhaa na mara zote hizo tumeshuhudia viongozi hao wakipongeza na kumsifia Mheshimiwa Rais hadharani kwa jitihada hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ameshakutana na viongozi wa siasa mmoja mmoja mfano amekutana na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama cha Maendeleo na Demokrasia - Mheshimiwa Freeman Mbowe mara tu baada ya kufutiwa mashtaka yaliyokuwa yakimkabili, lakini pia alikutana na Mheshimiwa Tundu Lissu - Makamu Mwenyekiti wa Chama cha CHADEMA nchini Ubelgiji baada ya Mheshimiwa Tundu Lissu kupelekea maombi hayo kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekutana pia na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo - Mheshimiwa Juma Duni, lakini Mheshimiwa Rais pia amekuwa akishiriki katika hafla mbalimbali za kijamii na za kibinafsi zinazohusiana na ama viongozi wa vyama vya kisiasa mfano alishiriki katika uzinduzi wa Taasisi ya Maalim Seif Sharif Hamad iliyofanyika kule Zanzibar na juzi alishiriki katika uzinduzi wa kitabu cha aliyekuwa Mbunge kupitia Chama cha CHADEMA Ndugu Sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia mbali ya kukutana na viongozi mmoja mmoja na kushiriki katika matukio yale, lakini Mheshimiwa Rais amekutana pia na viongozi wa vyama kwa ujumla wake, lakini pia Mheshimiwa Rais amekutana na Umoja wa Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni ambapo vilikuwa vikiongozwa na Mheshimiwa Zito Zuberi Kabwe Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo. *(Makofi)*

Katika hatua nyingine za kisiasa amekutana pia na Baraza la Vyama vyote vya Siasa ambapo alikuwa mgeni rasmi kwenye mkutano wao na ndipo kilipozaliwa kikosi kazi kinachoongozwa na Profesa Rwekaza Mukandala ambapo vikapelekea kuunda *task force* hiyo yenye uwakilishi kutoka taasisi mbalimbali ikiwemo taasisi za dini, wanasiasa, wanazuoni, asasi za kiraia, watu mashuhuri na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia dhamira ya taasisi hiyo ni kuweza kuratibu na kukusanya maoni ya wadau kuhusu demokrasia nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kupitia Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi ambayo Mheshimiwa Rais ndio Mwenyekiti wake, ilipelekea kuunda timu ya viongozi waliohusisha Chama cha Mapinduzi na Chama cha CHADEMA kwa lengo la kushirikiana kukabiliana na changamoto mbalimbali za kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba niseme machache; kwanza hakuna sababu yoyote kwa Mtanzania yeyote aliyepo popote pale ikiwemo viongozi hao wa CHADEMA walioko nje ya nchi kutokurejea nchini, ili sio tu waweze kutumia fursa nyingi ambazo nimezieleza za maendeleo hayo makubwa kiuchumi, kisalama na kisiasa yaliyopo, lakini kushiriki kikamilifu katika kutoa michango yao kwa maendeleo ya nchi yao katika nyanja zote kwani hapa ni nyumbani kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa sio kipindi cha maswali na majibu, kwa hiyo hakutakuwa na maswali ya nyongeza. *(Makofi)*

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi huo ulioutoa kwa swali lililokuwa limeulizwa na Mheshimiwa Grace Tendega. *(Makofi)*

Mambo machache la kwanza ni mchango wa Mheshimiwa Henry Nicodemas Maganga wakati akimalizia mchango wake, amesema hivi; "Mheshimiwa Spika, *yes* naomba kumalizia, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, maana nafasi ni ngumu sana kuzipata humu ndani, ahsante sana." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitoe ufafanuzi kidogo kwanza Mheshimiwa Maganga hii ni mara yake ya tano kuchangia, na ninayo orodha hapa mbele ambayo ipo hapa mbele siku zote kama ninavyosema kwa sababu nataka kuweka usawa kwa Wabunge humu ndani, kwa hiyo, Mbunge aliyechangia mara nyingi zaidi kuliko Wabunge wengine amechangia mara sita na hao Wabunge ambao wamechangia mara sita wako wanne, wengine wote wamechangia mara tano, wengine mara nne, wengine mara tatu, wengine mara mbili karibia wale wa mara moja ni wachache sana na ambao hawajachangia kabisa wapo, lakini ni wachache pia.

Kwa hiyo, orodha tunayo hapa mbele nafasi za kuchangia zinapatikana kama haukuzipata kwenye chama chama chako ukiandika hapa mbele na tukiona una sifuri ama una moja, utapewa nafasi usiwe na wasiwasi. Kwa hiyo, nimeona niliweke hilo sawa nafasi za kuchangia Bungeni zinapatikana. *(Makofi)*

Lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge ningependa kulisema leo kwa sababu ndio tumemaliza bajeti zote za kisekta, hii ilikuwa ni ya mwisho kabisa wakati tukisubiri Bajeti Kuu ya Serikali, nichukue fursa hii kuwapongeza sana sana Mawaziri wote, Naibu Mawaziri kwa ushirikiano wenu ambao

mmeutoa kwa Kamati zetu za Bunge, mmefanya kazi nao kwa karibu hatujapata malalamiko na mmekuwa mkihudhuria pia vikao vya Kamati kila mnapoitwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawapongeza sana Mawaziri kwa kuwepo kwenu kwenye hizo Kamati kwa sababu msipokuwepo huko basi mahusiano kidogo yanakuwa magumu na pia kusikiliza mawazo ya Wabunge inakuwa ngumu, kwa hiyo, ninawapongeza sana, sana, sana Mawaziri kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Naona Mheshimiwa Waziri wa Fedha anapiga sana makofi na wewe nikupongeze kwa sababu Waziri wa Fedha mara nyingi kipindi hiki anakuwa na pilika nyingi kwenye kujadili hapa na pale, akajadili na Benki ya Dunia, akajadili na *IMF,* basi kunakuwa ni kutafutana, lakini amejitahidi kuwepo muda mwingi nadhani Kamati ya Bajeti wanashuhudia hilo kwa hilo, kwa hiyo nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba ni kipindi kigumu kwako, lakini umejitahidi kutoa muda wako kusikiliza Kamati yetu ya Bajeti na Kamati nyingine ambazo zilikuwa zinahitaji uwepo wako, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia niwapongeze Wenyeviti wetu wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na Makamu wao, wamesimamia Kamati zetu vizuri zimeleta taarifa hapa kwa wakati na wote tunakubali mawazo kwa kweli waliyoyatoa yanaashiria kwamba wamefanya kazi nzuri, walitembelea miradi na wakarejesha hapa taarifa na sasa wametazama mawazo ya Serikali katika bajeti ijayo na wametueleza hapa ndani nini kinafanyika huko, kwa hiyo, viongozi wenzangu kwenye Kamati ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini pia niwapongeze Wajumbe sasa ambao ndio Wabunge ninyi kwa kazi nzuri sana mnayoifanya kwenye Kamati hadi mnalifanya Bunge lifanye kazi yake kwa ufanisi kwa sababu Kamati zenu zinafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, ninawapongeza sana Wabunge wote kwa kazi nzuri, nafahamu huwa kuna changamoto za hapa na pale huko kwenye Kamati, lakini kwa ujumla wake mambo yameenda

vizuri kwa hiyo ninawapongeza sana, na tutaendelea kujitahidi changamoto zile ambazo ni za kiutendaji tutaendelea kuzifanyia kazi ili Bunge liendelee kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Lakini pia niwashukuru sana watendaji wetu wa Bunge kwa maana ya Makatibu wa Kamati na watendaji wote chini ya Katibu wetu wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ambayo kwa kweli wametusaidia Kamati zetu kufanya kazi vizuri kwa ushauri wao na kwa kweli kufanya kazi kwa weledi mkubwa sana. Ninawapongeza sana Katibu wa Bunge pamoja na watumishi wote wa Bunge. *(Makofi)*

Vivyo hivyo niwapongeze pia watendaji kwenye Wizara zote ambazo nimeshazipongeza hapa na wao wamewasaidia Mawaziri kuleta hapa taarifa ambazo zinaonesha weledi wa hali ya juu hadi Wabunge wanakuwa na mambo machache tu ya kurekebisha hapa na pale kwa hiyo tunawapongeza sana pia watumishi wote ambao wanaongozwa na Makatibu Wakuu wa Wizara husika, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kwamba leo ni siku yetu ya mwisho kwa maana ya mijadala ya bajeti za kisekta, sasa kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 124 siku sita kuanzia siku ya kesho tutakuwa tukitumia Kanuni yetu ya 124 ambayo inatoa fursa kwa Kamati yetu ya Bajeti kukutana sasa na Serikali kwa yale mambo ambayo Serikali kipindi kile wanapojadili na Kamati yapo mambo ambayo wanakuwa hawajaafikiana na yapo mambo ambayo wanaendelea kushauriana.

Sasa hiki kipindi cha siku sita ndicho kipindi ambacho Kamati ya Bajeti na pamoja na Serikali wanayatazama mambo hayo yaliyotokana na taarifa za Kamati, lakini na mengine ambayo yalijitokeza humu ndani wakati wa mjadala, kuongeza hapa, kupunguza pale, basi mawazo hayo pia ni kipindi hiki yanatazamwa.

Kwa hiyo katika siku sita zijazo utaratibu wetu utakuwa kidogo tofauti kwa mujibu wa hii Kanuni ya 124 tutakutana hapa Wabunge wote asubuhi kama kawaida, halafu Kamati ya Bajeti itaenda kukutana na Serikali na kipindi hiki Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi wanakuwa ni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wenyeviti wote wanalazimika kuhudhuria Kamati ya Bajeti wakati wa kipindi hiki ili waweze kusema yale yaliyojitokeza kwenye Kamati zao waweze kuyaeleza kule kwenye Kamati ya Bajeti na baada ya siku sita sasa utaratibu utaendelea wa kawaida na haya yote ni maandalizi ya kusomwa kwa Bajeti Kuu. Bajeti Kuu inakuwa imetazama sasa mawazo yote yaliyotokea kwenye kipindi hiki tulichokuwa tunajadili bajeti za kisekta.

Kwa hiyo, kwa kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nimetoka hapa kumpongeza Waziri wa Fedha, lakini sasa nimtake Waziri wa Fedha na Naibu Waziri muwe na huo utayari katika hizi siku kuhudhuria siku zote kwenye Kamati yetu ya Bajeti wakati mtakapokuwa mnajadili yale mambo ya msingi kabisa ili muweze kutuletea sasa Bunge zima Bajeti Kuu ya Serikali na mimi nawatakia kila la heri Wenyeviti wote wa Kamati, lakini pia upande wa Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa ufafanuzi huo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 7.25 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 8 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*